

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

IDARA YA KISWAHILI

**MSHABAHA NA TOFAUTI KATI YA HADITHI FUPI YA
KISASA NA NGANO**

MISIGO DANIEL MWANZU

C50/ 32730/ 2015

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI
YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA SHULE
YA FANI NA SAYANSI ZA KIJAMII, CHUO
KIKUU CHA KENYATTA**

MACHI, 2021

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.


Sahihi: ~~MISIGO~~ Tarehe: 25/3/21

MISIGO DANIEL MWANZU

NAMBARI YA USAJILI: C50/ 32730/ 2015

WASIMAMIZI;


Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi:  Tarehe: 29/3/2021

DKT. RICHARD MAKHANU WAFULA

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu Cha Kenyatta

Sahihi:  Tarehe: 30/3/2021

DKT. JOSEPH JESSEE MURITHI

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu Cha Kenyatta

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu Richard Imbambi Misigo na Roselyne

Nyaroya kwa kunifaa kwa hali na mali.

SHUKRANI

Kwanza, namshukuru Mola kwa kunipa uwezo na kunijalia nguvu za kufanya kazi hii. Neema na rehema zake zimefanya kazi hii kukamilika.

Aidha, nawashukuru kwa dhati wasimamizi wangu Dkt. Richard Wafula na Dkt. Jessee Murithi kwa kunitia hamasa ya kutia bidii ili kukamilisha kazi hii. Wosia wenu, mapendekezo na mwongozo katika kila hatua niliyopiga hadi kufika kiwango hiki. Asanteni sana na Mungu mwenye neema awabariki.

Nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili kwa kunitia shime katika masomo yangu. Aidha, siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu tulioshirikiana nao katika masomo na mjadala. Hawa ni pamoja na Melvin, Jackline, Ndungu, Simiyu, Macharia, Lawi, Hezron na Steve. Nawashukuru nyote kwa kurahisisha safari yangu ya kiusomi na kunifaa kwa njia moja au nyingine. Rabuka awabariki kwa wema wenu.

Mwishowe, nawashukuru mwalimu mkuu Simon Mburu na naibu mwalimu mkuu Titus Gachuhi kwa kufanya utafiti wangu kuwa mwepesi. Mola awabariki. Hali kadhalika, siwezi kuwasahau walimu wenzangu ikiwemo Felister Chepkoech na Douglas Mureithi kwa kunipa mshawasha kuendelea na utafiti huu.

IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia mshabaha na tofauti kati ya hadithi fupi ya kisasa na ngano. Diwani zilizoshughulikiwa ni: *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* (Sanja, 2011), *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (Mbatiah, 2007) na *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* (Mc Onyango, 2006). Hali kadhalika, ngano zilizoshughulikiwa zimo katika vitabu vya *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* (Steere, 1870) na *Myths and Legends of the Swahili* (Knappert, 1970). Utafiti ulilenga kuchanganua muundo, mtindo, maudhui na wahusika katika hadithi fupi ya kisasa na ngano. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya vikale iliyoasisiwa na Jung ama Frazer na kuimarishwa katika fasihi na Northrop Frye (1957) na baadaye ikaendelezwa na Campbell (2004), Guerin (2005) na Larsen (2018). Kulingana na Frye, kikale ni ishara ambayo huzua taswira inayojirudiarudia katika kazi ya sanaa kiasi kwamba inatambuliwa kama kiungo cha ujuzi wa mtunzi wa kazi fulani. Nadharia hii imeteuliwa kwa msingi kuwa ilituwezesha kuonyesha ikiwa taswira zinazojitokeza katika hadithi fupi zinasheheni picha kongwe zinazojirudiarudia mara kwa mara kama ilivyo katika ngano. Kwa msingi huu tumebaini kuwa kuna vigezo tofauti vya kupimia kazi za hadithi fupi na ngano. Aidha, utafiti huu umefanyika katika maktaba za vyuo vikuu nchini Kenya. Data ya kimsingi imepatikana kutokana na kusoma diwani ya hadithi fupi, ngano zilizomo katika vitabu vya Steere na Knappert, tasnifu, majarida na vitabu vinavyohusiana na mada ya utafiti. Data imechanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya kimaelezo na lugha ya nathari kuambatana na malengo ya utafiti. Utafiti huu umeonyesha kuwa kuna tofauti nyingi kati ya hadithi fupi ya kisasa na ngano kuliko mshabaha. Hii inathibitisha kuwa hakuna hadithi fupi iliyotokana na ngano.

ABSTRACT

This research aimed at analyzing the similarities and differences between modern short stories and folktales. The researcher used three collections of short stories by different authors. The selected collections are: *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* (Sanja, 2011), *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (Mbatiah, 2007) and *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* (Mc Onyango, 2006). The research also analysed folktales obtained from two books titled: *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* (Steere, 1870) and *Myths and Legends of the Swahili* (Knappert, 1970). This research aimed at analysing the structure, style, themes and characters of folktales and modern short stories. The researcher employed archetype theory. This theory was invented by Jung or Frazer and reinforced in literature by Northrop Frye (1957) and later modified by Campbell (2004), Guerin (2005) and Larsen (2018). According to Frye, archetypes are symbols that bring about recurring images in literary works in that they are recognized as the basis of identifying such works. The researcher chose this theory on the basis that it enabled him to know if archetypal images are exhibited by short stories just like in folktales. Through this the researcher found out that there are different parameters of identifying short stories and folktales. This research was done in libraries of universities found in Kenya. The researcher analysed the chosen short stories, folktales present in books of Steere and Knappert, thesis, journals and other relevant materials related to our research problem. The data was analysed and presented according to research objectives. This research showed that there are a lot of differences between folktales and modern short stories than similarities. This proves that no short story originated from a folktale.

UFAFANUZI WA ISTILAHU

- Kikale:** Ni taswira inayojitokeza mara kwa mara katika kazi ya kifasihi.
- Kimelea:** Ni dhana inayotumiwa kuonyesha kuwa utanzu mmoja ulitokana na mwingine. Katika muktadha huu unamaanisha kuwa utanzu wa hadithi fupi ulitokana na ngano.
- Motifu:** Ni kipengele cha kimuundo, kimaudhui, wahusika na kimtindo kinachorudiwarudiwa katika kazi ya fasihi ili kutoa ujumbe fulani.
- Nadharia ya vikale:** Ni nadharia iliyoasisiwa na Jung ama Frazer (1890- 1915) na kuimarishwa katika fasihi na Northrop Frye (1957) na kuendelezwa na Campbell (2004), Guerin (2005) na Larsen (2018).

VIFUPISHO

Uk.:

Ukurasa

YALIYOMO

IKIRARI	ii
TABARUKU.....	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI	v
ABSTRACT.....	vi
UFAFANUZI WA ISTILAH.....	vii
VIFUPISHO	viii
YALIYOMO.....	ix
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI.....	1
1.1 Usuli wa Mada	1
1.2 Suala la Utafiti.....	3
1.3 Malengo ya Utafiti	4
1.4 Maswali ya Utafiti.....	5
1.5 Sababu za Kuchagua Mada	5
1.6 Upeo na Mipaka	7
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.....	7
1.8 Misingi ya Nadharia	15
1.8.1 Mihimili ya Nadharia ya Vikale	18
1.9 Mbinu za Utafiti	20
1.9.1 Muundo wa Utafiti	21
1.9.2 Mahali pa Utafiti.....	21
1.9.3 Uteuzi wa Sampuli.....	21

1.9.4 Ukusanyaji wa Data.....	23
1.9.5 Uchanganuzi wa Data.....	23
1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo	23
1.9.7 Maadili ya Utafiti.....	24
1.9.8 Changamoto za Utafiti.....	24
1.9.9 Hitimisho	25
SURA YA PILI: MUUNDO NA MTINDO WA NGANO NA HADITHI FUPI YA KISASA YA KISWAHILI	26
2.0 Utangulizi	26
2.1 Dhana ya Muundo	26
2.2 Muundo wa Ngano na Hadithi Fupi.....	28
2.2.1 Mwanzo	28
2.2.2 Sehemu ya Kati.....	32
2.2.3 Mwisho	35
2.3 Dhana ya Mtindo.....	44
2.4 Mtindo wa Ngano na Hadithi Fupi.....	45
2.4.1 Urudiaji wa Maneno, Vishazi, Vifungu na Matukio	45
2.4.2 Mtindo wa Nambari.....	53
2.4.3 Safari na Msako	58
2.4.3.1 Safari.....	58
2.4.3.2 Msako	58
2.4.3.3 Motifu	59
2.4.3.4 Motifu ya Msako na Safari	60
2.5 Hitimisho.....	67

SURA YA TATU: MAUDHUI YA NGANO NA HADITHI FUPI YA	
KISASA YA KISWAHILI	68
3.0 Utangulizi	68
3.1 Dhana ya Maudhui	68
3.2 Maudhui ya Ngano na Hadithi Fupi.....	68
3.2.1. Maudhui ya Wema na Uovu.....	69
3.2.2. Maudhui ya Ujanja	76
3.2.3. Maudhui ya Ushujaa.....	82
3.2.4 Maudhui ya Mauti (Kifo)	88
3.3. Hitimisho.....	94
SURA YA NNE: WAHUSIKA WA NGANO NA HADITHI FUPI YA	
KISASA YA KISWAHILI	96
4.0 Utangulizi	96
4.1 Wahusika wa Ngano na Hadithi Fupi	96
4.1.1 Wahusika Wajanja.....	96
4.1.2. Wahusika Katili	102
4.1.3 Wahusika Mashujaa.....	109
4.1.4 Wahusika Majahili (Wakinzani wa Nguli).....	114
4.1.5 Wahusika Wema.....	117
4.2 Hitimisho.....	120
SURA YA TANO: HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO YA	
UTAFITI.....	123
5.0 Utangulizi	123
5.1 Muhtasari.....	123

5.2 Matokeo ya Utafiti kwa Mujibu wa Malengo	125
5.3 Mapendekezo	129
5.4 Hitimisho	130
MAREJELEO	131

SURA YA KWANZA UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Fasihi ni sanaa maalumu ya matumizi ya lugha inayohusiana na tungo za kisanaa kama vile: mashairi, riwaya, tamthilia, tenzi, misemo, vitendawili, hadithi, ngano na methali (Kingei na Kisovi, 2005). Tungo hizi huwasilishwa kwa maneno teule ambayo yanaweza kuandikwa au kusimuliwa. Baadhi ya tanzu za fasihi andishi kama vile riwaya na hadithi fupi zimenasibishwa na tanzu za fasihi simulizi kama vile ngano. Hii ni kwa sababu tanzu za riwaya na hadithi fupi zimeonyesha ukuruba wa moja kwa moja na ngano. Riwaya za kale kama kazi za Shabaan Robert za *Kufikirika* (1946) na *Kusadikika* (1951) zina mianzo na miishio maalum kama ngano za kiasili zinazotumia “paukwa wakaishi raha mustarehe.” Matteredu (2003) anasema:

Amezifanya (Shabaan Robert) riwaya zake ziachane na wakati wa kuzifanya ni za kale wakati zinapojadili mambo ya wakati uliopo. Hii ni hali iliyomo katika fasihi simulizi (Uk. 35).

Mukopi (2005) anaeleza kuwa tanzu zingine za fasihi simulizi zinafanana na hadithi fupi za Kiswahili. Hii ni kwa sababu tanzu hizi ni fupi na zinatumia lugha ya nathari. Kutokana na haya, kumeibuka mitazamo miwili kuhusu chimbuko la hadithi fupi.

Mtazamo wa kwanza wa wahakiki unasisitiza kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ni zao la mchakato wa kistari kutoka kwa ngano hadi kwa hadithi fupi. Baadhi ya wahakiki wanaoshikilia mtazamo huu ni Sengo (1982), Senkoro (1982),

Msokile (1992), Mohochi (1995) na Wamitila (2002). Wahakiki hawa wanaeleza kuwa baadhi ya sifa za hadithi fupi kama vile: tukio moja, lugha ya nathari, mwanzo na mwisho wake, uwili wa wahusika wake na ufupi wake zinapatikana katika ngano. Ndiposa Wamitila (2002), anaeleza kuwa ngano ndicho kiwango cha chini cha hadithi fupi. Hali kadhalika, Timammy na Swaleh (2013) wanaongezea mawazo haya kwa kusema kuwa hadithi fupi ilitokana na ngano. Aidha, Timammy na Swaleh (2013) wanaeleza kuwa mitindo inayobainika kwa uandishi wa hadithi fupi ya kisasa ni sawia na ile ya ngano.

Mtazamo wa pili unashikilia kuwa kila utanzu wa kifasihi una asili yake kivyake. Mtazamo huu unashikiliwa na Wellek na Warren (1976), Mukopi (2005) na Chemutai (2016). Wellek na Warren (1976) wanaeleza kuwa kila utanzu wa kifasihi uliibuka kivyake. Wataalam hawa japo walikuwa na mtazamo kuwa kila utanzu una asili yake walipuuza dhana ya mwingiliano matini. Walipuuza dhana kuwa tanzu mbalimbali huingiliana. Aidha, maoni yao yanatofautiana na maoni ya Mbatiah (2016) ambaye anaeleza kuwa utanzu wowote wa fasihi andishi unafaa kutilia maanani chimbuko lake katika fasihi simulizi. Naye Mukopi (2005), anaeleza kuwa hadithi fupi sio zao la mchakato wa kistari kutoka kwa ngano hadi kwa hadithi fupi. Anaeleza kuwa hadithi fupi ilitokana na ujuzi wa uandishi na sifa zinazotokana na mbinu za usimulizi. Kwa msingi huu, mwandishi anaweza kutumia ubunifu wake na kutunga hadithi bila kujua ngano za hapo awali. Mukopi anaungwa mkono na Chemutai (2016) anapoeleza kuwa utanzu wa ngano hauwezi kulinganishwa na hadithi fupi za kisasa kwani utanzu wa hadithi fupi ulichipuka

baada ya tanzu nyingine za fasihi. Hali kadhalika, anabaini kuwa hadithi fupi ya kisasa ina muundo changamano ilhali ngano ina muundo sahili.

Ijapokuwa kuna mitazamo miwili kuhusu asili ya hadithi fupi ya Kiswahili, wataalamu husika hawajaunga mkono maoni yao kwa utafiti wa kina kuonyesha ikiwa kuna uhusiano wa kistari baina ya hadithi fupi ya kisasa na ngano. Tafiti zao pia hazijaonyesha tofauti mahususi baina ya ngano na hadithi fupi. Hali kadhalika, wataalamu hawa hawakufuatilia kwa makini fasihi ya kimagharibi kuhusu asili ya hadithi fupi iliyoanzishwa na Edgar Poe (1809-1849). Poe aliandika hadithi fupi kama vile: *The Pit and Pendulum* (1842), *Black Cat* (1843), *Premature Burial* (1844), *The Tell-Tale Heart* (1843) na *Mask of Red Death* (1842).

1.2 Suala la Utafiti

Kumekuwa na mitazamo miwili kuhusu chanzo cha hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili. Mtazamo wa kwanza unaeleza kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ni kimelea cha ngano. Baadhi ya wataalam wanaoshikilia mtazamo huu ni kama vile: Sengo (1982), Msokile (1992), Mohochi (1995) na Wamitila (2002). Kwa upande mwingine, mtazamo wa pili unashikilia kuwa kila utanzu wa kifasihi una asili yake kivyake. Mtazamo huu kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ina asili yake kivyake unashikiliwa na wataalam kama vile: Mukopi (2005) na Chemutai (2016). Hata hivyo, wataalam husika wa mitazamo hii miwili hawajaunga mkono maoni yao kwa utafiti wa kina kuonyesha ikiwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ni kimelea cha ngano. Tafiti zao pia hazijaonyesha tofauti mahususi baina ya ngano

na hadithi fupi. Utafiti huu umefidia pengo hili kwa kuchanganua miundo, wahusika, mtindo na maudhui ya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili na ngano. Uchanganuzi huu umelenga kubainisha sifa za kimuundo, kimtindo, kimaudhui na wahusika zinazojitokeza katika baadhi ya ngano na hadithi fupi. Mtafiti amechanganua hadithi fupi zinazoonyesha sifa zinazokaribiana na ngano na zile zinazoonyesha sifa tofauti na ngano. Hali kadhalika, amechanganua ngano teule. Kutokana na sifa hizi, mtafiti alibainisha kuwa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zina sifa tofauti na zile zinazojitokeza mara kwa mara katika ngano. Kwa kufanya hivi, tumebainisha kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ni utanzu ulioibuka kivyake. Diwani zilizoshughulikiwa ni: *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* (2011), *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007) na *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* (Mc Onyango, 2006). Hali kadhalika, mtafiti alichanganua ngano zilizomo katika vitabu vya *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* (1870) na *Myths and Legends of the Swahili* (1970).

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na malengo yafuatayo:

- 1) Kubainisha namna mbalimbali miundo hujitokeza katika ngano na hadithi fupi.
- 2) Kujadili mitindo mbalimbali inayojitokeza katika ngano na hadithi fupi.
- 3) Kujadili maudhui yanayoshughulikiwa katika ngano na hadithi fupi.

- 4) Kufafanua wahusika mbalimbali wanaopatikana katika ngano na hadithi fupi.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

- 1) Miundo ya ngano na hadithi fupi hujitokeza vipi?
- 2) Mitindo ya ngano na hadithi fupi hujitokeza vipi?
- 3) Ni maudhui yepi yanayoshughulikiwa katika ngano na hadithi fupi?
- 4) Ni wahusika wepi wanaopatikana katika ngano na hadithi fupi?

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Wahakiki wengi wanahitilafiana kuhusu uhusiano wa ngano na hadithi fupi. Kuna wale wanaoshikilia kuwa hadithi fupi ya kisasa ni kimelea cha ngano (Mohochi 1997, Senkoro 1982 na Timammy na Swaleh 2013). Kwa upande mwingine, kuna wale wanaoshikilia kwamba kila utanzu wa fasihi uliibuka kivyake (Wellek na Warren 1976, Mukopi 2005 na Chemutai 2016). Utafiti huu umechaguliwa ili kujaribu kusuluhisha mgogoro huu kwa kulinganisha na kulinganua sifa za kimtindo, kimaudhui, wahusika na kimuundo baina ya hadithi fupi za kisasa za Kiswahili na ngano.

Hadithi fupi ni utanzu unaoendelea kuimarika kwa haraka sana tangu mwaka wa 2000 hadi 2017. Zaidi ya mikusanyiko kama kumi na mitano hivi imetokea na kuchapishwa. Hii mikusanyiko inazidi mikusanyiko ya awali ya kati ya mwaka 1967 hadi 1999. Utanzu unaoendelea hivi unapaswa kusomwa na kuhakikiwa ili

sifa zake za kisanaa zibainike kwa wote wanaosoma. Ndiyo maana mtafiti huyu anataka kutoa mchango katika usomi wa hadithi fupi.

Walimu ni washikadau muhimu katika maisha ya wanafunzi. Hii ni kwa sababu walimu ndio huelimisha wanafunzi. Walimu katika shule ya upili hufunza sifa za hadithi fupi na ngano. Utafiti huu umewapa walimu mwanga zaidi kuhusu sifa hizi.

Isitoshe, mtafiti amechagua utafiti wake kwa misingi kuwa diwani alizochagua ni za karne ya ishirini na moja na zinasheheni maudhui ya kisasa. Diwani za *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* (2011), *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007) na *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* (2006) zinaafiki kuitwa diwani zinazosheheni hadithi fupi za kisasa za lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu hadithi zilizoko katika diwani hizi zimeandikwa katika karne ya ishirini na moja na zinasheheni maudhui ya kisasa.

Steere ni miongoni mwa wataalamu wachache wa kigeni waliochangia fasihi ya Kiswahili. Wataalam wengine wa kigeni waliochangia fasihi ya Kiswahili ni kama vile: Fredrick Johnson, Johann Rebmann na Ludwig Krapf. Steere aliandika kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* mnamo 1870 ilhali Knappert alihariri kitabu cha *Myths and Legends of the Swahili* mnamo 1970. Isitoshe, watunzi hawa hawajashughulikiwa hivi karibuni kwa kina kwa kulinganishwa na waandishi wenyeji wa Kiswahili. Utafiti huu umewafufua wataalam hawa kwa kulinganisha na kulinganua ngano walizokusanya na hadithi fupi zilizohaririwa na wataalam wa kisasa.

1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu umejikita katika kuchanganua hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ili kubainisha ikiwa ni kimelea cha ngano. Tumefanya hivi kwa kuchanganua muundo, mtindo maudhui na wahusika katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili na ngano. Uchanganuzi huu umethibitisha kuwa sifa za kimuundo, kimtindo, kimaudhui na wahusika zinazojirudia katika ngano ni tofauti zile za hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili. Hadithi fupi zilizoshughulikiwa zimo katika diwani za *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007) iliyohaririwa na Mbatiah na *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* (2011) iliyohaririwa na Sanja. Aidha, mtafiti alichagua hadithi ya “Waliohujumu Ujamaa” iliyomo katika diwani ya *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* (2006) iliyohaririwa na Mc Onyango. Isitoshe, mtafiti ameangazia ngano zilizomo katika vitabu viwili. Vitabu hivyo ni: *Myths and Legends of the Swahili* (1970) na *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* (1870). Hali kadhalika, utafiti huu umejiegemeza kwenye nadharia ya vikale.

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Mengi yameandikwa kuhusu ngano na hadithi fupi za Kiswahili kwa mfano: Senkoro (1982), Mohochi (1995), Mukopi (2005) na Muusya (2012). Aidha, kuna tahakiki zilizofanywa kuhusu sifa za ngano na hadithi fupi. Tumedurusu baadhi ya tahakiki hizi kwa malengo ya kuzilinganisha na kuzitofautisha na kazi yetu. Senko (1982) ameshughulikia suala la hadithi fupi kwa jumla. Amechanganua jinsi utanzu huu unavyotofautiana na tanzu zingine za fasihi andishi. Amezungumzia sifa za

hadithi fupi kama vile aina ya wahusika ambao ni wachache. Anadai kuwa muundo wa hadithi fupi umetokana na muundo wa ngano za hapo awali. Tofauti na yeye, utafiti wetu haujazingatia jinsi hadithi fupi inatofautiana na tanzu za fasihi andishi bali ulizingatia jinsi inatofautiana na ngano ambayo ni utanzu wa fasihi simulizi. Hata hivyo, utafiti wake ulikuwa wa manufaa kwetu kwani umetupa mwanga zaidi kuhusu sifa za hadithi fupi.

Senkoro (1982) ameshughulikia utanzu wa hadithi fupi. Anaeleza kuwa utanzu wa hadithi fupi ulizuka kutoka kwa ngano za hapo awali. Isitoshe, anaongezea kuwa mandhari ya hadithi fupi huwa ya wazi. Hali kadhalika, hadithi fupi huwa na wahusika wachache. Utafiti wa Senkoro ulikuwa wa manufaa kwetu kwani umetuwezesha kuchambua umbo la ngano na hadithi fupi na kubaini ikiwa ni tofauti au la. Utafiti huu ni tofauti na wa Senkoro kwani hatujachambua tu muundo na wahusika wa hadithi fupi na ngano bali pia maudhui yanayojitokeza.

Mohochi (1995) ameeleza kuhusu fani katika hadithi fupi kwa mapana. Katika kazi yake ameeleza kuwa utanzu huu huwa na wahusika wachache kuliko wa riwaya. Aidha, amebaini kuwa utanzu wa hadithi fupi huelezea tukio moja tu. Isitoshe, ameeleza kuwa hadithi fupi ni zao la mchakato wa kistari kutoka kwa ngano hadi kwa hadithi fupi. Utafiti wake umetupa mwanga zaidi kuhusu fani katika hadithi fupi. Hata hivyo, tofauti naye utafiti huu haukuzingatia kipengele cha fani peke yake bali pia maudhui. Hali kadhalika, tumechanganua maudhui, wahusika, muundo na mtindo katika ngano na kulinganisha na hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili. Ulinganifu huu umenuia kuthibitisha ikiwa maoni ya Mohochi kuwa

hadithi fupi ni zao la mchakato wa kistari kutoka kwa ngano hadi kwa hadithi fupi ni kweli.

Mohochi (1997) katika makala kuhusu “Hadithi Fupi: Utanzu Uliodharauliwa” anasema kuwa:

Jamii nyingi zimekuwa na hadithi fupi katika masimulizi ya mdomo na hatimaye katika maandishi. Ngano ndiyo aina ya fasihi ambayo ina historia ndefu katika jamii (Uk. 63).

Mohochi anashikilia kuwa historia ya hadithi fupi imejengeka kutoka kwa ngano za kale. Anaeleza kuwa hadithi hizi zilinasibishwa na utamaduni wa jamii. Mohochi anatambua kuwa muda huu wote, hadithi fupi zimesimuliwa kwa minajili ya kukashifu matendo maovu na kuburudisha. Utafiti wake umetusaidia kuelewa historia ya hadithi fupi. Tofauti ni kuwa Mohochi (1997) hathibitishi madai yake kwa utafiti wa kina kuhusu historia ya hadithi fupi kujengeka kwa ngano. Utafiti huu umefidia pengo hili kwa kuchanganua miundo, mtindo na maudhui ya ngano na hadithi fupi. Uchanganuzi huu umelinganisha na kulinganua vipengele hivi vya ngano na hadithi fupi ili kuthibitisha maoni ya Mohochi.

Kimani na Chimerah (1999) wamezungumzia uhusika, usimulizi na dhamira katika ngano. Wanaeleza kuwa dhamira kuu ya ngano ni kuerevusha binadamu ili wasipatwe na maafa. Wamechanganua pia vipengele vya chuku, taswira, nyimbo, matumizi ya nyimbo na sentensi fupifupi katika ngano. Uchambuzi wao umetupa mhimili mzuri katika kuelewa dhamira na baadhi ya fani katika ngano. Utafiti wao ulishughulikia tu ngano. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na utafiti wa Kimani na

Chimerah (1999) kwani tumechambua pia hadithi fupi. Hali kadhalika, uchambuzi huu umezingatia pia maudhui mbalimbali, wahusika na miundo ya ngano na kuilinganisha na hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.

Wamitila (2002) anaelezea jinsi utanzu wa hadithi fupi ulivyoendelea hadi sasa. Ameangazia hadithi fupi kwa kuzingatia sifa ya ufupi, wahusika ambao ni wachache na mandhari inayobainika wazi. Amedai kuwa hadithi fupi ni zao la mchakato wa kistari kutoka kwa ngano hadi kwa hadithi fupi. Kazi ya Wamitila haina ushahidi wa kutosha ili kuthibitisha madai haya. Utafiti huu umefidia upungufu huu kwa kuweka wazi sifa za ngano na hadithi fupi ili kuthibitisha madai yake.

Wamitila (2003) amejadili sifa mbalimbali za ngano na hadithi fupi. Baadhi ya sifa za hadithi fupi alizozitaja ni: wahusika wachache, ufupi, kipindi kifupi cha wakati, mandhari ambayo si pana na mgogoro kukuzwa mapema. Hali kadhalika, amejadili sifa za ngano kama vile: urudiaji na uwili wa wahusika. Kazi yake imetupa mwanga zaidi kuhusu sifa za hadithi fupi na ngano. Hata hivyo, utafiti huu umelenga zaidi ya kueleza sifa hizo kwani tumezilinganisha ili kubaini ikiwa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili ni kimelea cha ngano.

Matteru (2003) katika makala yake ya “Fasihi Simulizi na Uandishi wa Kiswahili” amebaini kuwa Shabaan Robert amezifanya hadithi zake kutumia nyakati za kale wakati wa kujadili mambo ya wakati uliopo. Anaeleza zaidi kuwa hali hii ni sawa katika fasihi simulizi. Utafiti wake umekuwa nguzo katika mjadala kati ya wakati

wa ngano na hadithi fupi katika utafiti wetu. Utafiti wake hauonyeshi kinaganaga iwapo Shabaan Robert alitumia ngano katika hadithi zake.

Mukopi (2005) ametafiti kuhusu Hadithi Fupi za Kisasa za Kiswahili kama Utanzu Mahuluti. Ameangazia diwani tatu. Nazo ni: *Pendo la Heba* (1997), *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000) na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004). Akitumia nadharia ya mwingiliano matini amebaini kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili sio mwendelezo wa kistari kutoka kwa ngano hadi kwa hadithi fupi bali ni mwingiliano kati ya sifa za usimulizi na sifa za uandishi. Ametaja baadhi ya sifa kama vile: monolojia, upenyezi wa mwandishi mwenyewe, matumizi ya baadhi ya semi na kukatiza sentensi. Utafiti wa Mukopi umekuwa wa manufaa kwetu kwani umetupa mwanga zaidi kuhusu sifa za uandishi na usimulizi katika hadithi fupi. Utafiti wa Mukopi umelenga kubainisha jinsi hadithi fupi za kisasa za Kiswahili ni mwingiliano baina ya sifa za usimulizi na sifa za uandishi. Tofauti naye, utafiti huu umelenga kuonyesha mshabaha na tofauti kati ya ngano na hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.

Wamitila (2008) ameangazia maana ya hadithi fupi, nadharia ya hadithi fupi na sifa za hadithi fupi. Baadhi ya sifa anazozitaja ni: ubanifu, uanzaji wa hadithi, utamatishaji wa hadithi, umoja, usimulizi na mandhari. Kazi yake imetupa mwanga zaidi kuhusu sifa za hadithi fupi. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na wetu kwani tumechanganua pia sifa za ngano na kuzilinganisha na zile za hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.

Senkoro (2011) katika utafiti wake amegundua kuwa wahusika wa fasihi simulizi huwa na sehemu mbili kuu: sehemu ya wema na sehemu ya uovu, sehemu ya haki na sehemu ya uonevu. Ameeleza kuwa baadhi ya waandishi wanawasawiri wahusika wao kwa kuzingatia sehemu hizi mbili kuu. Utafiti wa Senkoro ulitufaa katika kuelewa zaidi kipengele cha wahusika katika ngano na hadithi fupi. Hata hivyo, tofauti na Senkoro utafiti wetu haujazingatia fasihi simulizi kijumla. Mtafiti amezingatia wahusika wa ngano na kuwalinganisha na wale wa hadithi fupi ya Kiswahili ili kubaini ikiwa waandishi hao wa hadithi fupi wameathiriwa na baadhi ya ngano katika uundaji wao wa wahusika.

Muusya (2012) ametafiti kuhusu mandhari katika hadithi zinazopatikana katika diwani mbili za Kiswahili. Diwani hizi ni: *Pendo la Heba na Hadithi Nyingine* na *Mizungu ya Nabii na Hadithi Nyingine*. Amegundua kuwa waandishi wa hadithi fupi husawiri mandhari iliyojikita katika eneo moja. Ameeleza kuwa mandhari hii haibadiliki na ikibadilika ni kwa kiwango kidogo tu. Ugunduzi wake umetupa mwanga zaidi kuhusu mandhari ya hadithi fupi. Tofauti na utafiti wake, utafiti huu haukujiegemeza tu katika mandhari bali pia vipengele vingine kama vile maudhui na wahusika.

Kenguru (2013) ameshughulikia athari ya fasihi simulizi katika riwaya ya *Utubora Mkulima* kwa kutumia nadharia ya vikale. Amebaini kuwa waandishi wengi akiwemo Shabaan Robert wamechota vipengele vya wahusika, mbinu na maudhui kutoka kwa fasihi simulizi. Ameeleza kuwa fasihi andishi ni kimelea cha fasihi simulizi. Hivi kwamba waandishi kama vile Shaaban Robert wasingefuzu

kujitokeza kama waandishi wa vitabu kama si kutokana na hadithi za akina bibi. Hali kadhalika, amebaini kuwa Shabaan Robert anazungumzia maudhui ya wema na uovu, haki, bidii, heshima na uhusiano. Kijumla, ameeleza kuwa uandishi wa Shabaan Robert umeathiriwa na fasihi simulizi kwa kuzingatia: usimulizi maizi, wahusika, miishio ya hadithi na umuhimu wake katika jamii. Utafiti wa Kenguru umekuwa wa manufaa kwetu kwani ulitupa mwanga zaidi kuhusu uhusiano uliopo baina ya fasihi simulizi (ngano) na fasihi andishi (hadithi fupi). Kupitia utafiti wake, tumepata mwanga zaidi kuhusu nadharia ya vikale, asili yake na mihimili yake. Hata hivyo, tofauti na Kenguru aliyetafiti kuhusu riwaya na fasihi simulizi kijumla utafiti huu ulizingatia hadithi fupi na ngano. Utafiti huu pia umechanganua miundo, mtindo, wahusika na maudhui ya ngano na hadithi fupi. Uchanganuzi huu umelenga kulinganisha vipengele hivi ili kubaini ikiwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ni kimelea cha ngano.

Onchangu (2013) ametafiti kuhusu Mtindo katika Riwaya na Hadithi Fupi za Clara Momanyi. Riwaya na hadithi fupi hizo ni: *Tumaini* (2006), “Ngome ya Nafsi” katika *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004), “Masazo ya Fisadi” na “Mtumbwi wa Maskini” katika *Takrima Nono na Hadithi Nyingine* (2011). Katika utafiti wake ameeleza maana ya hadithi fupi, historia yake na sifa za hadithi fupi. Baadhi ya sifa alizozitaja ni: uasili, umoja, ubanifu, ubora wa kimtindo na kiini wazi. Utafiti wake umekuwa wa manufaa kwetu kwani baadhi ya sifa alizozitaja zitatumwa kama kielelezo katika utafiti wetu. Hata hivyo, utafiti huu haujazingatia riwaya bali ngano na vipengele vingine vya fani. Utafiti huu pia

haujakomea katika kuchanganua kipengele cha mtindo katika hadithi fupi bali pia tumelinganisha mtindo huo na ule wa ngano.

Oyoyo (2013) ameshughulikia Uhakiki wa Fani katika Ngano Tano za Kiswahili. Ngano alizozichambua ni: “Kisa cha Binti Matlai Shamshi”, “Kisa cha Cheche na Sungura”, “Mighani ya Fumo Liyongo”, “Sungura na Simba” na “Kisa cha Ndovu na Binadamu”. Kwa kutumia nadharia ya umuundo amebaini kuwa ploti za ngano ni sahili na huwa na wazo moja kuu. Pia ameshughulikia sifa za wahusika na mbinu za usimulizi katika ngano. Utafiti wake ulitupa mwanga zaidi kuhusu sifa za ngano. Hata hivyo, tofauti naye tumechanganua pia maudhui katika ngano. Utafiti huu pia umelinganisha sifa hizi za ngano na sifa za hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.

Nyamsenda (2015) ameshughulikia Ushujaa wa Shujaa wa Motifu za Safari na Msako katika Ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibari. Baadhi ya ngano alizozishughulikia ni kama vile: ngano za “Watoto Wawili na Mazimwi”, ngano ya “Dege”, “Hekaya za Pangoni”, “Radhi ya Mali” na “Nyange Shimoni”. Amebaini kuwa kuna taswira zinazojirudia katika ngano kuhusu mashujaa kama vile: msisitizo katika utamaduni wa waikizu, shujaa kurudi nyumbani na shujaa kuondoka peke yake. Usawa baina yetu naye ni kuwa utafiti wetu pia umetumikiza nadharia ya vikale. Utafiti wake umekuwa wa manufaa kwetu kwani umetuelekeza kubaini ikiwa sifa hizo za ushujaa zinajitokeza katika ngano tulizoziteua. Utafiti wa Nyamsenda umelenga kulinganisha na kulinganua sifa za ushujaa zinazojitokeza katika ngano pekee. Hata hivyo, tofauti naye utafiti huu umelenga kulinganisha na

kulinganua sifa hizi za ushujaa zinazojitokeza katika ngano na zile sifa za ushujaa zinazojitokeza katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.

Chemutai (2016) ameshughulikia Mtindo katika Hadithi Fupi ya Kisasa. Baadhi ya hadithi alizozishughulikia ni “Pendo la Heba” (1996) na “Mayai Waziri wa Maradhi” (2004). Akitumia nadharia ya mtindo amechanganua historia na maendeleo ya hadithi fupi. Pia ameangazia mitindo mbalimbali ya hadithi fupi kama vile: tashbihi na majazi na athari ya mitindo hiyo. Utafiti wake umekuwa wa manufaa kwetu kwani umetuwezesha kuelewa mitindo ya hadithi fupi. Utafiti wetu umetofautiana naye kwani hatukukomea katika kuchanganua mtindo wa ngano bali pia tumechanganua mtindo wa hadithi fupi. Hali kadhalika, utafiti huu umechanganua vipengele vingine katika ngano na hadithi fupi kama vile: maudhui, wahusika na muundo na kuvilinganisha ili kubaini ukuruba uliopo baina ya ngano na hadithi fupi.

Kutokana na tafiti ambazo zimeorodheshwa ni wazi kuwa kuna tafiti anuwai zilizofanywa kuhusu hadithi fupi na kiasi kuhusu ngano. Hata hivyo, tafiti hizi hazijalinganisha na kulinganua hadithi fupi za kisasa za Kiswahili na ngano kimuundo, kimtindo, wahusika na kimaudhui.

1.8 Misingi ya Nadharia

Nadharia ya vikale ina mikondo mitatu. Nazo ni: Frazer, Jung na Frye. Hata hivyo, utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya vikale kulingana na maelezo ya Frye (1957). Aidha, mtafiti ameangazia wahakiki wengine walioendeleza nadharia ya

vikale kama vile: Guerin (2005), Campbell (2004) na Larsen (2018). Kulingana na Frye (1957), Wafula (1999), Wamitila (2003), Guerin (2005) na Wafula na Njogu (2007) vikale ni picha kongwe zinazojirudiarudia katika kazi ya fasihi. Picha hizi huweza kutambulika kama kiunzi cha ujuzi wa mtunzi wa kazi fulani ya kifasihi. Kwa mfano Wafula (1999) akitumia tamthilia ya *Marejeo* na *Wingu Jeusi* anathibitisha kuwa neno mkuyu ni kikale katika kazi hizi za Chacha.

Frye (1957) aliangalia vikale vya kimuundo katika tenzi. Kulingana naye, japo kuna jamii tofautitofauti kitovu cha fasihi ni kimoja. Amebaini kuwa kazi za fasihi hujengeka kutoka kwa kazi za awali. Hali hii inatokana na sababu kuwa wanadamu huingiliana (Kemunto, 2015). Ndiposa, nadharia hii inasisitiza usawa wa binadamu popote walipo. Aidha, fasihi ya jamii ya nchi mbalimbali huweza kuwekwa katika duara moja. Hivyo basi tofauti za kihistoria na kitamaduni haziwezi kutumika kuelezea upekee wa mtunzi fulani (Marete, 1992).

Kwa upande mwingine, Larsen (2018) aliangalia vikale vinavyojitokeza katika Bibilia. Akitumia mtazamo wa kidini, anaeleza kuwa Yesu ni shujaa ambaye kutokana na kutenda miujiza anakuwa na marafiki wengi na pia maadui. Hali hii ndiyo inaibua mgogoro baina ya makundi haya mawili.

Usawa baina ya mawazo ya binadamu huweza kutokana na baadhi ya taswira kongwe kurudiwarudiwa katika kazi tofauti za kifasihi. Kurudiwa huku huathiri miundo, mtindo na maudhui yanayotiliwa maanani katika kazi husika. Hali hii huweza kuathiri usawiri wa wahusika katika kazi za kisanaa. Frye akitumia ngano

za visakale na visasili anaeleza kuwa ili vipera hivi vikubalike lazima mtunzi atumie mbinu ya majazi. Majazi ni mbinu ya kisanaa ya kuwapa wahusika wa kazi ya fasihi majina yanayoakisi sifa na matendo yao.

Wahusika katika kazi za kisanaa huweza kugawanywa katika sehemu mbili kuu kutegemea sifa wanazopewa. Kuna wale wanaopewa sifa hasi na wale wanaopewa sifa chanya. Kutokana na sifa hizi, kumeibuka vikale vifuatavyo: mashujaa, wasingiziwa, mpenzi, baba na mama na watu wenye ndimi kali. Ruwaza hizi za aina za wahusika huweza kufanana katika kazi tofauti za kifasihi (Kemunto, 2015). Mfano ni mhusika nguli ambaye ni kikale katika kazi za fasihi. Mhusika nguli katika kazi hizi hupewa sifa zinazozidi binadamu wa kawaida. Hata hivyo, licha ya uwezo mkuu anaopewa mhusika nguli Guerin (2005) anaeleza kuwa mhusika huyu lazima aanguke au kushindwa. Kwa mfano Lwanda Magere miongoni mwa jamii ya waluo na Fumo Liyongo miongoni mwa jamii ya wamijikenda. Marete (1992) anaeleza kuwa sifa hizi ndizo nguzo muhimu katika kazi za kisanaa. Aidha, Campbell (2004) anaeleza kuwa kuna ruwaza tatu zinazomtambulisha shujaa. Nazo ni: shujaa kuondoka alipo, shujaa kukutana na vikwazo na kuvishinda na mwishowe shujaa kurudi katika jamii yake ili kupigana apate ushindi.

Guerin (2005) akimnukuu Frye (1957) anaeleza kuwa kazi ya fasihi huweza kuwa na ishara mbalimbali zinazoashiria dhana moja. Aidha, Frye (1957) anaangalia dhana hii kwa kutumia mtazamo wa kidini. Anaeleza kuwa mti usiozaa matunda na msalaba huweza kuashiria dhana moja. Hali kadhalika, ndege huweza kuashiria

roho mtakatifu. Ishara hizi tofauti huibua maudhui makuu yanayojitokeza katika kazi za kisanaa tofauti kiasi kuwa zinatawala maudhui mengine. Maudhui yanayotawala kazi hizi huweza kutambulisha kazi hizo za kisanaa. Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007) baadhi ya maudhui yanayotawala kazi za kifasihi ni kama vile: mauti, ufasiri wa ndoto, wema na uovu na kuwaasa wanaoishi.

Frye anaeleza kuwa dunia imegawanywa katika pande mbili. Upande wa Mungu na upande wa Ibilisi. Pande hizi huwa katika vita siku zote kwani zinaendeleza maudhui tofauti ya wema na uovu. Anathibitisha kauli yake kwa kutumia mfano wa Ayubu katika Biblia ambapo shida yake ilitokana na vita baina ya Mungu na Ibilisi. Katika vita hivi, tabia mbalimbali za Mungu na Ibilisi hujitokeza kwa mfano kufa, kuzaliwa upya na kupuuza jambo fulani. Isitoshe, Frye anaeleza zaidi kuhusu muundo wa visakale ambapo shujaa anazaliwa, anaendeleza safari kuelekea kifo chake, kupotea kwa shujaa na kuzaliwa upya kwa shujaa.

1.8.1 Mihimili ya Nadharia ya Vikale

Kwa ufupi mihimili ya nadharia hii kwa mujibu wa Northrop Frye (1957) ni kama ifuatavyo:

- a) Miundo ya kazi za fasihi za jamii tofauti hufanana.
- b) Taswira mbalimbali za kimtindo hujirudiarudia katika kazi tofauti za kifasihi.
- c) Maudhui yanayotawala maudhui mengine katika kazi tofauti za kifasihi yanafanana na yanajirudia katika kazi tofauti za kifasihi.

- d) Sifa za wahusika zinazopewa kipaumbele katika kazi za fasihi hufanana na hujirudia kutoka kazi moja hadi nyingine.
- e) Uhalisia huanza kwa uchunguzi wa visasili na vikale. Vikale ni maigizo ya vitendo vilivyo katika mipaka ya matamano asilia ya walimwengu. Miungu huwakilisha tabia tofauti tofauti. Kwa mfano hufurahia wanawake, hupigana wao kwa wao, huliwaza na kumsaidia binadamu aliyedhulumiwa au kumtazama tu.
- f) Kazi ya fasihi hugawika katika sehemu nne kuu. Nazo ni: sehemu inayohusu mapenzi, tanzia, dhihaka na futuhi. Sehemu hizi huathiri visakale kwani kuna kuzaliwa kwa shujaa, safari yake kuelekea kushindwa na kifo, kupotea kwake na kuzaliwa upya kwa shujaa.

Mihimili ifuatayo minne imetumiwa katika utafiti wetu kwa mujibu wa maswali yetu ya utafiti ili kutuwezesha kufikia suala letu la utafiti. Nayo ni:

- a) Miundo ya kazi za fasihi ya jamii tofauti hufanana. Mhimili huu umetusaidia kubaini ikiwa miundo mbalimbali ya ngano na hadithi fupi hufanana au hutofautiana.
- b) Taswira mbalimbali za kimitindo hujirudiarudia katika kazi mbalimbali za fasihi. Mhimili huu umetusaidia kubaini ikiwa kuna mitindo maalum inayojirudia na kufanana katika ngano na hadithi fupi.
- c) Maudhui yanayotawala maudhui mengine katika kazi ya kifasihi yanafanana na yanajirudiarudia katika kazi tofauti. Mhimili huu

umetusaidia kubaini ikiwa maudhui yanayopewa kipaumbele katika ngano na hadithi fupi yanafanana.

- d) Sifa za wahusika zinazopewa kipaumbele katika kazi za fasihi hufanana na hujirudia kutoka kazi moja hadi nyingine. Mhimili huu umetusaidia kubaini sifa zinazopewa wahusika fulani katika ngano pia zinajitokeza katika hadithi fupi.

Mihimili hii minne ya nadharia ya vikale ilituongoza katika utafiti wetu ili kujua iwapo kuna vigezo sawia vya kupimia hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili na ngano. Kwa kuchanganua miundo, wahusika, maudhui na mitindo ya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili na ngano tukiongozwa na mihimili hii minne, tumeweza kuthibitisha ni kwa kiasi kipi hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili na ngano zinahusiana na kutofautiana. Uchanganuzi huu umeweza kudhihirisha kuwa fasihi simulizi (ngano) si picha kongwe ya fasihi andishi (hadithi fupi). Kudhihirisha huku kumbainisha kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili sio kimelea cha ngano.

1.9 Mbinu za Utafiti

Katika sehemu hii mtafiti ameangazia njia za utafiti. Amegawanya njia hizi katika makundi yafuatayo: muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, njia za kukusanya data, uteuzi wa sampuli, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo.

1.9.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kimaelezo. Maelezo yametolewa kuhusu maudhui, wahusika, mitindo na miundo ya ngano na hadithi fupi. Maelezo haya yametolewa kwa minajili ya kulinganisha na kulinganua sifa za kimuundo, wahusika, maudhui na kimtindo baina ya ngano na hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Ulinganishaji na ulinganuaji huu umelenga kubaini ikiwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ni kimelea cha ngano.

1.9.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu umejikita katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta na vyuo vingine nchini Kenya kwa mfano Chuo Kikuu cha Nairobi, Chuo Kikuu cha Jomo Kenyatta na Chuo Kikuu cha Egerton. Usomaji huu umelenga diwani mbili za hadithi fupi, vitabu viwili vya ngano na yale yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya vikale, hadithi fupi na ngano. Mtafiti alisoma makala mbalimbali yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti kama vile: vitabu, tasnifu, magazeti na majarida.

1.9.3 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli umefanywa kimakusudi kutokana na usomaji wa awali. Mtafiti ameteua hadithi nane katika diwani za *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* (2011) na *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007). Aidha, mtafiti ameteua hadithi ya “Waliohujumu Ujamaa” iliyomo kwenye diwani ya *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* (2006). Hadithi hizi zimeteuliwa kwa kutumia mbinu kusudio. Mtafiti alibuni utaratibu maalum uliomwongoza katika uteuzi wa sampuli.

Mbinu hii ilihusisha kuchagua hadithi fupi zinazoonyesha sifa zinazofanana na ngano na zile zinazoonyesha sifa zinazotofautiana na ngano. Hadithi zilizoteuliwa ni pamoja na:

Kurudi Nyumbani na Hadithi Mwavyaji wa Roho na Hadithi

Nyingine

Safari ya Maangamizi (uk. 154-171)

Njozi ya Mtu Mweupe (uk. 22-33)

Njia ya Mwongo (uk. 172-186)

Shetani Hana Hatia (uk. 52-63)

Nyingine

Dr. Strese (uk. 37-53)

Mwavyaji wa Roho (uk. 71-84)

Uganga wa Pete (uk. 98- 108)

Kadhia ya Sikujua (uk. 118-127)

Aidha, mtafiti ameteua ngano kutoka kwa vitabu vya *Myths and Legends of the Swahili* (1970) na *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* (1870). Ngano hizi zimeteuliwa kimakusudi kwa msingi kuwa zinaonyesha sifa zinazoweza kunasibishwa na hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Ngano zilizoteuliwa ni:

Myths and Legends of the Swahili

Hadithi za Abunuwasi (uk. 112-120)

Hadithi zinazodhihaki jamii (uk. 145-

151)

Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar

Sultan Darai (uk. 11-38)

Hadithi ya Liyongo (uk. 439-454)

Kutokana na sampuli hii, mtafiti ameweza kubainisha mshabaha na tofauti zilizomo baina ya hadithi fupi za kisasa za Kiswahili na ngano. Amefanya hivi kwa kuchanganua maudhui, wahusika, mtindo na miundo ya hadithi fupi na ngano alizoziteua.

1.9.4 Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu umetumia usomaji wa kina kama njia kuu ya kukusanya data. Mtafiti amekusanya data kwa kusoma na kuchambua hadithi zilizoko katika diwani tatu na ngano zilizomo katika vitabu viwili. Miongoni mwa yale yaliyotengwa yalikusiana na wahusika, miundo, maudhui na mitindo inayojitokeza katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili na ngano.

1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Data imekusanywa na kunukuliwa. Mwishowe, data imechanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Aidha, mtafiti ameangazia nadharia ya vikale. Mtafiti amechanganua data inayohusu miundo, wahusika, mitindo na maudhui ya hadithi fupi za kisasa za Kiswahili na ngano. Mwishowe, mtafiti amebaini kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili si kimelea cha ngano. Hii ni kwa sababu sifa nyingi za hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zinatofautiana na sifa za ngano.

1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Data iliyokusanywa imewasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia sura mbalimbali. Uwasilishaji wa data umefanywa kwa kuongozwa na malengo ya

utafiti pamoja na mihimili ya nadharia ya vikale. Mtafiti amebainisha kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili si kimelea cha ngano. Hii ni kwa sababu sifa nyingi za hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zinatofautiana na sifa za ngano.

1.9.7 Maadili ya Utafiti

Utafiti huu umefanywa kwa kuzingatia maadili ya utafiti ambayo ni uwazi na uaminifu. Utafiti huu haukuiba mawazo ya waandishi wa hapo awali kwani wizi wa kitaaluma ni kinyume na maadili ya utafiti. Kulingana na Mligo (2012), wizi wa kitaaluma huhusisha wizi wa mawazo, maneno au vifungu vya maneno kutoka kwa watafiti wengine. Utafiti huu umeepukana na wizi huu kwa kutambua mchango wa wataalam na waandishi wengine kwa kuwanukuu.

1.9.8 Changamoto za Utafiti

Licha ya kuwa malengo yameafikiwa, utafiti huu umekumbwa na changamoto kadhaa. Baadhi ya vitabu ikiwemo *Myths and Legends of the Swahili* (1970) na *Anatomy of Criticism* (1957) vimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza na hivyo basi, ilimbidi mtafiti atafsiri kazi hizi. Utafsiri huu umetugharimu muda. Aidha, ni vigumu tafsiri kuwa sawa kabisa na matini chanzi. Ilikuwa vigumu kwa mtafiti kuamua kwa kiasi gani tafsiri yake iegeme kwenye lugha chanzi au lugha lengwa. Hali kadhalika, utafiti huu ulihitaji hela nyingi. Kutokana na ukosefu wa ufadhili kutoka mashirika ya kiserikali ilimbidi mtafiti atafute njia nyinginezo za kujigharamia. Hali hii imeathiri utafiti kwa sababu mtafiti hakuweza kupata vitabu

vingi ili kuvisoma. Labda mtafiti angekuwa na hela zaidi utafiti huu ungekuwa bora zaidi kwa kuwa mtafiti angewanukuu wasomi wengi zaidi.

1.9.9 Hitimisho

Katika sura hii, tumejadili vipengele muhimu katika utafiti. Vipengele hivi ni: ikisiri, ufafanuzi wa istilahi, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti na sababu za kuchagua mada. Hali kadhalika, utafiti huu umejadili upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi na mihimili ya nadharia ya vikale. Isitoshe, mbinu za utafiti ikiwemo: muundo wa utafiti, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, maadili ya utafiti na changamoto za utafiti zimeangaziwa.

SURA YA PILI
MUUNDO NA MTINDO WA NGANO NA HADITHI FUPI YA KISASA
YA KISWAHILI

2.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, suala la utafiti limefafanuliwa na jinsi ya kulifanyia uchunguzi kuelezwa. Aidha, sababu za kuchagua mada, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na upeo wa utafiti yameelezwa. Isitoshe, lengo letu la kwanza ni kubainisha namna mbalimbali miundo hujitokeza katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili na ngano. Aidha, lengo letu la pili ni kujadili mitindo mbalimbali inayojitokeza katika hadithi fupi na ngano. Malengo haya mawili yamejadiliwa katika sura hii.


Imebainika kuwa kuna mitazamo miwili kuhusu asili ya hadithi fupi. Mtazamo wa kwanza unaelezea hadithi fupi kama zao la mchakato wa kistari kutoka kwa ngano hadi kwa hadithi fupi ilhali mtazamo wa pili unaeleza kuwa hadithi fupi ni utanzu ulioibuka kivyake. Ni kutokana na mitazamo hii miwili ndipo mtafiti akiongozwa na nadharia ya vikale amejadili miundo na mitindo mbalimbali ya hadithi fupi za kisasa za Kiswahili na ngano katika sura hii. Kujadili huku kutabainisha ikiwa sifa za kimiundo na kimtindo zinazojitokeza katika ngano mara kwa mara pia zinajitokeza katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.

2.1 Dhana ya Muundo

Muundo unaeleza jinsi kazi ya fasihi ilivyo kwa kuitazama. Mbatiah (2001) anaeleza kuwa muundo ni uhusiano wa elementi za kazi za kifasihi. Maelezo haya

yanaoana na yale ya Wamitila (2003) ambaye anasema kuwa dhana ya muundo hutumiwa kueleza sifa za nje zinazoipa kazi ya kifasihi umbo linaloweza kutambulika. Kutokana na maelezo haya, tunagundua kuwa muundo wa kazi huweza kuonekana bayana hata kabla ya kuisoma kazi ya kifasihi.

Hata hivyo, maelezo ya Wamitila yana udhaifu kwani muundo wa kazi ya kifasihi huweza kutambulishwa pia kupitia usomaji. Kutokana na maelezo ya wataalam hawa, muundo ni sifa za ndani na za nje zinazoipa kazi ya kifasihi sura inayoweza kutambulika. Hull (1988), Shore (1993), Wamitila (2002) na Chemutai (2016) wanakubaliana kuwa utanzu wa hadithi fupi huweza kugawanya katika sehemu tatu kuu. Sehemu hizo ni: mwanzo, sehemu ya kati na mwisho. Sehemu hizo huweza kuwakilishwa kwa mchoro ufuatao:



Mchoro wa sehemu za muundo wa hadithi fupi

2.2 Muundo wa Ngano na Hadithi Fupi

Miundo ya ngano na hadithi fupi huhusisha sifa zifuatazo:

2.2.1 Mwanzo

Wamitila (2008) anaeleza kuwa ngano za fasihi simulizi huwa na fomula maalum za utangulizi. Gatricya (2014) na Mbatiah (2016) wanashadidia maoni haya kwa kueleza kwamba fomula hizi huweza kuwa ‘hapo zamani za kale’ au ‘paliondokea’. Katika kitabu cha *Myths and Legends of the Swahili* kuna ngano ya “Maskini na Tajiri” ambayo fomula hii inabainika. Mwandishi anaeleza hivi:

Hapo zamani za kale kuliishi mtu Maskini na tajiri.
Maskini alikuwa na mifugo wachache ilhali tajiri alikuwa
na mifugo wengi (Uk. 146).

Mwandishi ameanza sentensi yake kwa kishazi ‘hapo zamani za kale’ katika mfano huu. Kishazi hiki kinatumiwa mwanzoni kabla ya kuwatambulisha wahusika wakuu ambao ni Maskini na Tajiri. Hali kadhalika, mtindo huu wa usimulizi pia unapatikana katika ngano ya “Liyongo” iliyomo katika kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*. Mwandishi anaeleza hivi:

Hapo zamani za Shanga palikuwa mtu, jina lake Liyongo,
naye ana nguvu sana, mtu mkubwa sana katika mji (Uk. 439).

Nukuu hii katika ngano ya “Liyongo” inaanza kwa kishazi ‘hapo zamani za’.
Mwandishi ametumia kishazi hiki kabla ya kumtambulisha mhusika Liyongo.
Ngano hizi mbili zinatumia mwanzo wa ‘hapo zamani za’ kama fomula maalum.
Kwa hivyo, mwanzo huu huweza kuchukuliwa kama muundo wa kivikale

unaotambulisha ngano hizi. Hali hii inaweza kuwa imetokana na uigaji wa miundo ya awali. Ndiposa, Ngure (2003) anaeleza kuwa mtindo wa fasihi simulizi ni wa kikasuku yaani wa kuiga tu. Hali kadhalika, Mbatiah (2016) anaeleza kuwa fomula hizi hubainisha kuwa ngano hurejelea wakati wa nyuma usiopimika.

Kwa upande mwingine, Wamitila (2008) na Makena (2018) wanakubaliana kuwa hadithi fupi huwa na mianzo tofauti. Wamitila (2008: 189-196) anaelezea mianzo ifuatayo ya hadithi fupi: mwanzo wa kifomula, kirejeshi, kielekezi, kifafanuzi, kipenyezi, kingogoro, kimazungumzo, urudiaji wa kichwa na kidrama. Katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* kuna hadithi ya “Safari ya Maangamizi” inayotumia mwanzo wa kimazungumzo. Mwandishi anaeleza hivi:

Mzee Majuto ambaye daima hurauka mapema alisikika nje ya nyumba yake akisemezana na mkewe. “Mama Kimweri, jana usiku niliota ndoto ya ajabu!” “Ah! Ati ndoto? Mkewe aliuliza huku akijifunga kanga yake kiunoni. “Ndiyo..... (Uk. 154).

Mfano huu unaonyesha jinsi mwandishi wa hadithi ya “Safari ya Maangamizi” alivyotumia mbinu ya kimazungumzo mwanzoni mwa hadithi kuelezea ndoto ya ajabu aliyoiota Mzee Majuto.

Hadithi ya “Uganga wa Pete” iliyomo katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* inatumia mwanzo unaoonekana ni wa kifomula. Mwandishi anaanza hadithi yake hivi:

Miaka nenda miaka rudi palikuwepo katika nchi fulani mtu mmoja Maskini sana kiasi kwamba hana mbele wala nyuma (Uk. 99).

Nukuu hii katika hadithi ya “Uganga wa Pete” inatumia kishazi ‘miaka nenda miaka rudi’ kabla ya kumtambulisha mhusika mkuu anayeitwa Maskini. Camara (1986) anaeleza hivi:

Japo ngano huelezea matukio ya kitambo, matukio yake huelezwa ni kana kwamba yanatendeka kwa sasa (Uk. 6).

Maneno haya ya Camara (1986) yanaonyesha kuwa ngano haionyeshi wakati unaopimika kihistoria. Hadithi ya “Uganga wa Pete” tuliyoijadili inaonyesha ukosefu wa wakati mahususi kama zilivyo ngano. Hadithi hii inaanza kwa maneno ‘miaka nenda miaka rudi’. Mfano huu unabainisha kuwa muundo huu umetokana na ngano za awali. Usawa huu unaonekana kuambatana na maelezo ya Frye (1982).

Frye anaeleza hivi:

Kazi za kifasihi huwa na maumbo yanayoyatawala. Maumbo haya yanatambulisha kazi hizo licha ya tofauti za kimazingira (Uk. xiii).

Kutokana na maelezo haya ya Frye (1982), inabainika kuwa kazi za kifasihi huweza kufanana kiumbo licha ya kutungwa katika mazingira tofauti. Nadharia ya vikale inashikilia kuwa licha ya kuwa kazi za fasihi zimetungwa katika nyakati tofauti au mazingira tofauti maumbo yake hufanana. Ndiposa, hadithi hii ya “Uganga wa Pete” ina mwanzo unaofanana na ngano za “Liyongo” na “Maskini na Tajiri” licha ya kuwa imetungwa katika mazingira tofauti na nyakati tofauti.

Mbinu nyingine iliyotumika katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ni ile ya taharuki. Mwandishi wa hadithi ya “Shetani Hana Hatia” inayopatikana katika

diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* ametumia mbinu hii mwanzoni mwa hadithi. Anaanza hadithi yake hivi:

Paka-shume alizinduka ghafla kutoka kwenye ulimwengu wa ndoto si ndoto. Kwa hakika alikuwa amezirai. Fahamu ziliporejea, polepole ndipo alinyemelewa na usingizi wa mang'amung'amu. Alihisi maumivu makali akiuchuma mwili wake mzima kama moto wa tanuri ya kuyeyusha vyuma (Uk. 52).

Hadithi hii ya “Shetani Hana Hatia” imetuacha katika hali ya taharuki. Tunajiuliza ni nini hasa kilichosababisha Paka-shume kuzirai na kuhisi maumivu makali. Isitoshe, tunajiuliza ni nini hasa kilitendeka baadaye. Hadithi zingine zilizotumia mbinu hii ni kama vile “Unyayo Bustanini” katika diwani ya *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine* na “Kijana Yule” katika diwani ya *Kicheko cha Ushindi na Hadithi Nyingine*.

Mwishowe, kuna hadithi ya “Njozi ya Mtu Mweupe” iliyoko kwenye diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* inayotumia mwanzo wa kifafanuzi. Mwandishi anaeleza hivi:

Katika ujana wangu nilitambua jambo moja kuhusu maumbile ya binadamu. Nalo ni kuwa maisha ya watu wengi yalitawaliwa na imani na mapendeleo yasiyokuwa na mantiki. Hali hii ni kinyume na falsafa yangu kuhusu maisha yangu.... (Uk. 22).

Hadithi hii ya “Njozi ya Mtu Mweupe” inatumia mbinu ya kifafanuzi ili kutuelezea jinsi maumbile ya binadamu yalivyo. Hali kadhalika, anaeleza kuwa binadamu ametawaliwa na mapendeleo yasiyokuwa na mantiki.

Imebainika kuwa ngano huwa na mianzo maalum ambayo ni ya kifomula (Wamitila, 2008). Kwa upande mwingine, hadithi fupi za kisasa za Kiswahili huwa na mianzo tofauti kutoka hadithi moja hadi nyingine. Mifano ni kama vile: hadithi ya “Njozi ya Mtu Mweupe” inayotumia mwanzo wa kifafanuzi, “Safari ya Maangamizi” inatumia mwanzo wa kimazungumzo, hadithi ya “Shetani Hana Hatia” inatumia mwanzo wa kitaharuki na “Uganga wa Pete” inatumia mwanzo wa kifomula. Kwa msingi huu, mwanzo wa kifomula “hapo zamani za” ambao ni kikale katika ngano haujirudii katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Hali hii inatofautiana na mhimili wa nadharia ya vikale unaoeleza kuwa miundo ya kazi za kifasihi ya jamii tofauti hufanana. Kwa msingi huu, maelezo ya Frye (1982) kuwa kazi ya fasihi huwa na sifa maalum zinazoridhishwa na kusambazwa hayana mashiko. Kutokana na haya, inabainika kuwa mtu anaweza kutunga hadithi kwa kutumia mianzo tofauti bila kuzingatia ngano za awali. Ndiposa, Mukopi (2005) anaeleza kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ilitokana na utaalamu wa uandishi na usimulizi. Jambo hili linaonyesha kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili sio kimelea cha ngano.

2.2.2 Sehemu ya Kati

Kulingana na Chemutai (2016), sehemu ya kati ya hadithi fupi husawiri utata uliopo baina ya wahusika mbalimbali. Hii ni kwa sababu wahusika hawa wana mitazamo tofauti. Mitazamo hii tofauti ndio huibua migogoro baina yao. Ngongolo (2015) anaeleza kuwa mwandishi hukuza dhamira kuu kwa kuelezea matukio mbalimbali. Matukio haya ndiyo husawiri migogoro baina ya wahusika.

Hadithi ya “Safari ya Maangamizi” iliyomo katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* inahusu mhusika aitwaye Pendo. Hadithi hii inaanza kwa kutuelezea kuhusu kifo cha Pendo. Baadaye kwa kutumia mbinu ya kisengerenyuma mwandishi anaelezea yaliyotukia maishani mwake Pendo kabla aage dunia. Matukio haya yanaonyesha kuwa Pendo alikuwa mtu mzuri wa kuigwa. Alikuwa ni msichana mwenye nidhamu ya hali ya juu. Aidha, alikuwa ni msichana wa kwanza katika kijiji chao kuenda chuo kikuu. Hata hivyo, sehemu ya kati ya hadithi hii inaibua mgogoro unaobadilisha mkondo wa maisha ya Pendo. Hadithi hii inafika upeo wakati ambapo Pendo anaponajisiwa na wanaume akiwa chuoni. Baada ya kisa hiki, Pendo anagundua kuwa ameambukizwa virusi vya UKIMWI. Baadaye kunatokea hali ya mpomoko ambapo Pendo anabadilika kimaadili na kuamua kuwaambukiza wanaume ugonjwa wa UKIMWI.

Hadithi Nyingine ni ile ya “Uganga wa Pete” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Hadithi hii inaeleza kuhusu Maskini ambaye alienda kuomba msaada kwa mama kitumbua. Akiwa hapo anabaini idadi ya vitumbua vilivyotengenezwa bila kutazama Mama Vitumbua akipika. Mama Vitumbua basi anamuona Maskini kama mganga. Baadaye, tunaona Maskini akitatua baadhi ya matatizo ya jamii kama vile kutafuta pete ya mfalme iliyopotea. Hata hivyo, hadithi hii inafika upeo wakati ambapo mgogoro unaibuka baina ya Maskini na watu wachache ambao hawakuamini uwezo wake. Watu hao waliamini kuwa uganga wa Maskini ni wa kubahatisha tu. Mgogoro huu unakuzwa wakati ambapo wanaamua kuiba mali ya mfalme ili kumuadhibu Maskini. Hata hivyo, kwa kubahatisha

Maskini anawatambua walioiba mali ya mfalme. Hadithi hii inaisha kwa mbinu ya kitatuzi kwani Maskini anatatua shida za wanajamii na baadaye kutuzwa.

Kwa upande mwingine, sehemu ya kati ya ngano pia husawiri migogoro ambayo huweza kutatuliwa au huweza kuibua kuanguka kwa shujaa. Mfano ni ngano ya “Liyongo” iliyomo katika kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*. Sehemu ya kati ya ngano hii inasawiri migogoro baina ya Liyongo na wahusika mbalimbali. Kwanza, mwandishi anaelezea kuhusu mgogoro baina ya wanakijiji wa Shanga na Liyongo. Mgogoro huu unasababishwa na Liyongo kwa sababu ndiye anayewadhulumu. Baadaye kunatokea mgogoro baina ya Liyongo na mfalme. Mgogoro huu unatokea kwa sababu mfalme alihofia kuwa Liyongo atampokonya ufalme. Anaamua kutafuta usaidizi kutoka kwa Wagalla ambao wanashindwa kumuangamiza Liyongo. Hata hivyo, ngano hii inafika upeo wa juu wakati ambapo mfalme anamuita mwanawe Liyongo na kumhadaa kuwa akimsaidia katika harakati ya kumuangamiza Liyongo, atampa zawadi. Hali hii inamfanya mwanawe Liyongo kumuangamiza Liyongo ili apate ufalme. Hata hivyo, ngano hii inaisha kwa kuonyesha kuanguka kwa Liyongo na pia mwanawe Liyongo.

Aidha, kuna ngano ya “Sultan Darai” inayopatikana katika kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*. Sehemu ya kati ya ngano hii inasawiri migogoro kati ya mkewe seremala na mtoto wake seremala. Hii inatokana na sababu kuwa mkewe seremala anakataa kumpa mtoto huyo chakula. Aidha, anamdanganya seremala kuwa amempa mtotowe chakula. Anafanya hivi kama njia ya kuficha

uovu wake. Hata hivyo, seremala anagundua ukweli na kuamua kuoia bibi mwingine.

Mwishowe, kuna ngano ya “Kibwana” inayopatikana katika kitabu cha *Myths and Legends of the Swahili*. Ngano hii inatueleza kuhusu Kibwana ambaye alielezwa na babake asiwahi kumuambia yeyote siri yake. Upeo wa ngano hii unatokea wakati Kibwana anapona tango msituni. Baadaye anakuwa na mgogoro nafsiini kuhusu ikiwa ni vyema kumuambia mkewe siri hii au la. Anaamua kumuambia mkewe siri hiyo. Mwishoni mwa ngano tunaona anaadhibiwa.

Kutokana na maelezo haya, imebainika kuwa sehemu ya kati ya ngano na hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili huwa na sifa sawia. Tanzu hizi zote huhusisha mfuatano wa matukio ambayo huibua migogoro. Migogoro hii huweza kutatuliwa au kuibua hali ya kuanguka kwa mhusika. Mifano ni kama: hadithi ya “Safari ya Maangamizi” inayoonyesha mgogoro kati ya Pendo na wanaume, hadithi ya “Uganga wa Pete” inayoonyesha mgogoro kati ya Maskini na wanajamii wachache ambao hawakuamini uwezo wake na ngano ya “Liyongo” inayosawiri mgogoro kati ya Liyongo na wanajamii.

2.2.3 Mwisho

Wamitila (2008) na Russel (2009) wanakubaliana kuwa ngano hutamatika kwa maneno maalum kama vile ‘wakaishi raha mustarehe’. Wakati mwingine ngano huweza kuishia na maneno ‘hadithi yangu imeishia hapo’ (Ngure, 2003).

M'ngaruthi (2007) anaongezea kwa kuelezea kuwa ngano za visasili na usuli huishia kwa maneno kama vile 'hii ndiyo sababu fisi huchechemea'.

Katika kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* kuna ngano ya "Sultan Darai" ambayo inatamatika kwa maneno 'raha mustarehe'. Ngano hiyo inatamatika hivi:

Na yule mwanamke akajikalia na mali yake. Kule, yeye na babaye na nduguye na jamaa yake wakaishi raha mustarehe (Uk. 136).

Mfano huu unatumia maneno 'raha mustarehe' ili kueleza jinsi mhusika mwanamke alivyoishi na jamaa zake baada ya kupata mali.

Ngano nyingine inayotamatika kwa kutumia fomula maalum imo katika kitabu cha *Myths and Legends of the Swahili*. Katika kitabu hiki kuna ngano ya "Mwanamke Atolewa Mahari ya Ng'ombe Mia Moja" inayotamatika kwa maneno 'wakaishi miaka mingi kwa raha na Amani'. Mwandishi anaeleza hivi:

Alichukua binti wake na bwanake na kuwapeleka nyumbani ambapo waliishi kwa raha na amani (Uk. 125).

Nukuu hii inaonyesha jinsi bwana, binti na bibi yake walivyoishi mwishowe. Ngano hizi mbili zinathibitisha uwepo wa kikale 'raha'. Kuwepo kwa neno 'raha' katika ngano inabainisha kuwa ngano nyingi za awali humalizika kwa muundo sawia.

Hata hivyo, kuna ngano zingine zinazoishia kwa kukariri mada fulani au funzo fulani. Wamitila (2008) na Makena (2018) wanakubaliana kuwa funzo hili hubainika waziwazi kwenye sehemu ya mwisho ya ngano inayohusika. Umuhimu wa sehemu hii ni kumfanya mja abadilishe mwenendo wake. Ndiposa, asiyetaka kubadilika huangamia au hujuta (Njogu na Chimera, 1999). Kitabu cha *Myths and Legends of the Swahili* kina ngano ya “Abunuwasi na Wezi Wawili” ambayo inaoana na kauli hii. Mwandishi anamalizia hivi:

Abunuwasi alikuwa ametabiri kuwa mwizi mmoja atarudi. Kwa hivyo aliwaita askari na kuwaambia wajifiche. Mwizi alipowasili, alimuambia kilichotendeka na akataka kupewa fomula ya miujiza. Punde alipomaliza hadithi yake, mwizi huyo alishikwa na askari wale kwani walikuwa wamesikia kila kitu. Baadaye walipata maiti ya mwenzake na mwizi huyo akahukumiwa kunyongwa. Usimdhuru mtu mwerevu (Uk. 114).

Mfano huu unathibitisha kuwa mwizi mmoja anaangamia na mwingine anashikwa kwa sababu ya kudanganyika haraka. Hali kadhalika, mwandishi anamalizia kwa funzo kuu kuwa haifai tumdhuru mtu mwerevu.

Isitoshe, kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* kina ngano ya “Liyongo” inayomalizika kwa mtindo huu. Mwandishi anamalizia hivi:

Akaenda kuwaambia watu mjini ya kwamba amekufa, wakaenda kumtazama, wakamwona amekufa, wakamzika. Wakamkamata yule kijana na wakaamua wasimpe ufalme (Uk. 452).

Nukuu hii inathibitisha kuwa kuna kijana anayejuta kwa ajili ya matendo yake. Hali ya mtu kujuta mwishowe kwa sababu ya matendo yake na funzo kuu kubainika waziwazi katika ngano huweza kuchukuliwa kama kikale katika ngano hizi.

Kutokana na haya, imebainika kuwa ngano huwa na miishio maalum. Miishio hii huweza kuwa ya kiadili au ya kifomula. Ndiposa Okpewho (1992) anaeleza kuwa ngano huwa na mianzo na miishio maalum ambayo hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Hali hii inaonyesha kuwa kila jamii ilikuwa na fomula maalum ya ufunguzi na utamatishaji wa ngano ambayo ilirithiswa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine.

Hadithi fupi za kisasa za Kiswahili huweza kutamatika kwa njia tofauti. Wamitila (2008: 197-204) anaainisha mbinu tofauti za kumalizia hadithi ikiwemo: mwisho wa kifomula, adili/mada, kimzunguko, kiasilia au kikawaida, kitaharuki, kimaswali, kilinganuzi, kiishara, kimshtukizo na kidhamira. Katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* kuna hadithi ya “Njia ya Mwongo” inayotumia mbinu ya kiadili ili kumalizia hadithi hiyo. Mwandishi anaeleza hivi:

Wazazi wao waliwaomba walimu wawape adhabu ya kufagia madarasa yao kila siku kwa juma zima. Hii ilikuwa adhabu tosha kuwakumbusha siku zote kwamba mchezo hauwezi kuchukua mahali pa kazi (Uk. 186).

Hadithi hii ina sentensi ya mwisho ‘mchezo hauwezi kuchukua mahali pa kazi’ ambayo inabainisha waziwazi dhamira ya mwandishi. Inabainika kuwa wahusika wakuu walileta mchezo walipopewa kazi. Hatimaye, wanajuta kwani wanapewa

adhabu ya kufagia madarasa yao juma zima. Isitoshe, katika hadithi hiyo anwani yake inarudiwa mwishoni mwa hadithi kama zilivyo ngano za awali. Mwandishi anaeleza hivi:

Ama kwa kweli njia ya mwongo fupi.
Baadhi ya wanakijiji walisikika wakisema
huku wakitembea kuelekea makwao..... (Uk. 186).

Dondoo hili linalopatikana mwishoni mwa hadithi ya “Njia ya mwongo” linatumia maneno ‘njia ya mwongo’ katika aya ya mwisho. Mwandishi amerudia anwani yake mwishoni mwa hadithi hii.

Mfano mwingine unapatikana katika hadithi ya “Uganga wa Pete” iliyomo katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Mwandishi anaonyesha kuwa dhamira yake kuu ni kuhimiza ushirikiano baina ya mke na mume. Hadithi hiyo inatamatika hivi:

Hapo tena babu alimaliza ngano yake na kumsihi mwanamume kumheshimu mkewe na kushirikiana naye maana ni ubavu wake tangu ngano za kale (Uk. 109).

Hali kadhalika, nukuu hii inaishia kwa maneno ‘alimalizia ngano yake’. Dhana ‘kumalizia ngano’ inaonekana kuwa sawia na muundo uliozoeleka wa kutamatisha ngano ‘hadithi yangu imeishia hapo’. Hadithi hii ya “Uganga wa Pete” inatamatika kwa kutumia mbinu ya kifomula.

Imebainika kuwa hadithi za “Njia ya Mwongo” na “Uganga wa Pete” zina miishio inayofanana na ngano tulizojadili. Hadithi ya “Njia ya Mwongo” ina mwisho inayorudia anwani ilhali hadithi ya “Uganga wa Pete” ina mwisho wa kifomula.

Hali hii inaambatana na mhimili wa nadharia ya vikale unaoeleza kuwa miundo ya kazi tofauti hufanana. Kwa msingi huu, miundo ya kazi za awali huweza kurithishwa. Ndiposa, Volger (2007) na Synder (2005) wanakubaliana kuwa kuna muundo mmoja unaojitokeza katika kila hadithi. Aidha, wanaeleza kuwa hadithi zote ni sawa kwani mwandishi wa kila hadithi huanza na muundo sawia. Hali hii yaweza kubainisha kuwa waandishi wa hadithi za “Uganga wa Pete” na “Njia ya Mwongo” waliathirika na ngano za awali. Hii ni kwa sababu wametumia miishio inayofanana na miishio ya ngano za awali.

Kuna hadithi zingine za kisasa za Kiswahili zinazotumia miishio ya kimzunguko. Miishio ya kimzunguko inaashiria kuwa hadithi huishia sehemu iliyoanzia yaani wakati wa kutamatisha hadithi mwandishi hurejelea matukio ya mwanzoni mwa hadithi. Mifano ya hadithi hizi ni kama vile: “Shetani Hana Hatia” na “Safari ya Maangamizi” zilizomo katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Katika hadithi ya “Safari ya Maangamizi”, mwandishi anaanza hadithi yake hivi:

Mzee Majuto ambaye daima hurauka mapema alisikika nje ya nyumba yake akisemezana na mkewe (Uk. 154).

Dondoo hili linabainisha kuwa hadithi inaanza Mzee Majuto na mkewe wakiwa nyumbani. Baadaye hadithini tunaambiwa kuwa kulikuwa na msafara wa magari kuelekea kwa Mzee Majuto katika shughuli ya mazishi. Mwandishi anaendeleza hadithi yake hivi:

Msafara wa magari hatimaye uliondoka kuelekea nyumbani kwa Mzee Majuto. Baada ya kuwasili, waliwakuta watu sufufu ambao walikuwa wamefika kumuaga mmoja wao (Uk. 162).

Hatimaye, mwandishi anamalizia hadithi yake hapo nyumbani mwa Mzee Majuto. Mwandishi anaeleza hivi:

Kilio kikubwa kilipasua anga. Wengi walizirai, wengi walirukwa na akili, wakaanza kukimbia ovyo huku wakipiga unyende. Baada ya kumaliza kazi yake, Farida aligeuka na kuenda na hamsini zake (Uk. 171).

Mfano huu unaonyesha jinsi watu walivyohuzunika baada ya Farida kusoma barua mbele ya hadhira katika mazishi ya Pendo. Inabainika kuwa shughuli za mazishi zilitendeka nje ya nyumba ya Mzee Majuto. Kwa hivyo, hadithi hii inaanzia nyumbani mwa Mzee Majuto na inamalizikia hapo.

Hadithi nyingine inayotumia mwisho wa kimzunguko ni ile ya “Shetani Hana Hatia” inayopatikana kwenye diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Mwandishi anaanza kwa kutueleza kuwa Paka-shume yumo hospitalini na amefungwa kwa pingu. Anaeleza hivi:

Alitaka kujikuna kwenye kichwa ambacho sasa alianza kuhusu kuwa ni kizito kama kwamba kilikuwa kimehimili uzito wa duma nzima. Alipoinua mkono wake wa kushoto kufanya hivyo, alishangaa tena kugundua kuwa alikuwa katiwa pingu kwenye kitanda chake cha chuma (Uk. 53).

Baadaye hadithini tunagundua kuwa Paka-shume yumo kitandani mle hospitalini.

Hapo anakumbuka matukio ya awali. Mwishoni mwa hadithi mwandishi anaeleza hivi:

Daktari aliahidi kuwaletea keshoye. Wakati wote huu, Paka-shume alikuwa akisikiliza mazungumzo yao kwa siri, huku akijifanya amelala (Uk. 63).

Nukuu hii inathibitisha kuwa Paka-shume alikuwa bado yumo kitandani akimsikiliza daktari. Hadithi hii inaanzia Paka-shume akiwa kitandani na inaishia akiwa bado kitandani.

Diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* ina hadithi ya “Njozi ya Mtu Mweupe” ambayo haibainishi waziwazi dhamira ya mwandishi katika aya yake ya mwisho. Haielezi wazi falsafa ya mwandishi iliyomuongoza bali anamalizia kwa kuangazia maisha yajayo kati yake na Saida. Mwandishi anaeleza hivi:

Nililemewa sana na msiba wa kumpoteza babangu. Saida alinituliza na kunipa matumaini. Katika muda wa miezi michache tungeoana. Tungeishi hapo shambani, tuzae watoto na tuwe raia wa taifa lenye watu wa rangi na makabila tofautitofauti. Kufikia hapo, falsafa yangu ilikuwa imeniongoza vizuri sana na nilijua kwamba ingeendelea kuwa dira ya maisha yangu katika siku zijazo (Uk. 33).

Mwishowe, kuna hadithi ya “Daktari Strese” iliyomo katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* ambayo haituonyeshi dhamira ya hadithi bayana mwishoni mwake. Mwandishi anamalizia hivi:

Kila jioni Strese aliketishwa kitini sebuleni walimokuwa wazee wengine. Hapo ndipo walipopokea wageni waliokuja kumsabahi. Jioni ya leo, Daktari Strese alikuwa ameketi palepale kitini alipokuwa akiwekwa kwa muda ambao hakuutambua tena. Macho yake yalitazama picha zilizoonyeshwa kwenye runinga iliyokuwa mbele yake, bali hakuona kitu (Uk. 53).

Mfano huu unabainisha kuwa Dr Strese alikuwa kitini na alikuwa amedhoofika kiafya kwani hangeweza kuona picha zilizoonyeshwa katika runinga yake. Hata hivyo, hadithi hii haibainishi wazi katika dondoo hili lengo la mwandishi.

Hadithi tulizozijadili zimebainisha miundo tofauti ya kumalizia. Hali hii inaenda kinyume na maoni ya Vogler (2007) kuwa kila hadithi ni sawia kwa sababu zina miundo inayofanana. Hata hivyo, kuna hadithi zinazoisha kwa miundo sawia na ngano tulizojadili. Kwa upande mwingine, zipo hadithi zinazoisha kwa miundo tofauti na ngano hizo. Mifano ya hadithi zinazoonyesha miundo sawia ya kumalizia na ngano tulizojadili ni kama vile: hadithi ya “Njia ya Mwongo” inayopatikana katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* na hadithi ya “Uganga wa Pete” inayopatikana katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* zinazoishia kwa mwisho wa adili. Huku kubainisha funzo waziwazi mwishoni mwa hadithi ni kikale kwani inapatikana katika ngano tulizojadili.

Hadithi zinazoonyesha muundo wa kumalizia tofauti na ngano tulizojadili ni kama vile: Hadithi ya “Safari ya Maangamizi” na “Shetani Hana Hatia” zilizomo katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* zinatumia mwisho wa kimzunguko. Hali kadhalika, hadithi ya “Njozi ya Mtu Mweupe” iliyomo katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* na “Daktari Strese” iliyomo katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* hazionyeshi dhamira waziwazi mwishoni mwa hadithi kama zilivyo ngano. Hili linaashiria kuwa mtunzi wa hadithi fupi sio lazima aige mtindo wa ngano wa kubainisha funzo waziwazi mwishoni mwa kazi ya fasihi. Mtunzi huyu anaweza kuamua atunge hadithi inayoficha dhamira yake kuu.

2.3 Dhana ya Mtindo

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza mtindo kama ujuzi wa msanii kujieleza katika kazi yake. Kwa upande mwingine, Wamitila (2003) anaeleza mtindo kama mkusanyiko wa mbinu zinazomwezesha msanii kuwasilisha ujumbe wake kwa ufasaha. Hali kadhalika, Wamitila (2008) anaeleza mtindo kama sifa zinazotofautisha kazi fulani na nyingine. Kutokana na maelezo ya wataalam hawa, mtindo ni mbinu za kipekee zinazotofautisha kazi tofauti na kumwezesha mtungaji kuwasilisha ujumbe. Aidha, Mwinyi (2015) anaeleza kuwa utofauti huu hutokana na tofauti za kiujuzi, kihisia na kifalsafa za waandishi.

2.4 Mtindo wa Ngano na Hadithi Fupi

Russel (2009) anaeleza sifa za kimtindo zinazotambulisha ngano kama vile: lugha nyepesi inayotegemea fomula maalum, marudio ya maneno au virai au vishazi, matumizi ya dayolojia kwa wingi na pia motifu mbalimbali. Mitindo hii hujirudia kutoka ngano moja hadi nyingine. Baadhi ya sifa za kimtindo za ngano na hadithi fupi ni kama vile:

2.4.1 Urudiaji wa Maneno, Vishazi, Vifungu na Matukio

Wamitila (2003) anakiri kuwa urudiaji hupatikana katika tanzu za fasihi simulizi. Mbinu ya urudiaji huweza kujitokeza katika virai, sentensi, maneno na nyimbo. Hata hivyo, Adagala na Kabira (1985), Mulokozi (1996) na Oyoyo (2013) wanakubaliana kuwa urudiaji huu ni muhimu kwani hutilia mkazo ujumbe fulani. Adagala na Kabira (1985) wanaeleza kuwa:

Mara nyingi wimbo huweza kurudiwarudiwa ili kuteka hadhira. Urudiaji huu haupatikani tu katika wimbo bali pia katika matukio ili kusesitiza ujumbe fulani (Uk. xv).

Kwa upande wake, Hagan (1988) anaongezea mawazo ya Adagala na Kabira (1985) kwa kusema kuwa ngano huwa na lugha yenye sifa ya uradidi. Adagala na Kabira (1985) wanatumia mfano wa ngano ya “Kalisanga na Kaliteyo” miongoni mwa waluhya ili kuthibitisha kuwepo kwa urudiaji katika nyimbo zilizopo kwenye ngano za Kiafrika. Wanaeleza hivi:

Kaliteyo alienda msituni na kuanza kuimba:
Kalisanga, Kalisanga, Mtoto wa mama yangu,
Kalisanga
Utaenda kusiaga na nani?
Utakusanya kuni na nani?
Mtoto wa mama yangu, Kalisanga (Uk. 45).

Mfano huu unabainisha urudiaji wa jina ‘Kalisanga’. Hata hivyo, Kaliteyo anapomaliza wimbo huu baadaye anajibiwa hivi:

Kaliteyo, Kaliteyo
Mtoto wa mama yangu, Kaliteyo,
Utaenda kukusanya kuni na mama yako,
Utaenda kusiaga na mama yako,
Mtoto wa mama yangu, Kaliteyo (Uk. 46).

Wimbo huu aliouimba Kalisanga unabainisha urudiaji wa neno ‘Kaliteyo’. Mwandishi anaelezea kuhusu mtu ambaye Kaliteyo ataandamana naye kusiaga na kukusanya kuni.

Ngano ya “Sultan Darai” inayopatikana katika kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* inatumia mtindo huu wa urudiaji. Mwandishi wa ngano hiyo anatumia kuwa seremala aliporudi nyumbani kutoka kazini alimwambia mkewe awaite watoto waje kula. Hata hivyo, mkewe anamjibu ya kuwa watoto hawali mara mbili. Mwandishi anaeleza hivi:

Akamwambia waite watoto tule chakula.
Mwanamke akamwambia, Ah! Bwana watoto
wale mara mbili nami nimekwisha wapa sehemu zao..... (Uk. 17).

Hata hivyo, mhusika mkuu ambaye ni seremala anaporejea nyumbani mara ya pili anasema tu maneno yale tu na anajibiwa kwa maneno yale tu. Mwandishi anaeleza hivi:

Waite watoto waje kula chakula. Ah! Bwana!
Maneno niliyokwambia asubuhi hayakutosha?
Akamwambia, maneno gani bibi? Sikukwambia
vijana hawali mara mbili chakula... (Uk. 18).

Mara ya tatu, seremala anaporejea nyumbani anasema maneno hayo tu. Mwandishi anaeleza hivi:

Mumewe akanawa mikono. Akamwambia waite watoto tupate kula chakula. Ah! Mume wangu huna masikio? Maneno yayo hayo siku zote, ela vijana wakae kitako na chakula kimekwisha wakungojea wewe hata arudipo kazini, saa ya saa saba? Watoto hawa wangekufa na njaa, lakini miye hupika upesi maksudi, hawa vijana wale na mapema ili wasione njaa. Basi wewe kila siku unaporudi kazini huwaita watoto ule nao, wataka kuwalisha mara mbili au tatu haya basi mambo gani? (Uk. 26).

Urudiaji wa maneno ‘mara mbili’ na ‘waite watoto waje kula’ unabainika katika vifungu hivi vitatu kutoka ngano ya “Sultan Darai”. Hata hivyo, urudiaji huu unasisitiza ujumbe fulani katika ngano hii. Frye (1957) anaeleza hivi:

Kwa kuhakiki muundo wa kazi kivikale inabainika kuwa kuna matendo ya wahusika yanayojirudiarudia. Matendo haya huhusu matukio ya kila siku (Uk. 105).

Kutokana na maelezo ya Frye (1957), inabainika kuwa urudiaji wa matendo ya wahusika ni dhana ya kawaida. Mtunzi hurudia matendo haya ili kuibua maudhui yaliyozoeleka katika jamii. Hali hii inabainika wakati mtunzi wa ngano ya “Sultan

Darai” anaporudia kitendo cha seremala kuita watoto wale chakula. Kwa kufanya hivyo, mwandishi anaelezea maudhui ya upendo katika jamii.

Isitoshe, ngano ya “Sultan Darai” iliyomo kwenye kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* ina urudiaji wa baadhi ya maneno katika sentensi moja.

Maneno haya yanasisitizwa ili kuonyesha umuhimu wao. Mwandishi anaeleza hivi:

Ee bwana hushuki ukaenda kumtazama paa wako, hushuki kumtazama kiatu chako, hushuki kumtazama mboni ya jicho, hushuki kwenda kumtazama hisani wako, hushuki kumtazama msimamizi wako (Uk. 126).

Maneno haya yalisemwa na mkewe Maskini. Anarudia baadhi ya maneno ikiwemo ‘hushuki’ na ‘kumtazama’ ili kumsisitizia Maskini kuwa ni jambo la busara kuenda kumjulia hali paa wake.

Hali kadhalika, Park (2004) anaeleza kuwa ngano huwa urudiaji wa silabi ‘-ka’. Silabi hii hutumiwa kuonyesha wakati katika ngano. Ngano ya “Liyongo” iliyomo kwenye kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* ina urudiaji wa silabi ‘-ka’. Mwandishi anaeleza hivi:

Akaenda kuwaambia watu mjini, ya kwamba amekufa, wakaenda kumtazama, wakamwona amekufa, wakamzika na kaburi lake laonekana katika Ozi hata leo (Uk. 452).

Aidha, ngano huweza kurudia silabi ‘-ja’. Mfano ni ngano ya “Sultan Darai” iliyomo kwenye kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*.

Mwandishi anaeleza hivi:

Akamwambia, na mimi tokea siku aliokufa paa yule, sijala chakula, wala sijanywa maji, sijanena, wala sijacheka (Uk. 134).

Urudiaji wa silabi ni mtindo ambao umeigwa na baadhi ya kazi kutoka kazi za awali. Frye (1957) anaeleza kuwa ili kuhakiki fasihi ni lazima tuangalie dhana ya urudiaji kwani ndio msingi wa utamaduni. Aidha, anathibitisha urudiaji wa silabi kwa kueleza hivi:

Mashairi ya Mariane Moore yaliyoandikwa na Sabina (1935) yana urudiaji wa maneno na silabi. Silabi hizi zinajitokeza mwishoni mwa mshororo wa kwanza na nane (Uk. 278).

Kwa upande wa mwingine, kuna hadithi ya “Waliohujumu Ujamaa” iliyomo katika diwani ya *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* inayotumia mtindo wa urudiaji. Mwandishi anarudia baadhi ya maneno katika wimbo ulioimbwa na Sungura aliposikia habari kuhusu kifo cha Fisi. Mwandishi anaeleza hivi:

Wasifu wake ukawa wimbo:
Mtoto lia, ulie sana
Kufiwa na mjomba hilo nalo si mzaha Lia, ulie sana
Lakini lia ukipepesua
Lia ujibanze kwa mama
Kichwa cha maiti kugemea upanga na shoka!
Lia si jambo dogo kufiwa na mjomba (Uk. 117).

Nukuu hii inaonyesha kuwa Sungura alikuwa anawahimiza familia yake Fisi waendeleo kulia. Hali kadhalika, maneno kama vile: ‘lia’ na ‘ulie’ yanarudiwa katika wimbo huu.

Mfano mwingine wa wimbo uliomo katika hadithi hiyo ya “Waliohujumu ujamaa” ni wimbo wa Sungura unaoeleza kuhusu umuhimu wa Fisi kwake. Sungura anaimba hivi:

Kaka ee, kaka
Kaka ee, kaka
Unaniacha ba nani kaka?
Umekuwa ndiye baba
Umekuwa ndiye mama
Kaka ee, kaka
Wabaki na nani kaka? (Uk. 111).

Nukuu hii inabainisha kuwa sungura alimtegemea sana Fisi. Isitoshe, mwandishi anarudia vishazi ‘kaka ee’ na ‘umekuwa ndiye’.

Isitoshe, hadithi ya “Uganga wa Pete” inayopatikana katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* inabainisha urudiaji wa neno ‘usiku’ wakati Maskini anaposisitiza kuwa uganga wake hufanyika wakati huo. Mara ya kwanza Maskini anapoitwa ili aweze kubaini mahali ilipo pete ya mfalme anasema kuwa uganga wake hufanyika usiku. Anaeleza hivi:

Maskini alijitia ujasiri kwa kusema kuwa hilo lingetekezwa ila alisema mambo yake ya kiganga hufanyika usiku (Uk. 101).

Kisa kingine kinatukia wakati mtumishi wa mfalme anapokuja kumtafuta Maskini ili kumweleza kuhusu farasi aliyetoweka. Kwa mara nyingine, Maskini anaeleza kuwa uganga wake hufanywa usiku. Mwandishi anaeleza hivi:

Maskini aliporudi nyumbani, alijiwa na mtumishi wa mfalme.
Mtumishi alimweleza kuwa mfalme amempoteza farasi wake
na alitaka mganga
amsaidie kumweleza kama huyo farasi yuko wapi.
Wakati huo wote mkewe amejikalia jikoni kajitia hamnazo.
Kwa mara nyingine, Maskini alikariri kuwa kama mganga
mambo yake hufanywa usiku..... (Uk. 103).

Mwishowe, mali ya mfalme inapoporwa na wezi. Maskini anaitwa ili kutambua
wezi hao. Hata hivyo, Maskini anarudia maneno yale yale aliyozoea. Mwandishi
anaeleza hivi:

Jukumu hili lilikuwa gumu na nzito na lilimfadhaisha sana
Maskini. Hakujua kama ajitoe vipi. Kwa mara nyingine,
akaomba arudi nyumbani kwake kwa kujidai kuwa mambo
yake yeye hufanya usiku.... (Uk. 104).

Urudiaji huu wa maneno yale kuwa ‘uganga hufanyika usiku’ unasisitiza maudhui
ya hekima. Kwa kupitia maneno haya, Maskini anajiepusha mara tatu kugunduliwa
kuwa yeye si mganga halisi. Hadithi hizi za “Uganga wa Pete” na “Waliohujumu
Ujamaa” zinabainisha urudiaji wa maneno. Hali hii ni sawia na ngano tulizojadili
za “Sultan Darai” na “Kalisanga na Kaliteyo”. Urudiaji wa baadhi ya maneno na
silabi katika fasihi huweza kuonyesha kuwa baadhi ya kazi ziliiga mtindo huu
kutoka kwa kazi nyinginezo. Hali kadhalika, Mwinyi (2015) anaeleza kuwa
urudiaji wa silabi huweza kujitokeza katika mashairi. Akitumia ngano ya “Asili ya
Mwezi Kapatwa” anaeleza hivi:

Saba! Saba!
Tonge zangu saba si baba
Mpaka nitashiba
Saba! Saba!

Mfano huu unabainisha urudiaji wa vina ‘-ba’ katika shairi. Aidha, Frye (1957) anaeleza kuwa mashairi huweza kuiga mashairi mengine yaliyotungwa awali. Kwa msingi huu, shairi hili linaweza kuwa limeiga mtindo wa urudiaji kutoka mashairi ya awali. Aidha, kuna uwezekano kuwa hadithi ya “Uganga wa Pete” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* imeiga mtindo wa urudiaji kutoka kwa hadithi simulizi yaani ngano.

Isitoshe, Mbuthia na Iribemwangi (2014) wanasema kuwa mbinu ya urudiaji huweza kupatikana katika hadithi fupi. Wakitumia mfano wa hadithi ya “Juma Kamwambia Mke Akidhani ni Mama Mwenye Nyumba Waliopanga” wanabainisha kuwa kuna urudiaji wa jina Juma. Mbuthia na Iribemwangi (2014) wanaeleza kuwa mwandishi wa hadithi hii amerudia jina la Juma ili kutuonyesha matatizo anayopitia Juma kutokana na kuajiriwa na mwajiri katili. Hali hii inamfanya akose kumtambua mke wake anapozungumza naye.

Kwa upande mwingine, kuna hadithi zisizobainisha urudiaji huu wa matukio na maneno. Baadhi ya hadithi hizo ni: hadithi ya “Safari ya Maangamizi”, “Njia ya Mwongo”, “Shetani hana Hatia”, “Mwavyaji wa Roho”, “Dr. Strese” na “Kadhia ya Sikujua”. Hadithi hizi zinaelezea matukio mara moja tu bila kuyarudia. Kwa kufanya hivi waandishi wa hadithi hizi hawasisitizi baadhi ya maudhui hadithini. Kwa mfano katika hadithi ya “Njia ya Mwongo” mwandishi anatueleza kuhusu jinsi Kipkorir na Kipchumba walivyoenda kuogelea badala ya kuangalia mifugo wao. Anaeleza tukio hili mara moja tu hadithini. Hali hii inaonyesha kuwa urudiaji

sio lazima ujitokeze katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Hata hivyo, urudiaji ni mbinu ya kawaida katika tanzu za fasihi simulizi ikiwemo ngano.

2.4.2 Mtindo wa Nambari

Liabenow (2014) anaeleza kuwa nambari huwakilisha mila, utamaduni, dini, asili na mbinu za utambaji wa ngano. Kwa upande wake Solovyeva (2015) anashadidia maoni haya kwa kueleza kuwa nambari hizi zinazojitokeza katika ngano huwa tofauti kutoka ngano moja hadi nyingine. Wa Mutiso (2014) naye anaongezea kwa kueleza kuwa nambari haziwakilishi tu matukio ya kiajabu pekee bali huweza kutumiwa kivitakale. Nambari hizi huweza pia kutambulisha ngano za jamii fulani (Masoud, 2015). Aidha, Wa Mutiso (2014) anabaini kuwa nambari hazijitokezi katika fasihi simulizi pekee bali pia fasihi andishi. Wa Mutiso (2014) anatumia mfano wa utenzi wa Fatumah kuelezea matumizi ya nambari nne. Anaeleza kuwa mwandishi ametumia nambari nne kuelezea malaika wanne, siku nne takatifu, makhalifa wanne na miezi minne takatifu.

Kwa upande mwingine, Solovyeva (2015) anaeleza kuwa nambari mbili hutumika zaidi kifomula katika ngano. Senkoro (2011) anaongezea kwa kusema kuwa nambari mbili huhusishwa na wema na uovu. Russel (2009) na Gatricya (2014) wanakubaliana kuwa ploti ya ngano huhusisha mfumo unaojirudiarudia na unaoweza kubashirika. Russel (2009) anatoa mfano wa nguruwe watatu na dubu watatu. Aidha, Guerin (2005) akimnukuu Frye (1957) anaeleza kuwa urudiaji wa nambari tatu ni kikale na huweza kuashiria dhana mbalimbali. Akitumia mtazamo

wa kidini anaeleza kuwa nambari hii huweza kuashiria utatu mtakatifu. Urudiaji huu wa nambari tatu kifomula huweza kupatikana katika ngano ya “Abunuwasi Alikufa na Akafufuka” iliyomo kwenye kitabu cha *Myths and Legends of the Swahili*. Mwandishi anatumia nambari tatu kuelezea mara ngapi Abunuwasi alianguka, siku ngapi alibaki akiwa amelala na mara ngapi tarumbeta ililia. Kwa msingi huu, inaonekana kuwa mambo hutendeka mara ya tatu. Mwandishi anaeleza hivi:

Akasema hivi: Siku ambayo punda wako atateleza mara tatu utakufa! Siku nyingi baadaye, Abunuwasi alikuwa akisafiri akiwa juu ya punda wake mzee. Punda aliteleza mara ya kwanza na ya pili. Punda alipoteleza mara ya tatu, Abunuwasi alianguka chini akasema maombi na kulala. Alibaki katika hali hiyo kwa siku tatu wakati.....Mpigaji tarumbeta alipokuja alipokuwa Abunuwasi aliipuliza tarumbeta yake mara tatu (Uk. 113).

Hata hivyo, urudiaji wa kinambari huweza kujitokeza katika ngano bila kuandika nambari hizo. Mfano ni kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* ambacho kina ngano ya “Sultan Darai” kinachorudia tukio moja mara tatu. Mwandishi anarudia maneno ‘waite watoto wale mara tatu’. Aidha, ngano hii ya “Sultan Darai” inagawanya wahusika wake na vifaa kwa mtindo wa uwili. Japo mwandishi haandiki moja kwa moja nambari mbili anaonyesha kuwa ameathirika na mtindo wa nambari mbili katika kugawa kwake. Mwandishi anaeleza hivi:

Aliondoka seremala, akaenda kuoja mke. Akakaa na mke wake miaka mingi hatta akapata kijana mwanamke. Yule mkewe akapatikana na ugonjwa hatta akafariki dunia, akakaa na mtoto wake mdogo (Uk. 12).

Nukuu hii inabainisha kuwa seremala na mwanawe waliishi wakiwa watu wawili baada ya mkewe kufa. Baadaye ilimbidi seremala kutafuta mke mwingine ili aweze kumsaidia kutunza mwanawe. Hata hivyo, anatafutiwa mke aliye na mtoto. Mwanamke huyu anakuja na mwanawe kwake seremala. Mwandishi anaeleza hivi:

Naye ana mtoto mmoja mwanamke, aliyeachiwa na marehemu mumewe (Uk. 14).

Kisa kingine katika ngano hiyo ya “Sultan Darai” kinacholeta dhana ya uwili ni wakati seremala anapouliza kuwa mwanamke huyo atahitaji nini. Mwandishi anaeleza hivi:

Mwanamke akamwambia, “mimi sina neno, maadamu yamewasili mahari na nguo sina jambo” (Uk. 14).

Mfano huu unabainisha kuwa mwanamke huyo alihitaji vitu viwili. Navyo ni: mahari na nguo. Mwishowe, katika ngano hiyo ya “Sultan Darai” mwandishi anatumia dhana ya uwili kutofautisha vyakula. Anaeleza hivi:

Akatoka kwenda zake kazini, mwanamke akapika chakula jioni, kabla hajaja mumewe, akawapakulia watoto, akampa mwanawe wali mwema na yule akampa ukoko, tena uliungua (Uk. 18).

Mfano huu unathibitisha kuwa mke wa seremala aliwapa watoto wali aina mbili: wali mwema na wali uliungua. Mfano huu unatuonyesha kuwa nia ya mwandishi ni kulinganua vyakula hivi.

Ngano hii ya “Sultan Darai” inatumia nambari mbili kuelezea ni mara ngapi watoto wanakula. Mwandishi amerudia nambari ‘mbili’ mara tatu katika ngano hii. Matumizi ya nambari katika ngano hizi sio kisadfa tu bali nambari hizi kimaksudi.

Jung (1975) anaeleza kuwa nambari hazitumiki kisdafa tu bali kila nambari ina maana katika jamii. Aidha, Guerin (2005) akimnukuu Frye (1957) anamuunga mkono kwa kueleza kuwa nambari hutumika kivikale. Anatumia mfano wa nambari nne ambayo huwakilisha misimu minne katika mwaka. Isitoshe, Masoud (2015) anabainisha majukumu mbalimbali ya motifu ya nambari katika ngano za wapemba. Masoud (2015) anaorodhesha majukumu yafuatayo ya motifu ya nambari: kutambulisha jamii, kudhihirisha ujaala, kudokeza utamaduni na falsafa za wanajamii na pia kupamba kazi ya fasihi.

Kwa upande mwingine, mtindo wa utatu huweza kujitokeza katika urudiaji wa matukio ya hadithi fupi. Katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* kuna hadithi ya “Uganga wa Pete” inayorudia tukio la Maskini kusema kuwa ‘uganga wake hufanywa usiku’ mara tatu.

Katika hadithi ya “Kadhia ya Sikujua” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* mwandishi anatumia mtindo wa uwili kuelezea idadi ya wahusika bila kuandika idadi mahususi hadithini. Mwandishi anaeleza hivi:

Mke wa kwanza ni Rehema na wa pili ni Juha (Uk. 119).

Mfano huu unathibitisha idadi ya wake Bwana Sikujua alikuwa nao. Alikuwa na wake wawili. Nao ni: Bi Juha na Bi Rehema.

Mwandishi anaeleza kuwa kila mke alikuwa na watoto wawili bila kutaja nambari waziwazi. Anaeleza hivi:

Watoto wa Bi. Rehema ni Staha na Binti Baraka.
Nao wa Bi. Juha ni Kazibure na Binti Hiana (Uk. 119).

Nukuu hii inathibitisha kuwa kila mke alikuwa na watoto wawili. Watoto wa Bi. Juha walikuwa ni Kazibure na Binti Hiana ilhali watoto wa Bi. Rehema walikuwa ni Staha na Binti Baraka. Mtindo huu wa nambari ambao unajitokeza katika ngano ya “Abunuwasi Alikufa Akafufuka” umekuwepo tangu kitambo. Aidha, mtindo huu unaonekana kuigwa na hadithi ya “Kadhia ya Sikujua” japo si wazi. Mwandishi wa hadithi ya “Kadhia ya Sikujua” anaonekana kutumia mbinu ya uwili kulinganisha vitu. Hali hii ni sawia na katika ngano ya “Sultan Darai”.

Isitoshe, mtindo wa nambari umetumika katika kazi ya fasihi kutoka jadi. Ndiposa, Jung (1975) anaeleza kuwa nambari zimetumiwa kivitokele tangu jadi na inaendelea kutumika kila siku. Aidha, anaongezea kuwa nambari zina maana katika jamii. Hali kadhalika, Jung (1975) anaeleza hivi:

Kila kitu kiliumbwa duniani na mwanadamu isipokuwa nambari. Nambari ziliumbwa na Mungu mwenyewe (Uk. 28).

Mfano huu unabainisha kuwa mtindo wa kutumia nambari ni wa kale mno. Aidha, Timammy na Swaleh (2013) wanaeleza kuwa ukuruba baina ya ngano na hadithi fupi unatokana na mitindo sawia baina ya tanzu hizi inayohusishwa na fasihi simulizi. Kwa msingi huu, inawezekana kuwa mtindo wa nambari ambao umetumika katika tanzu za fasihi simulizi haswa ngano umeigwa na tanzu za fasihi andishi kama vile hadithi fupi.

Kwa upande mwingine, hadithi ya “Safari ya Maangamizi”, “Njia ya Mwongo”, “Shetani hana Hatia”, “Mwavyaji wa Roho” na “Dr. Strese” hazionyeshi matumizi ya mtindo wa nambari moja kusheheni hadithi nzima.

2.4.3 Safari na Msako

2.4.3.1 Safari

Safari ni kitendo cha kuondoka eneo moja na kuelekea eneo lingine. Eneo hili huwa ni mbali na sehemu alipo msafiri. Senkoro (1997) na Kunene (1985) wanakubaliana kuwa kazi yoyote ya fasihi huwa na aina mbili za safari. Nazo ni: safari ya nje na safari ya mawazo/ kisaikolojia. Safari ya kimawazo ni safari inayofikirika yaani iliyo mawazoni mwa mtu. Katika safari hii, msomaji hupelekwa katika eneo lisiloafiki kuitwa ya kihalisia. Safari hii inajitokeza katika riwaya ya Shabaan Robert ya *Kusadikika*. Kwa upande mwingine, safari ya nje ni safari inayohusu kuenda sehemu inayoweza kuitwa eneo la kihalisia. Mfano wa ngano inayohusu safari ya nje ni ngano ya “Liyongo”.

2.4.3.2 Msako

Msako ni hali ya kumtafuta mtu au kitu kilicho na manufaa kwa mhusika. Wakati mhusika anapoenda kukisaka kitu hiki anakumbwa na vikwazo vingi katika safari yake. Mhusika huyu mara nyingi huwa ni shujaa anayetegemewa na jamii. Shujaa ana wajibu wa kutekeleza masuala fulani. Utekelezaji wa masuala haya hurejesha hali ya utulivu katika jamii. Mfano wa kazi ya kifasihi iliyo na maudhui ya msako ni hadithi ya “Mfalme na Majitu”. Katika hadithi hii, mfalme Jabu Nene anamtuma

mwanakijiji mmoja ili kutafuta mkia wa jitu. Inaaminika kuwa mkia huo utamaliza ukame katika eneo lao la Udurubo. Hali hii inaonyesha kuwa msako ni mbinu mojawapo inayotumiwa katika fasihi hasa kazi za fasihi zinazohusu mashujaa. Katika kazi hizi zinazohusu mashujaa, msako hutumiwa kama mbinu ya kuiokoa jamii kutokana na tatizo fulani.

2.4.3.3 Motifu

Wamitila (2003) anaeleza motifu kama elementi ya kimuundo na kimaudhui inayotawala kazi fulani. Kwa upande mwingine, Mulokozi (2009) anaeleza motifu kama kipengele radidi cha kijadi au kimaudhui kinachotumiwa na wasanii katika kazi zao ili kutoa ujumbe fulani. Hali kadhalika, Nyamsenda (2015) anaeleza motifu kama dhana inayorudiwarudiwa katika kazi za fasihi. Kijumla, motifu ni kipengele cha kimuundo, kimaudhui, wahusika na kimtindo kinachorudiwarudiwa katika kazi ya fasihi ili kutoa ujumbe fulani. Mfano wa motifu unajitokeza katika utendi wa “Liyongo” iliyomo katika kitabu cha *Tenzi Tatu za Kale* (1999). Utendi huu umetawaliwa na safari nyingi ikiwemo: safari ya Liyongo kuelekea Pate, safari ya Liyongo kuelekea msituni baada ya kutoroka gerezani na safari ya kijakazi Saada kuelekea gerezani kumpelekea Liyongo chakula. Kipengele hiki cha safari kimetawala utendi huu kwa hivyo ni motifu.

2.4.3.4 Motifu ya Msako na Safari

Nyamsenda (2015) anaeleza kuwa ngano za safari na msako ni ngano ambazo dhamira kuu hujengwa katika safari na msako wa mhusika mkuu ambaye ni shujaa. Frye (1957) anaeleza kuwa katika visakale kuna safari ya shujaa ambapo anazaliwa, anaendeleza safari kuelekea kifo chake, kupotea kwa shujaa na kuzaliwa kwa shujaa mwingine. Katika safari hii, shujaa huweza kukumbana na vikwazo. Hata hivyo, ili shujaa asafiri lazima awe na jambo linalomchochea kusafiri. Aidha, Kemunto (2015) anaorodhesha sababu zinazomfanya shujaa kuandaa safari. Kemunto (2015) anaorodhesha sababu zifuatazo: kutafuta utambulisho, kutafuta nchi nzuri ambayo jamii imeahidiwa, kutafuta mbinu za kulipiza kisasi, kuwaokoa wanajamii, kusaka hekima na busara na kuwaokoa wanajamii kutokana na janga fulani. Kwa upande wake Guerin (2005), safari ya shujaa humpa wajibu ambayo lazima atekeleze ili kuiokoa jamii yake. Guerin (2005) anaeleza hivi:

Katika msako shujaa huenda safari ndefu. Safari hii humpa majukumu ambayo lazima atekeleze ili aiokoe jamii yake. Aidha, shujaa hukumbwa na matatizo mengi katika safari hii ikiwemo kujibu vitendawili vigumu (Uk. 190).

“Ngano ya Liyongo” iliyomo katika kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* ina kipengele cha safari. Mwandishi wa ngano hii anatuelezea kuhusu safari ya maisha ya mhusika Liyongo hadi kuelekea katika kifo chake. Safari hii anaianza akiwa peke yake. Mwandishi anaanza ngano kwa kutuelezea kuhusu mhusika Liyongo ambaye anawadhulumu wanakijiji wa Shanga kwa kuwakataza

kuchota maji kisimani na kuchanja kuni. Licha ya kuwa Liyongo ana nguvu nyingi anatumia uwezo wake kwa maslahi yake tu wala hasaidii jamii yake. Hali hii ni kinyume na utungo wa *Mkasa wa Shujaa Liyongo* uliotungwa na Matundura (2001). Katika kitabu hiki, Liyongo anasawiriwa kama mtetezi wa wanyonge. Hali hii ni kinyume na “Ngano ya Liyongo” iliyomo katika kitabu cha Steere inayosawiri Liyongo kama adui wa jamii. Katika kitabu cha *Mkasa wa Shujaa Liyongo* mwandishi anatuonyesha jinsi Liyongo alivyomwokoja kijana mmoja aliyekamatwa mguu na mamba.

Isitoshe, katika safari hii iliyomo katika kitabu cha Steere Liyongo anakumbana na matatizo si haba kama vile kufungwa gerezani. Liyongo anafungwa gerezani lakini hatimaye anafaulu kutoroka kuelekea msituni kwa minajili ya kuokoa maisha yake. Safari ya kuelekea msituni ni ya kulazimishwa kwani anatoroka ili aokoe maisha yake. Kupelekwa gerezani kwa Liyongo kunamtenganisha na jamii yake na baadaye anapotoroka anarudi kujumuika na wanajamii ikiwemo mtotowe. Ndiposa, Frye (1957) anaeleza kuwa katika visakale shujaa lazima aishi mbali na jamii yake, abadilike kifikra au kitabia na arejee kwa jamii yake mwishowe.

Liyongo anapotaka kutoroka gerezani hafanyi hivi peke yake bali anaomba usaidizi kwa watu walio karibu naye. Akitumia shairi anamtuma kijakazi amwambie mamake amwekee tupa kati kati ya mkate wa wishwa. Liyongo anatumia tupa hii kukereza minyororo na kutoroka kuelekea msituni. Baadaye, mfalme anatumia wanakijiji wengine ili wamuangamize Liyongo wakati wa kuchuma mikoma. Hata

hivyo, Liyongo anagundua hila yao na kuwakwepa. Hatimaye, mfalme anaamua kumtumia mtoto wake Liyongo ili kumuangamiza Liyongo.

Japo Liyongo anatambua kuwa mtotowe anataka kumuangamiza, anamuambia siri ya nguvu zake. Mtoto huyu anafaulu kumuangamiza Liyongo kwa kutumia sindano ya shaba. Anafanya hivi ili aweze kupewa ufalme. Mwandishi anamsawiri mkinzani huyu wa Liyongo kama mlafi. Mtoto wake Liyongo anasahau uhusiano alio nao na Liyongo kwani anaamua kumuangamiza ili aweze kupewa ufalme. Hata hivyo, anajuta kwani badala ya kupewa ufalme anashikwa na kutiwa gerezani.

Liyongo anaangamia kwa sababu anasalitiwa na mtoto wake. Anamuamini mtoto wake na kumuambia siri ya nguvu alizonazo. Hali hii inaoana na hadithi ya Samsoni na Delila katika Biblia. Samsoni alimuamini mkewe Delila na akamuambia siri ya nguvu zake. Anapofanya hivi basi anasalitiwa na Delila. Delila anamsaliti kwa Wafilisti. Anafanya hivi kwa maslahi yake mwenyewe kwani alilipwa fedha. Hali ya shujaa kuanguka kutokana na matendo yake ni dhana ya kawaida katika visakale. Ndiposa, Guerin (2005) anaeleza kuwa shujaa lazima aanguke ili afidie dhambi za wanajamii. Hata hivyo, hali hii ni kinyume kwani kufa kwa Liyongo haikuwa kwa sababu ya kufidia makosa ya wanajamii.

Frye (1957) anaeleza kuwa shujaa huweza kuanguka kutokana na udhaifu wake kitabia. Hali kadhalika, Frye (1957) anaongezea kuwa udhaifu huu huweza kutokana na kiburi alicho nacho mhusika. Mhusika huyu huwa hataki kusikiliza mawaidha ya wenzake na huweza kupotoka kimaadili. Mfano ni Samsoni wa

uyahudi ambaye alikatazwa na wazazi wake asimuo Delila. Samsoni anapuuza mawaidha ya wazazi wake. Kuanguka kwake kunasababishwa na Delila. Samsoni anaingia mtegoni kwa sababu alikaidi mawaidha ya wazazi wake. Baadaye, anasalitiwa na Delila. Hali hii inasababisha kuanguka kwake.

Ngano nyingine ni ile ya “Abunuwasi na Wezi Wawili” inayopatikana katika kitabu cha *Myths and Legends of the Swahili*. Katika ngano hii, mwandishi anatumia mtindo wa safari. Mwandishi anatueleza kuhusu safari ya Abunuwasi ambapo anaenda sokoni kwa minajili ya kununua kondoo. Hata hivyo, wakati anapokuwa njiani kuelekea nyumbani anakumbana na tatizo. Anavamiwa na wezi wawili ambao wanampokonya kondoo. Baadaye, Abunuwasi anaamua kulipiza kisasi. Mara ya kwanza, anawadanganya wezi wale wawili kuwa ana mti unaozaa dhahabu na wanamuamini. Matokeo ya kuamini huku ni Abunuwasi kupewa ng’ombe mia moja. Abunuwasi kwa weledi wake anatabiri kuwa wezi hao wataweza kuja kwake ili kulipiza kisasi. Anaamua kwa usaidizi wa mkewe kuwadanganya wezi hao kuwa ana kijiti chenye uwezo wa kufufua mtu. Wezi hao wawili wanaamini na kununua kijiti hicho. Matokeo ya kuamini huku ni mwizi mmoja kushikwa kutokana na kumuangamiza mwenzake.

Mwishowe, Abunuwasi anaishi kwa amani kwa kuwa anawashinda wapinzani wake. Hali hii ni kinyume na maelezo ya Guerin (2005) kuwa shujaa lazima afe. Tofauti kati ya Liyongo na Abunuwasi ni kuwa Abunuwasi anawashinda maadui wake wote ilhali Liyongo anashindwa hatimaye. Kwa msingi huu basi, imebainika

kuwa sio lazima shujaa aanguke kwani kuna wakati shujaa anaweza kuwapiku maadui wake wote.

Hata hivyo, vitabu vya *Tenzi Tatu za Kale* (1999) na *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (2001) vinaonyesha safari ya ziada ambayo haipatikani katika kitabu cha Steere. Vitabu hivi vinasawiri safari ya Liyongo kutoka Shanga hadi Pate ili kuwaona Wagalla. Safari ambayo inamchukua Liyongo siku mbili tu badala ya siku nne.

Ngano hizi mbili yaani ya “Liyongo” na “Abunuwasi na Wezi Wawili” zina sifa fulani zinazofanana. Kwanza kabisa, wahusika hawa wanafunga safari wakiwa peke yao. Katika safari hii, wahusika wakuu wanakumbwa na changamoto kwa mfano Abunuwasi anafumaniwa na wezi ilhali Liyongo anatiwa gerezani. Isitoshe, wahusika wakuu wanathibitisha uwezo mkubwa kwani wote wana uwezo wa kutabiri mambo yatakayotokea kwa mfano Abunuwasi kutabiri wezi kuja kulipiza kisasi ilhali Liyongo anatambua kuwa mwanawe anataka kumuangamiza. Hali kadhalika, Liyongo na Abunuwasi wana wapinzani na wote wanapigania maslahi yao. Mwishowe, wahusika nguli yaani Liyongo na Abunuwasi katika ngano hizi wamepewa usaidizi ili kutatua changamoto zinazowakumba kwa mfano Liyongo kusaidiwa na mamake kutoroka gerezani na bibi yake Abunuwasi kumsaidia Abunuwasi ili kuwahadaa wezi wawili.

Kipengele cha safari hakibainiki tu katika ngano bali pia hadithi fupi. Kwa mujibu wa Nyamsenda (2015) motifu ya safari hupatikana katika fasihi simulizi na fasihi andishi. Hata hivyo, sio lazima safari hii iwe ya nje tu bali pia inaweza kuwa safari

ya kisaikolojia. Mfano wa safari ya kimawazo umo katika kitabu cha *Kusadikika*.

Mwandishi anaeleza hivi:

Kusadikika ni nchi ambayo kuwako kwake hufikirika kwa mawazo tu. Nchi hiyo iko katikati ya mipaka sita. Kwa upande wa kaskazini imepakana na upepo wa kaskazini na kwa upande wa kusini imepakana na upepo wa kusi. Mashariki imepakana na Matlai na Magharibi mpaka wake ni upepo wa umande. Kwa kuwa nchi yenyewe inaelea katika hewa kama wingu, zaidi ya kupakana na pepo nne hizo mna mipaka mingine (Uk. viii)

Mfano huu unaonyesha jinsi mwandishi anavyotusafirisha hadi nchi ya Kusadikika.

Anabainisha wazi kuwa nchi yenyewe ni ya kufikirika. Hali kadhalika, anasawiri sehemu zinazopakana na nchi hiyo.

Katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* kuna “hadithi ya Safari ya Maangamizi” inayoelezea safari ya maisha ya mhusika Pendo. Safari hii inaanza Pendo akiwa nyumbani na kuisha akirudishwa nyumbani akiwa maiti. Pendo anaondoka nyumbani kuelekea Chuo Kikuu cha KwenuKwetu. Pendo alikuwa msichana wa kwanza kutoka kijijini Sechu kuingia Chuo Kikuu. Anapofika huko anaendelea kutia bidii masomoni. Aidha, anakuwa mwanafunzi aliye na nidhamu ya hali ya juu kiasi kuwa wanakijiji walitaka kumchagua kuwa mbunge. Hata hivyo, ananjisiwa na wanaume ambao wanamuambukiza virusi vya Ukimwi. Baada ya kunjisiwa anabadilika kitabia. Anaamua kulipiza kisasi kwa kuwaambukiza wanaume kijijini virusi hivyo. Baadaye anapokaribia kuaga dunia anajuta na kuamua kuandika barua ya kuomba msamaha. Hatimaye, Pendo anaaga dunia na kurudishwa nyumbani ili kuzikwa.

Hadithi hii ya “Safari ya Maangamizi” inaonyesha masuala mbalimbali kuhusu maisha ya Pendo. Kwanza kabisa, Pendo anaanza safari akiwa peke yake kwani anaenda Chuo Kikuu peke yake. Akiwa chuoni anatia bidii na kuwa na tabia njema. Hali hii inawafanya wanakijiji kutaka kumchagua kuwa mbunge ili atetee maslahi yao. Hata hivyo, Pendo anakumbana na wakinzani wake ambao wanamnajisi. Baada ya kunajisiwa anabadilika kwani anafikiria maslahi yake na sio ya wananchi. Hii inathibitika wakati anapoamua kulipiza kisasi kwa kuwaambukiza wenzake virusi vya ukimwi. Mwananadharia wa vikale Frye (1957) anaeleza kuwa mhusika huweza kuanguka kutokana na kufanya makosa ambayo hangeweza kuepuka kwa sababu ya kukosa uwezo wa kuyadhibiti makosa hayo. Hali hii haiwezi kumuafiki Pendo kwani anadhulumiwa. Hatuoni kosa la Pendo katika kisa hiki.

Hadithi Nyingine inayotumia mtindo wa safari ni ya “Uganga wa Pete” iliyomo katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Mhusika mkuu ambaye anaitwa Maskini anafunga safari nyingi akiwa peke yake. Safari hizi zimechochewa na sababu tofauti. Mara ya kwanza, anaenda kwa Mama Vitumbua ili kuomba usaidizi. Mara ya pili, anafunga safari ili kuelekea kwa mfalme kwa minajili ya kumuambia mfalme sehemu ilioko pete yake. Japo Maskini anaona jambo hili kuwa gumu anasaidiwa na mkewe ambaye anamueleza kuwa pete hiyo ilimezwa na Jogoo. Mara ya tatu, Maskini anaenda kwa mfalme ili aweze kutafuta farasi aliyepotea. Inasadifu kuwa farasi alipotoweka alienda porini. Hapo porini ndipo alipokuwa mke wake Maskini. Maskini aliporejea nyumbani mkewe anamueleza pale alipo farasi. Mwishowe, Maskini anaitwa na mfalme ili aweze kumsaidia

kutafuta simba anayewasumbua wanakijiji. Mara hii tena anasaidiwa na mkewe ili kumpata simba huyo. Kutokana na kutatua matatizo yanayowakumba wanajamii, Maskini anatumizwa kwa kupewa wadhifa.

2.5 Hitimisho

Sura hii imeangazia sifa za kimuundo na kimtindo za ngano na hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Sifa za kimuundo kama vile: mwanzo wa hadithi, sehemu ya kati na mwisho wa hadithi zimejadiliwa. Aidha, sifa za kimtindo kama vile: motifu ya safari na msako, matumizi ya nambari na urudiaji wa maneno zimeangaziwa. Utafiti huu umebaini kuwa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili sio zao la mchakato wa kistari wa kutoka kwa ngano hadi kwa hadithi fupi. Hii ni kwa sababu hadithi fupi nyingi za kisasa za Kiswahili zimebainisha sifa za kimtindo na kimuundo zinazotofautiana na ngano. Sifa hizi ni kama vile: ufichaji wa dhamira ya mwandishi, mianzo isiyo ya kifomula na miishio isiyo ya kifomula. Aidha, kuna hadithi iliyoonyesha sifa zinazofanana na ngano tulizojadili. Hadithi hii ni ya “Uganga wa Pete” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Hadithi hii ina sifa kama vile: mwanzo wa kifomula, mwisho wa kifomula na urudiaji wa maneno na nambari. Sifa hizi zinapatikana pia katika ngano zilizomo katika vitabu vya *Myths and Legends of the Swahili* na *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*. Hata hivyo, sehemu ya kati ya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili na ngano hufanana. Hii ni kwa sababu katika ngano sehemu ya kati huwa na migogoro baina ya wahusika kwa sababu ya mitazamo tofauti. Aidha, ni katika sehemu hii ndipo mwandishi huendeleza dhamira yake kuu.

SURA YA TATU

MAUDHUI YA NGANO NA HADITHI FUPI YA KISASA YA KISWAHILI

3.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeangazia miundo na mitindo mbalimbali ya ngano na hadithi fupi. Katika sura hii, tumeangazia maudhui mbalimbali yanayoshughulikiwa katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili na ngano. Mtafiti amefanya hivi ili kubaini ikiwa maudhui yanayojirudiarudia katika ngano ni sawia na maudhui yanayojirudia katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.

3.1 Dhana ya Maudhui

Mohamed (1995) anaeleza maudhui kama jumla ya mambo yanayoangaziwa na mwandishi. Kwa upande mwingine, Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza maudhui kama ujumbe wa jumla kuhusu matukio, wahusika na hali ya maisha kama yanavyojitokeza katika kazi ya fasihi. Isitoshe, Wamitila (2002) anaeleza maudhui kama jumla ya masuala yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi. Aidha, Park (2004) anaeleza maudhui kama mawazo makuu yanavyojitokeza katika kazi za watambaji ama waandishi. Kutokana na maelezo ya wataalam hawa, maudhui ni masuala mbalimbali yanayowasilishwa na mwandishi au mtambaji kwa hadhira.

3.2 Maudhui ya Ngano na Hadithi Fupi

Sehemu hii imejadili maudhui. Baadhi ya maudhui yaliyojadiliwa yamedondolewa katika ngano na hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili. Maudhui haya ni kama vile: wema na uovu, ujanja, ushujaa na kifo.

3.2.1. Maudhui ya Wema na Uovu

Maudhui ya wema na uovu yanajitokeza katika baadhi ya kazi za kifasihi. O'Grady (2008) anaangazia asili ya wema na uovu kwa mtazamo wa kidini. Anaeleza kuwa wema na uovu ulianza wakati binadamu alipomuasi Mungu kwa kula tunda lililokuwa katikati mwa bustani ya Edeni. Tendo hili lilimfanya binadamu kuwa na uwezo wa kubaini kilicho chema na kilicho kiovu. Hali kadhalika, Feldkamp (2008) anaeleza kuwa uovu huhusishwa na shetani. Akirejelea kitabu cha *Paradise Lost* (2001) anaeleza kuwa baada ya Shetani kushindwa na Mungu katika vita anageuka kuwa mwovu kwa kuwa anataka kulipiza kisasi dhidi ya Mungu. Ibilisi anafanya hivi kwa kuwaongoza wanadamu ili wafanye maovu.

Frye (1982) anaongezea mawazo haya kwa kueleza kuwa Biblia imeathiri baadhi ya kazi za kifasihi ambapo wahusika wao wanagawanywa katika sehemu mbili yaani sehemu ya wema na sehemu ya uovu. Kutokana na maelezo haya, inabainika kuwa kazi za kifasihi ikiwemo ngano zina maudhui ya wema na uovu. Paul (1992) anaeleza hivi:

Ngano zinazotambwa huonyesha kuwa matendo mema lazima yatuzwe ilhali matendo maovu lazima yaadhibiwe. Aidha, ngano hizi hufundisha kuwa si vizuri kuwa mvivu au mchoyo (Uk. 13).

Mfano huu unathibitisha kuwa ngano huwa na maudhui ya wema na uovu. Hata hivyo, wema katika ngano ulituzwa huku uovu ukiadhibiwa. Aidha, Adagala na Kabira (1985) wanaeleza kuwa kuna mgogoro baina ya uovu na wema katika ngano. Mfano wa ngano unaobainisha mgogoro baina ya wema na uovu ni ngano

ya “Abunuwasi Apata Punda” iliyomo kwenye kitabu cha *Myths and Legends of the Swahili*. Ngano hii ina mhusika aitwaye Abunuwasi. Abunuwasi alikuwa anapendwa zaidi na khalifa Haruni Rashidi. Kwa sababu ya kupendwa kwake, anaonewa wivu na bawabu.

Bawabu anaamua kutomfungulia mlango Abunuwasi ikiwa hataahidi kumpa chochote atakachopewa na Haruni. Abunuwasi basi anaandika mkataba na bawabu. Baadaye, Abunuwasi anaenda kwa Haruni na kumjuza kuwa anamhitaji amchape viboko mia moja. Hata hivyo, baada ya kuchapwa viboko takribani kumi Abunuwasi anaomba nafasi ili apumzike. Anapopewa nafasi hiyo anatoa karatasi iliyokuwa na kandarasi baina yake na bawabu. Haruni anasoma kandarasi hiyo na kukasirika. Anaamua kumuadhibu bawabu kwa kumchapa viboko hamsini. Hatimaye, Abunuwasi anapewa pesa za kununua punda na Haruni.

Ngano nyingine inayoonyesha maudhui ya wema na uovu ni ngano ya “Sultan Darai” iliyomo kwenye kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*. Mwandishi anarudia tukio mara tatu ili kusesitiza maudhui ya uovu. Mwandishi anaeleza hivi:

Akatoka kwenda kazini, mwanamke akapika chakula cha jioni, kabla hajaja mumewe akawapakulia watoto, akampa mwanawe wali mwema na yule akampa ukoko, tena uliungua (Uk. 18).

Dondoo hili linabainisha uovu wa mke wake seremala kwani anampa mwanawe seremala wali uliungua wakati seremala hayumo nyumbani. Mwandishi

anamfanya mhusika huyu kurudia matendo haya mara tatu ili kuisisitiza maudhui ya uovu. Hali kadhalika, mwandishi amerudia tukio lingine mara tatu ili kuonyesha maudhui ya wema. Mwandishi anaeleza hivi:

Akamwambia waite watoto tule chakula. Mwanamke
akamwambia, Ah! Bwana watoto wale mara mbili,
nami nimekwisha wapa sehemu zao (Uk. 17).

Mfano huu unaonyesha upendo alio nao seremala kwa wanawe. Mwandishi anarudia tendo la seremala kuita watoto wale mara tatu katika ngano ya “Sultan Darai”. Japokuwa mwandishi anasisitiza maudhui ya wema, anaonyesha pia katika jamii hiyo ilikuwa kaida kwa mwanamume kula na wanao anapoondoka kazini. Seremala habaguwi watoto hao kwani anataka wale wote pamoja. Mke wa seremala anaadhibiwa kwa sababu ya uovu wake. Seremala anamuadhibu kwa kutafuta mtumwa mwanamke ili amtunze mwanawe. Mkewe seremala ni mbinafsi. Anamnyima mtoto wa seremala wali mwema. Hatimaye, mkewe seremala anaaga dunia. Hali hii inaoana na maoni ya Adagala na Kabira (1985) kuwa wasimulizi wa ngano huhimiza upendo katika jamii. Aidha, wasimulizi hao hukashifu tabia ya ubinafsi katika jamii.

Kuna hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zinazoishia kwa mhusika anayetenda maovu kuadhibiwa. Mfano ni hadithi ya “Shetani Hana Hatia” iliyomo kwenye diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Hadithi hii ina mhusika aitwaye Paka-shume. Paka-shume anamnajisi mpwawe. Baadaye anakamatwa na

kuadhibiwa vikali. Hadithi hii inaisha Paka-shume akiwa kitandani. Anatibiwa hospitalini kutokana na majeraha aliyopata alipopigwa na umati wa watu. Hatimaye, anajuta. Mwandishi anaeleza hivi:

Paka-shume alikuwa akisikiliza mazungumzo yao kwa siri akijifanya amelala. Mshale wa majuto ulimfuma. Alijutia unyama aliomtendea mpwa wake (Uk. 63).

Paka-shume anajuta kwa sababu ya mkasa uliompata. Kujuta kwa wahusika waovu ni dhana ya kawaida inayojitokeza pia katika ngano. Ndiposa, Adagala na Kabira (1985) wanaeleza hivi:

Maudhui makuu katika ngano ni utetezi wa haki. Msimulizi hutetea wanaodhulumiwa. Watoto, wanawake, wasiojiweza, mayatima, wanyonge na watumwa hutetewa na msimulizi. Wahusika hawa wanapokumbwa na majaribio au matatizo huibuka washindi hatimaye (Uk. xvi).

Maelezo haya ya Adagala na Kabira (1985) yanaonyesha jinsi msimulizi wa ngano hutetea wanyonge katika jamii. Hali hii ni sawia na hadithi ya “Shetani hana Hatia” ambapo mhusika Paka-shume ameadhibiwa kutokana na kumnajisi mpwawe. Kuadhibiwa huku ni mbinu ya mwandishi kumtetea mpwa wake Paka-shume.

Isitoshe, ngano tulizojadili za “Abunuwasi Anunua Punda” na “Sultan Darai” zinaonyesha kuwa wahusika waovu wanaadhibiwa. Dhana ya wahusika kukumbwa na mikasa ni dhana ya kale. Akithibitisha uwepo wa mikasa katika kazi ya fasihi, O’Grady (2008) anaeleza kuwa katika ngano za kishujaa mtu yeyote anaweza kupatwa na mkasa. Isitoshe, imebainika kuwa mhusika mwema hutuzwa. Mfano ni ngano ya “Abunuwasi Apata Punda”. Katika ngano hiyo, Abunuwasi anapewa pesa

ya kununua punda. Frye (1957) akieleza kuhusu mgongano baina ya wema na uovu anaonyesha kuwa wahusika wema hutuzwa. Anatumia mfano wa kitabu cha *Ayubu* kuonyesha jinsi Ayubu aliteseka kwa sababu ya mgongano huu. Hatimaye, baada ya mateso hayo yote anarudishiwa yale aliyoyapoteza. Aidha, anaongezewa zaidi yaani mara saba.

Hadithi ya “Dr Strese” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* ina mhusika aitwaye Strese. Mhusika huyu anajitahidi kila awezavyo ili kuwakimu dada zake. Mwandishi anatueleza kuwa alikuwa akiwalipia watoto wa dada zake karo ya shule. Hata hivyo, baada ya kufanya mema analipwa na maovu. Mwandishi anaeleza hivi:

Ulimwengu wa eneo lile ulifahamu yaliyoendelea lakini dada zake wala wapwa wake hawakushtuka wala kujali walipoambiwa habari za kaka yao ila kwenda kurithi nyumba ya baba yao tu (Uk. 53).

Mfano huu unatubainishia jinsi dada zake Dr. Strese hawakujali kumsaidia ndugu yao. Wanahiari kuenda kuitisha urithi wao badala ya kumsaidia. Mwandishi anamalizia hadithi hii kwa kutuonyesha jinsi Dr. Strese anavyoteseka. Mwandishi wa hadithi hii ananua tumhurumie mhusika. Licha ya kuwa mhusika huyu amekuwa mwema, anateseka sana mwishowe. Hali hii inaoana na maoni ya O’Grady (2008) kuwa katika kazi ya fasihi mhusika yeyote anaweza kukumbwa na mkasa awe mwema au mbaya. Aidha, mwandishi wa hadithi hii alitarajia kutelimisha kuwa tusitende mema tukitarajia kulipwa na mema baadaye. Isitoshe,

anaonyesha jinsi katika jamii ya kisasa kuna watu wengine ambao hata wakitendewa mema hawana shukrani.

Isitoshe, kuna hadithi ya “Kadhia ya Sikujua” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Hadithi hii ina mhusika Bwana Sikujua. Bwana Sikujua aliweza kutagusana vizuri na wanakijiji. Mwandishi anaeleza kuwa Bwana Sikujua alipendwa na watu kwa sababu ya Bi. Rehema. Bi. Rehema alikuwa ni mcha Mungu na msaidizi wa wote. Hata hivyo, anaamua kumwoa mke mwingine aitwaye Bi. Juha. Bwana Sikujua anasahau mke wake wa kwanza (Rehema) na kumshughulikia Bi. Juha. Anawatenga watoto wake Bi. Rehema. Anaamua kuwapa watoto wake Bi Juha urithi na kuwaacha watoto wake Bi. Rehema bila urithi. Baadaye, Bwana Sikujua anajutia matendo yake. Mwandishi anaeleza hivi:

Siku zimepita na mwone Sikujua akiomba msamaha.
Nisamehe mke wangu, Rehema, nilikuwa Juha Sikujua! (Uk.
127).

Dondoo hili linalopatikana katika hadithi hii linaonyesha jinsi Bwana Sikujua alivyojuta hadi ikabidi aombe msamaha. Kutokana na kuomba kwake msamaha inaonekana kuwa alitaka kubadilika. Hali hii ni sawia na baadhi ya ngano kwani ngano huwa na jukumu la kumrekebisha mtu. Hata hivyo, mwandishi wa hadithi hii hatuelezi ikiwa Bi. Rehema alituzwa hatimaye kutokana na matendo yake.

Mwishowe, kuna hadithi ya “Mwavyaji wa Roho” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Katika hadithi hii, mwandishi anatueleza jinsi wahusika kama vile Bwana Kitambi na Jael walivyokuwa matajiri kutokana

na uovu. Bwana Kitambi ni mnafiki, mfidadi na muuzaji wa dawa za kulevya. Kwa sababu ya utajiri wake hashikwi na yeyote. Mwandishi anaeleza kuwa alikuwa anamiliki mabasi mengi na soko la uuzaji na ubadilishaji wa hisa. Isitoshe, alipata pesa nyingi kutokana na uuzaji wa dawa za kulevya. Licha ya matendo haya yote anajitokeza waziwazi kujifanya kuwa anatetea haki za wananchi kwa kueleza kuwa anapigana dhidi ya dawa za kulevya. Hali hii inawafanya wengi kumpigia kura na yeye kuibuka mshindi. Mwandishi anaeleza hivi:

“Tumezaa wana wetu na kuwalea vyema, sasa nyinyi na biashara yenu muwafanye vizuu! Mimi nafaa jamani! Hakuna wa kuwadhibiti hawa papa na nyangumi? Uuui!”
Mama alilia (Uk. 79).

Dondoo hili linalopatikana katika hadithi ya “Mwavyaji wa Roho” linaonyesha jinsi mama analalamika. Mama huyo amewalea wana wake vyema. Hata hivyo, biashara ya dawa za kulevya inawaangamiza. Hadithi hii inaonekana kutuonyesha jinsi walio waovu katika jamii wanafanikiwa maishani na hata hawaadhibiwi. Bwana Kitambi ni tajiri mno. Utajiri wake unatokana na unafiki, uuzaji wa dawa za kulevya na ufidadi. Hali hii ni tofauti sana na ngano tulizojadili kwani badala ya uovu kuadhibiwa unatuzwa. Kulingana na mtafiti, ngano nyingi zilihimiza wanajamii kuwa na maadili mema. Ndiposa, katika ngano hizo wahusika wema walituzwa ilhali waovu waliadhibiwa.

Kwa upande mwingine, hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zinasawiri ukweli uliopo kuwa katika jamii ya kisasa kuna watu ambao wamefanikiwa maishani ilhali

wanatenda maovu. Watu hawa wanafanikiwa kwa sababu hawachukuliwi hatua za kisheria japo wanafanya matendo yanayoenda kinyume na sheria ya nchi. Mfano ni mhusika Bwana Kitambi aliye katika hadithi ya “Mwavyaji wa Roho” ambaye anauza dawa za kulevya ilhali hashikwi na kuwekwa gerezani.

3.2.2. Maudhui ya Ujanja

Ujanja ni hali ambapo mhusika hutumia hila ili kumhadaa mhusika mwingine. Mhusika mjanja hufanya hivi ili kujinufaisha. Mfano ni kisa ambacho Abunuwasi anatomia ujanja dhidi ya mwenzake ili aweze kupata sufuria ya mwenzake. Mara ya kwanza anaposaidiwa na sufuria anampa sufuria nyingine kwa madai kuwa sufuria yake imezaa. Anaposaidiwa sufuria mara ya pili harudishi. Aliyempa sufuria anapomuuliza anamuambia sufuria imekufa kwani chochote kizaacho pia kinakufa.

Wilkinson (2017) anaeleza kuwa maudhui ya ujanja yanajitokeza katika ngano zilizomo katika jamii mbalimbali. Ngano hizi huelimisha wanadamu dhidi ya kuhadaika haraka. Jacobi (2000) na Campbell (2004) wanaeleza kuwa maudhui ya ujanja yamekuwepo tangu jadi.

Ndiposa, Frye (1957) akitumia mtazamo wa kidini, anamsawiri Mungu kama mjanja kwani aliingia kwenye mkataba na Shetani. Mkataba huu ndio ulisababisha mateso aliyopitia Ayubu. Isitoshe, ujanja huweza kujitokeza katika kisasili cha Wakristo kuhusu asili ya dhambi. Kisasili hicho kinaeleza kuwa dhambi ilitokana na ujanja wa Shetani kwani alimdanganya binadamu kuwa akila tunda la katikati

mwa bustani ya Edeni atakuwa na hekima. Binadamu basi alikula tunda hilo ili awe sawia na Mungu. Kwa kula tunda hilo binadamu aliweza kuanguka.

Kitabu cha *Myths and Legends of the Swahili* kina ngano ya “Abunuwasi Apata Punda”. Mhusika mkuu ambaye anaitwa Abunuwasi anaendeleza maudhui ya ujanja. Mwandishi anaeleza kuwa Abunuwasi alipendwa na Haruni. Kwa sababu ya kupendwa kwake, bawabu anamuonea wivu. Bawabu anamlazimisha Abunuwasi kuandika kandarasi kuwa atamgawia bawabu chochote atakachopewa na Haruni. Inambidi akubali masharti ya bawabu ndipo akubaliwe kuingia. Kandarasi hii ndiyo mbinu yake ya kujiokoa dhidi ya bawabu. Hali anayojikuta Abunuwasi inaoana na maoni ya Propp (1978) kuwa wahusika wajanja hujikuta katika matatizo. Aidha, anaeleza kuwa matatizo haya humlazimisha kutumia hekima ili kujinasua.

Baadaye, Abunuwasi anaingia kwake Haruni na kumshurutisha ampige viboko mia moja. Baada ya kucharazwa viboko takribani kumi, Abunuwasi anaomba nafasi ya kupumzika. Abunuwasi anachukua fursa hiyo kumuonyesha karatasi aliyoandika masuala waliyokubaliana na bawabu. Haruni anakasirika na kumuadhibu bawabu viboko hamsini. Kwa upande mwingine, Abunuwasi anapewa pesa ya kununua punda. Katika ngano hii, inabainika kuwa Abunuwasi alitumia ujanja kwa maslahi yake binafsi kwani hakutaka kumgawia bawabu pesa.

Mfano mwingine katika kitabu hicho cha *Myths and Legends of the Swahili* imo kwenye ngano ya “Abunuwasi na Wezi Wawili”. Mwandishi anaanza ngano hii

kwa kutueleza kuhusu Abunuwasi kunyang'anywa kondoo na wezi wawili. Wezi hao wanamnyang'anya kondoo kwa sababu walikuwa na nguvu nyingi kumshinda. Baadaye, Abunuwasi anaamua kutumia akili ili kulipiza kisasi. Mara ya kwanza, anawahadaa wezi hao kuwa ana mti unaozaa dhahabu na wanamuamini na kumpa ng'ombe mia moja. Mara ya pili, anawaambia kuwa ana kijiti chenye uwezo wa kufufua mtu na wanaamini na kumpa pesa. Inashangaza jinsi wezi hao walivyomuamini Abunuwasi katika visa hivyo viwili. Hawakuwazia kiundani maneno ya Abunuwasi. Hali hii inaweza kuonyesha kuwa maoni ya Makgamatha (1993) kuwa wahusika wajinga wanastahili kuhadaiwa yana mashiko. Hii ni kwa sababu wanaamini maneno ya mhusika mjanja bila kuwazia maneno hayo kiundani.

Mwishowe, kutokana na kudanganywa huku wezi hawa wawili wanajuta. Kwani mmoja wao anashikwa na kuhukumiwa kunyongwa kwa sababu ya kumuangamiza mwenzake. Kujuta kwao kunaonyesha kuwa Abunuwasi amefaulu kutumia akili badala ya nguvu kulipiza kisasi. Ushindi wa Abunuwasi unaonyesha kuwa kauli ya Canonici (1995) kuwa katika hekaya mwandishi au msimulizi anaonyesha kuwa akili ni bora kuliko nguvu za mwili ina mashiko. Aidha, Propp (1984) anashadidia maoni haya kwa kueleza kuwa ujanja na ulaghai ndizo silaha za wanyonge dhidi ya wenye nguvu.

Isitoshe, ngano ya "Liyongo" iliyomo kwenye kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* ina mhusika Liyongo. Mhusika huyu anakamatwa na kufungwa gerezani. Baadaye anagundua kuwa kwa kutumia akili anaweza kujiokoa

badala ya nguvu alizo nazo. Anaamua kumtuma kijakazi kwa mamake kwa kutumia shairi. Mamake Liyongo aliweza kumsaidia Liyongo kutoroka gerezani. Aidha, mamake Liyongo anaonyesha upendo kwake kwa kumtuma kijakazi gerezani amletee mkate. Mwandishi anaeleza hivi:

Akamwambia kijakazi chake (na yeye ndani na kijakazi nje ya mlango).
Ewe kijakazi nakutuma uwatumika
Kamwambie mama, ni mwinga siyalimka
Afanye mkate, pale kati tupa kaweka
Nikeze pingu na minyoo ikinyoka
Niingie ondoni ninyiririke ja mana nyoka
Tatange madari na makuta kuno kimeta (Uk. 443).

Mfano huu unaonyesha jinsi Liyongo alivyomtuma kijakazi amwekee tupa ndani ya mkate. Anatunga shairi ili askari wale wasielewe anachosema. Baadaye, kijakazi anakuja na mkate mzuri na mkate wa wishwa. Badala ya askari kuwazia mbona mkate wa wishwa umeletwa wanakula mkate mzuri na kuwacha ule wa wishwa. Matokeo ya ujinga wao ni Liyongo kukereza minyororo na kutoroka mwituni.

Hata hivyo, inabainika wazi kuwa Liyongo alitoroka gerezani kwa usaidizi wa mamake. Aidha, mamake alikuwa anamtuma kijakazi kumletea chakula kila siku. Hali hii inaoana na maoni ya Jung (1968) kuwa mama hutumika kama kikale katika ngano. Mama huweza kutumiwa na mwandishi ili kuisitiza maudhui ya uPendo, hekima na amani. Baada ya Liyongo kutoroka gerezani anaelekea kijijini na kuendelea kuwanyanyasa watu.

Ngano za “Abunuwasi Apati Punda”, “Abunuwasi na Wezi Wawili” na “Liyongo” zina maudhui ya ujanja. Ngano hizi zina wahusika wajanja. Hata hivyo, ujanja

unaojitokeza katika hadithi hizi ni wa kunufaisha wahusika wenyewe na sio jamii. Aidha, ujanja wao unaendeleza uovu. Liyongo anatumia ujanja ili kutoroka gerezani na kuwanyanyasa wanakijiji ilhali ujanja wa Abunuwasi unasababisha kifo cha Mwizi mmoja. Konrad (1983) anaeleza kuwa katika fasihi simulizi wahusika wajanja huweza kuchukuliwa kama vikale. Kutokana na maelezo haya, inabainika kuwa ngano hutumia wahusika wajanja kama vikale.

Hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zina maudhui ya ujanja. Mfano ni hadithi ya “Uganga wa Pete” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Hadithi hii ina mhusika Maskini ambaye anatumia ujanja ili kusuluhisha matatizo yanayowakumba wanajamii. Anatumia ujanja kupata pete ya mfalme, mali ya mfalme iliyoibwa na Simba mla watu. Kutokana na ujanja wake, anatumia kwa kupewa wadhifa na mfalme. Ujanja wake unafanya wengi kuamini kuwa yeye ni mganga. Hadithi hii ya “Uganga wa Pete” inasawiri maudhui ya ujanja kama ngano tulizojadili. Kujirudia huku kwa maudhui ya ujanja kunaonyesha kuwa maudhui yanayotawala kazi huweza kujirudia kutoka kazi moja hadi nyingine. Frye (1957) anaeleza kuwa fasihi ni kama ibada, jinsi ibada hurudiwa kila wakati basi fasihi pia hurudia mawazo yaliyojadiliwa awali. Mawazo haya yanabaini kuwa inawezekana mwandishi wa hadithi ya “Uganga wa Pete” alikuwa na uelewa wa maudhui yanayojitokeza katika ngano za awali kama vile ujanja.

Hata hivyo, ujanja wa Maskini ni wa kunufaisha jamii nzima. Aidha, tofauti na ngano tulizojadili Maskini haonyeshi kuwa mhusika mjanja kamili. Hii ni kwa

sababu kwa kila jambo anauliza mke wake ushauri. Isitoshe, inasadifu kuwa mke wake kila wakati yuko katika maeneo ambayo mikasa mbalimbali hutukia. Hali kadhalika, imebainika kuwa ujanja wa Maskini unatumika kuendeleza wema na sio uovu. Hii ni kwa sababu anasaidia mfalme kupata pete yake, mali yake na kushika Simba mla watu. Kwa msingi huu, usawiri wa ujanja wa hadithi hii ni tofauti na ngano tulizojadili.

Hadithi Nyingine ni ile ya “Waliohujumu Ujamaa” iliyomo kwenye diwani ya *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*. Katika hadithi hii, mhusika aitwaye Fisi anatumia ujanja. Anajenga kasri kubwa na kuwaambia wanyama waje kustarehe. Baadaye anajifanya kuwa amekufa ili wanyama wahudhuri matanga yake. Wanyama wote wanahudhuria kwa minajili ya kuomboleza. Hata hivyo, Sungura anagundua hila yake na kutoroka. Hatimaye, wanyama wote wanapowasili Fisi anaamka, anafunga mlango na kuwaua wote. Mwandishi anaeleza hivi:

Kule nyuma, baada ya kumsikia Sungura na wasifu wake wa maonyo, Fisi alijua ingechukua muda lakini mwishowe waombolezaji wengine wangeng’amua mazingaombwe ambayo yangefuata. Ghafla bin vuu Fisi alizinduka na kabla waombolezaji wale kupepesa aliruka na kushindilia mlango na kuufunga ndi ndi ndi kwa upande wa ndani. Filihali, upanga na shoka zikapata kazi (Uk. 118).

Dondoo hili linalopatikana katika hadithi hii linabainisha jinsi Fisi alivyowaua wanyama wenzake. Kutokana na dondoo hili, inabainika kuwa Fisi alitumia ujanja wake ili kujinufaisha. Aidha, anatumia ujanja kuendeleza maudhui ya uovu kwani anawaua wanyama wote. Hali hii ni sawia na ngano tulizojadili za “Abunuwasi na

Wezi Wawili” na “Liyongo”. Kutokana na hadithi hii, mtafiti ana msimamo kuwa mwandishi wa hadithi ya “Waliohujumu Ujamaa” alikuwa na uelewa wa ngano za hapo awali.

Hali kadhalika, kuna hadithi ya “Njia ya Mwongo” iliyomo kwenye diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Katika hadithi hii, jirani anawapata Korir na Kipchumba wakiogelea badala ya kuchunga mbuzi. Mbuzi hao basi wanakula mimea yake. Badala ya jirani kuwaadhibu moja kwa moja anaamua kutumia ujanja kwa kuchukua nguo za Korir na Kipchumba. Korir na Kipchumba basi inawabidi wavalie nguo zingine wakielekea nyumbani. Hata hivyo, keshoye chifu anajuzwa yaliyotukia siku hiyo. Nguo zinapotolewa hadharani inabainika kuwa ni za Kipchumba na Korir. Hatimaye, vijana hao wawili wanaadhibiwa. Adhabu hii inawabadilisha kwani wanatambua kuwa mchezo hauchukui mahali pa kazi. Ujanja wa jirani huyo basi umesaidia kutenda wema kwani Korir na Kipchumba wanabadilika kitabia.

3.2.3. Maudhui ya Ushujaa

Ushujaa ni hali ya kufanya jambo kwa ujasiri bila kuogopa matokeo yake. Ushujaa huweza kutambulishwa na namna mhusika anavyotumia akili yake, nguvu zake za mwili, nguvu za kivita na uganga kutekeleza jukumu fulani. Frye (1957) anaeleza kuwa shujaa huweza kuwa na uwezo unaotoshana na binadamu wa kawaida. Aidha, anaongezea kwa kusema kuwa shujaa huweza kupewa sifa zinazopita mipaka ya binadamu. Mfano ni Samsoni wa Uyahudi aliyekuwa na uwezo wa kuua jeshi la

Wafilisti kwa kutumia mfupa. Hali kadhalika, Frye (1957) anaongezea kwa kutuelezea kuwa shujaa hupitia hatua nne. Nazo ni: kuzaliwa kwa shujaa, safari ya shujaa kuelekea mauti au kuporomoka, kutoweka kwa mhusika nguli na kuzaliwa upya kwa shujaa.

Ngano ya “Liyongo” iliyomo kwenye kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* ina maudhui ya ushujaa. Ushujaa huu unajitokeza kwa namna mbalimbali. Kwanza kabisa, mwandishi anaeleza kuwa Liyongo alikuwa na nguvu nyingi. Nguvu zake Liyongo ziliwafanya wanakijiji wa Pate kuogopa kukabiliana naye moja kwa moja. Aidha, alikuwa na nguvu za kivita. Mwandishi anaeleza hivi:

Wakatupa vitu vyao na kwenda mbio wasidiriki,
akawakamata akawapiga vita akawaua (Uk. 446).

Mfano huu unaonyesha jinsi Liyongo alivyoogopewa kiasi kuwa askari wote walitoroka badala ya kumkabili. Isitoshe, Liyongo anaonyesha ushujaa kwa kutonywea mbele ya maadui. Ndiposa, Mberia (1989) anaeleza kuwa shujaa huwa jasiri ambaye hatishwi na mtu yeyote. Aidha, Njogu na Chimerah (1999) wanaongezea maoni haya kwa kueleza kuwa shujaa huwa na nguvu nyingi zinazoshinda binadamu wa kawaida.

Ushujaa wa Liyongo unajitokeza pia katika vipawa vyake. Liyongo alikuwa mtungaji mzuri wa mashairi na nyimbo. Mwandishi anaeleza kuwa wengi walikuja kusikiliza nyimbo zake. Isitoshe, alitunga shairi. Alitunga shairi hili kwa minajili ya kupata njia ya kutoroka gerezani. Hali hii ya shujaa kuwa na vipawa inaonyesha

kuwa maoni ya Wa Mutiso (1999) kuwa jagina huwa ni washairi, wanafalsafa na wenye elimu ya juu yana mashiko.

Hatimaye, ushujaa wa Liyongo unabainishwa na akili yake iliyo pevu mno. Mwandishi anaeleza kuwa Liyongo alitunga shairi. Katika shairi hili, anamtuma kijakazi ili amuambie mamake amwekee tupa ndani ya mkate wa wishwa. Anafanya hivi kwa sababu alijua kuwa askari waliomchunga hawapendi mkate wa wishwa. Kwa kufanya hivi, anapata nafasi ya kukereza minyororo na kutoweka msituni. Kutoroka huku inaoana na kauli ya Propp (1984) kuwa aghalabu shujaa hutoka katika mazingira yake na kuelekea katika mazingira tofauti. Kisa kingine kinachothibitisha kuwa Liyongo alikuwa na akili pevu kinatokea wakati anagundua hila waliyotaka kutumia wanakijiji ili kumuangamiza.

Mwandishi anaeleza kuwa wanakijiji walipanga kumfuma mishale anapopanda mti ili kuchuma mikoma. Hata hivyo, Liyongo anatambua na kuamua kuchuma mikoma kwa kutumia mishale badala ya kupanda. Isitoshe, Liyongo anapoulizwa na mtotowe siri ya nguvu zake anatambua mara moja kuwa anataka kumuua. Hata hivyo, hatuelewi ni kwa nini anamuambia siri yake na hatimaye kufa kirahisi. Anauliwa kwa kudungwa na sindano ya shaba kwenye kitovu chake. Kulingana na Mulokozi (1999), Liyongo alikuwa na nguvu za uganga kwani anauliwa tu na sindano ya shaba kudungwa kitovuni mwake. Hali ya kuanguka au kufa kwa shujaa ni dhana ya kawaida. Ndiposa, Frye (1957) na Mbogo (2011) wanaungama kuwa

shujaa lazima afe au aanguke. Aidha, Jung (1968) anaongezea kwa kueleza kuwa kuanguka au kufa kwa shujaa hutokana na kiburi chake.

Hata hivyo, ushujaa wa Liyongo katika kitabu cha Steere unatumika ili kujinufaisha. Steere anamsawiri Liyongo kama mhusika katili anayewadhulumu wananchi. Kwa mfano anaeleza kuwa Liyongo alikuwa anawakataza wajamii kuchota maji kisimani. Hali hii ni kinyume na jinsi ujasiri wa Liyongo unavyosawiriwa katika utendi wa Liyongo uliomo katika kitabu cha *Tenzi za Kale* (1999) na kitabu cha *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (2001). Vitabu hivi vinathibitisha kuwa Liyongo alitumia ushujaa wake ili kuwatetea wanajamii. Katika utendi wa Liyongo uliomo katika *Tenzi za Kale* (1999) mwandishi anaonyesha kuwa Liyongo alipendwa na wanajamii kiasi kuwa Wagalla walihitaji mbegu yake. Aidha, katika kitabu cha *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (2001) Liyongo anamwokoja kijana aliyeshambuliwa na mamba.

Isitoshe, kitabu cha *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (2001) cha Matundura kimenakili matendo mengine ya kishujaa ya Liyongo ambayo hayamo katika kitabu cha Steere. Mwandishi anaeleza kuwa Liyongo alionyesha ushujaa wake kwa kuua mamba aliyemshambulia kijana mmoja. Aidha, Liyongo anachukua siku mbili kutembea kutoka Shanga hadi Pate. Jambo hili lingemchukua binadamu wa kawaida siku nne. Isitoshe, anapuliza panda mbili hadi zinapasuka. Hali kadhalika, sauti ya mkoromo wa Liyongo ilisikika kama ngurumo. Hatimaye, mwandishi anaeleza kuwa Liyongo alilala msituni kwa sababu alikuwa ana uwezo wa kuua mnyama yeyote.

Kifo cha Liyongo katika kitabu cha Steere kinatokana na usaliti. Liyongo anasalitiwa na mwana wake ambaye anamuua hatimaye. Hata hivyo, haiaminiki ni kwa nini Liyongo anamuambia mwanawe siri ya nguvu yake licha ya kuwa alikuwa amejua kuwa mwanawe anataka kumuangamiza. Hali hii inaonyesha udhaifu wa Liyongo. Ndiposa Frye (1957) anaeleza kuwa shujaa hufa kwa sababu ya udhaifu wake.

Katika kitabu cha *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (2001) mwandishi anasawiri kifo cha Liyongo kwa namna tofauti. Anaeleza kuwa Liyongo alikufa akiwa amepiga goti na kuushika mshale uta wake na mshale tayari kufuma. Hali hii ni ya kustaajibisha.

Ngano nyingine ni ile ya “Uzinduzi wa Tiara” iliyomo kwenye kitabu cha *Myths and Legends of the Swahili*. Mhusika Abunuwasi anadhihirisha uwezo wake wa kishujaa kwani yuko na akili pevu. Katika ngano hiyo, tajiri anajaribu kuleta ugomvi kati ya Abunuwasi na khalifa. Tajiri anaenda kwa khalifa na kumuambia kuwa Abunuwasi alimuambia kuwa anaweza kujenga nyumba mawinguni. Mwandishi anaeleza hivi:

Akitarajia kuibua ugomvi baina ya Abunuwasi na khalifa,
Tajiri akasema ‘Abunuwasi ameniambia kuwa ana uwezo wa
kujenga nyumba mawinguni’ (Uk. 119).

Maneno haya yanamfanya khalifa kumwita Abunuwasi na kumuambia ajenge nyumba mawinguni. Anamuambia kuwa asipofanya hivyo atafukuzwa. Abunuwasi hakujibu chochote. Hata hivyo, Abunuwasi alijenga tiara iliyo na umbo unaofanana na nyumba. Aidha, alipaka rangi tiara hiyo. Baadaye, alitupa tiara angani ili ipae.

Hatimaye, alimuita khalifa na kumuambia kuwa aangalie nyumba iliyo angani. khalifa anaamini kuwa tiara hiyo ni nyumba.

Hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zina maudhui ya ushujaa. Mfano wa hadithi ni “Uganga wa Pete” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Mhusika mkuu wa hadithi hii anaitwa Maskini. Maskini anatumia hekima ili kutatua matatizo ya wanakijiji. Aliweza kupata pete ya mfalme, mali ya mfalme iliyoibwa na wezi na kushika Simba mla watu. Uwezo wa Maskini unawafanya wanakijiji kumuona kama mganga. Wanamuona kama shujaa wao kiasi kuwa wanampa wadhifa. Aidha, Maskini anaonyesha uwezo unaopita mipaka ya binadamu wakati anapobebwa na Simba mla watu. Mwandishi anaeleza hivi:

Ilikuwa kama saa sita hivi askari alipopeleka ripoti kumhusu mganga; na saa moja baadaye, simba akafika nyumbani kwa mfalme mganga akiwa mgongoni. Japo wote walikuwa wamechoka hoi, simba alikuwa zaidi. Aliweza kuangushwa kirahisi na askari wapatao sita na kwa matumizi ya mifumo mganga akaokolewa (Uk. 108).

Mfano huu unaonyesha uwezo mkubwa aliopewa Maskini. Inashangaza jinsi mtu anaweza kubebwa na simba bila kushambuliwa. Uwezo huu unamfanya aweze kulinganishwa na Liyongo. Uwezo huu wa usikawaida unaweza kuwa umetokana na kazi za fasihi za awali. Ndiposa, Frye (1957) anaeleza kuwa shujaa wa tanzia huwa na uwezo unaoning’inia kati ya Miungu na binadamu wa kawaida. Aidha, Larsen (2018) anaongezea mawazo haya kwa kueleza kuwa Yesu alikuwa ni shujaa kwani alitenda miujiza mingi iliyowashangaza wengi. Yesu alifanya miujiza kama vile: kusimamisha upepo, kuponya magonjwa na hata kufufua wafu. Hali hii

inaonyesha kuwa uwezo wa Yesu uliwashinda binadamu wa kawaida. Hata hivyo, uwezo wa Maskini ni wa kubahatisha tu kwani hangeweza kushambulia Simba. Maskini anaokolewa na wanajamii.

Maskini anaonyesha pia ana nguvu za kiakili kama alivyo Abunuwasi. Hali hii yaweza kuonyesha kuwa maoni ya Nyamsenda (2015) kuwa shujaa huwa na nguvu za kimwili, akili, kivita na uganga yana mashiko. Hata hivyo, Maskini haanguki bali anatuzwa. Hali hii ni tofauti na maoni ya Frye (1957) na Mbogo (2011) kuwa shujaa lazima aanguke au afe. Hata hivyo, hali hii inaoana na maoni ya Campbell (2004) kuwa shujaa hukumbwa na matatizo mengi akiwa safarini na hatimaye hurejea nyumbani na kusherehekewa. Hii ni kwa sababu ameshinda majaribio yote aliyopitia. Aidha, nguvu za kiakili za Maskini haziwezi kulinganishwa na mhusika kama Abunuwasi. Abunuwasi ni mhusika anayejitosheleza kamili na hahitaji kusaidiwa kwa lolote. Kwa upande mwingine, Maskini kila wakati anapokabiliwa na jambo gumu anauliza ushauri kutoka kwa mke wake kuhusu jinsi ya kutatua tatizo hilo. Hali hii inaonyesha kuwa uwezo alionao Maskini ni ya binadamu wa kawaida. Ndiposa, Frye (1957) anaeleza kuwa shujaa huweza pia kuwa na uwezo unaotoshana na binadamu wa kawaida. Hata hivyo, usawa baina ya wahusika Maskini na Abunuwasi ni kuwa wanawashinda maadui wao wote.

3.2.4 Maudhui ya Mauti (Kifo)

Wafula na Njogu (2007) wanaeleza aina ya vikale vya kimaudhui katika fasihi ikiwemo: wema na uovu, mauti, uwezo wa kufasiri ndoto, uwezo wa kufufuka na

kuwaasa wanaoishi. Kutokana na maelezo yao, inabainika kuwa mauti ni kikale. Hata hivyo, Frye (1976) anaelezea kifo kwa muktadha tofauti. Kulingana naye, kifo sio lazima kiwe cha kikweli. Kifo kwake kinaweza kutokea wakati mhusika anapitia mateso hasa akiwa gerezani. Mateso haya humfanya mhusika huyu aonekane ni kana kwamba ‘amekufa’. Kufa kwake ni hali ya kukosa tumaini la kuishi.

Isitoshe, anaongezea kuwa mhusika huyu anaweza kufufuka tena na kurudia hali yake ya kuwa shujaa kwa kujitoa katika hali hii. Matatizo anayoyapitia mhusika huweza kusawiri dhana ya kifo. Anatumia mfano wa hadithi ya “Bluebeard” ambapo wahusika hutupwa kwenye shimo kubwa lenye giza totoro na hatimaye hufaulu kutoroka. Frye (1976) akiongezea mawazo haya anaeleza dhana ya kifo na kufufuka hivi:

Katika fasihi kuna hatua zinazofuatwa ikiwemo mhusika kushuka chini hadi kuzimu na kurejea tena (Uk. 97).

Mfano huu unaonyesha jinsi dhana ya kifo huangaliwa kifasihi. Hali kadhalika, Frye anatoa mfano wa hadithi ya Jonah na Yesu katika Bibilia. Yesu aliweza kuelekea jehanamu kama ishara ya kufa na kurejea. Kwa upande mwingine, Jonah anamezwa na samaki. Jonah akiwa tumboni mwa samaki anazungukwa na kiza nene. Hata hivyo, Jonah anapotemwa na samaki anajikuta katika mazingira mapya yanayoashiria kufufuka kwake.

Katika ngano ya “Liyongo” iliyomo kwenye kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* kuna maudhui ya kifo. Mwandishi anataeleza kuhusu jinsi Liyongo alivyoshikwa na kufungwa. Mwandishi anaeleza hivi:

Wakamfunga kwa minyororo na kuweka mti katikati mwa miguu yake (Uk. 442).

Mfano huu unaonyesha jinsi Liyongo alivyofungwa kwa minyororo na mti. Hakuwa na uwezo wa kutumia nguvu zake ili kukata minyororo. Kwa msingi huu ni kana kwamba Liyongo ‘amekufa’. Hata hivyo, anatumia hekima ili kujiokoa. Kujiokoa huko kunaashiria kuzaliwa upya kwa Liyongo. Ndiposa, Campbell (2004) anaangalia dhana ya kufa na kufufuka kwa shujaa akizingatia msingi wa tohara. Anaeleza kuwa katika tohara mambo ya kale ya mhusika hufa au husaulika na mhusika huyu anazaliwa upya ili akabili majukumu ya baadaye. Liyongo basi anamtuma kijakazi kwa mamake ili aletewe tupa ikiwa ndani ya mkate wa wishwa. Anatumia tupa hii kukereza minyororo na kuhepa kuelekea msituni. Kuhepa kwake katika mazingira mapya kunaweza kuchukuliwa kama ‘kufufuka’.

Hali hii ya kufa na kufufuka imejadiliwa na Frye. Frye (1957) anaeleza shujaa hupitia ruwaza mbalimbali ikiwemo kuzaliwa, safari yake kuelekea kifo, kifo au anguko la shujaa na kufufuka kwa shujaa. Licha ya kujifufua katika hali hii, Liyongo anakufa hatimaye. Anamfichulia mtoto wake siri ya nguvu zake. Mtoto wake anamuua hatimaye. Mwandishi anaeleza hivi:

Akaenda hata alipofika akamshika mwanawe kumtumbuiza kwa nyimbo, akaanguka. Mamaye akalia, akajua mwanawe amekufa (Uk. 452).

Dondoo hili linalopatikana katika “Ngano ya Liyongo” linaonyesha jinsi mamake Liyongo alivyojaribu kumtumbuiza kwa nyimbo. Baadaye, anagundua kuwa Liyongo ameaga. Hata hivyo, Larsen (2018) anapoelezea Yesu kwa mtazamo wa kidini anaeleza kuwa Yesu alikufa baada ya kufanya miujiza mingi iliyowashangaza wengi. Kinyume na Liyongo, Yesu anapokufa anafufuka hatimaye na inaaminika kuwa anaishi milele.

Ngano nyingine ni ile ya “Abunuwasi na Wezi Wawili” iliyomo kwenye kitabu cha *Myths and Legends of the Swahili*. Katika ngano hii, mwizi mmoja anakufa kutokana na kudungwa kisu na mwizi mwenzake. Anamdunga kisu kutokana na ugomvi waliokuwa nao kuhusu kugawanya mali waliyopata kutoka kwa Abunuwasi. Kutokana na matendo yake anahukumiwa kunyongwa.

Ngano hizi mbili yaani ngano ya “Liyongo” na “Abunuwasi na Wezi Wawili” zinasawiri kifo kwa namna sawa. Kifo cha wahusika kinatokana na udhaifu wao. Katika ngano ya “Liyongo” kifo cha Liyongo kinatokana na kumfichulia mtoto wake siri ya nguvu zake. Isitoshe, ngano ya “Abunuwasi na Wezi Wawili” ina mwizi mmoja anayemuua mwenzake ili aweze kupata mali zaidi. Mwizi huyu hatimaye anahukumiwa kunyongwa. Hali hii inaweza kuoana na maelezo ya Frye (1957) kuwa mhusika hufa kutokana na udhaifu wake wa kitabia kwa mfano

uchoyo. Mose (2005) anashadidia maoni haya kwa kueleza kuwa kifo hutokana na makosa, uhalifu au dhambi inayosababishwa na mhusika wa tanzia.

Hadithi fupi za kisasa za Kiswahili pia zinaonyesha maudhui ya kifo. Hadithi ya “Safari ya Maangamizi” iliyomo kwenye diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* ina mhusika Pendo. Mhusika huyu anakufa kutokana na ugonjwa wa ukimwi. Hata hivyo, Pendo anaambukizwa ugonjwa huu na vijana waliomnajisi. Hali hii inaonyesha kifo cha Pendo hakikutokana na udhaifu wake wa kitabia. Kifo chake kinakinzana na mawazo ya Frye (1957) kuwa kifo cha mhusika kinafaa kitokane na udhaifu wa kitabia wa mhusika kwa mfano kukiuka maadili ya kijamii. Inabainika waziwazi kuwa Pendo kabla anajisiwe alikuwa ni bikra. Ubikira wake ni ithibati tosha kuwa alikuwa na maadili mema.

Isitoshe, kuna hadithi ya “Waliohujumu Ujamaa” iliyomo kwenye diwani ya *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*. Hadithi hii inaonyesha kuwa kifo kinatokana na ujinga wa wahusika. Wanyama kama vile Sungura na Kobe waliogundua hila ya Fisi waliweza kuepuka kuuliwa. Hata hivyo, wanyama waliobakia waliuliwa. Wanyama hawa hawakuweza kujiuliza ni kwa nini Fisi alilala huku shoka na upanga ukiwa ubavuni mwake. Isitoshe, hawakuwazia ni kwa nini Fisi alitokwa na mate badala ya upovu. Mwandishi anaeleza hivi:

Nyumba ya Fisi iligeuka kichinjio. Sakafuni pakawa na lundo la nyama. Damu ikafanya gharika iliyoenea hadi nje. Ikafanyisha unyevuunyevu hata kwenye nyasi na kwenye mashina ya mimea. Mle ndani Fisi akaanza karamu yake. Akala nyama, aliposhiba akalalia nyama. Aliteuka si haba na vundo la teuko likachanganyikiwa na harufu ya nyama katika nyumba ile

na mazingira yale yakanuka. Nyumba iliyojengwa na kusherehekewa kama ishara ya mapenzi kati ya viumbe wenye nasaba ikawa jaa la uozo na fondogoo (Uk. 119).

Mfano huu uliomo kwenye hadithi ya “Waliohujumu Ujamaa” unaonyesha jinsi Fisi alivyosherekea kwa kuwaua wenzake. Vifo vya wanyama hao vilitokana na ujinga wao. Waliamini tu Fisi ameaga bila kuchunguza kiundani. Hali ya mhusika kufa kutokana na udhaifu wake inajitokeza pia katika ngano tulizojadili za “Abunuwasi na Wezi Wawili” na “Liyongo”. Ndiposa, Mose (2005) anaeleza kuwa kifo hutokana na makosa yanayosababishwa na mhusika wa kazi ya fasihi.

Mwishowe, kuna hadithi ya “Njozi ya Mtu Mweupe” iliyomo kwenye diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Katika hadithi hii, msimulizi anampoteza mama yake. Kifo cha mama yake kinatokana na ugomvi. Babake anamuua mamake kwa kumpiga risasi. Inabainika kuwa anamuua kwa sababu ya kuporomosha biashara aliyomuachia. Baadaye, kunatokea kifo cha baba yake. Kifo cha baba yake kinatokana na ugonjwa kwani afya ya baba yake ilizorota. Mwandishi wa hadithi hii anatuonyesha kuwa sio lazima kifo kitokane na makosa ya mtu. Kifo kinaweza kutokana na hali zisizoepukika kama vile magonjwa.

Hali kadhalika, maudhui ya kifo yamejitokeza katika kazi ya fasihi kutoka kale. Ndiposa, maudhui ya kifo yanajirudia katika hadithi za Edgar Allan Poe. Mwandishi huyu alitumia mbinu ya uhalisiaajabu kuelezea kuhusu kifo. Baadhi ya hadithi zake zinazosheheni maudhui ya kifo ni kama vile: *The Tell-Tale Heart* (1843), *Premature Burial* (1844) na *Mask of Red Death* (1842).

3.3. Hitimisho

Sura hii imeangazia maudhui yanayoshughulikiwa katika ngano na hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Maudhui kama vile: ujanja, wema, uovu na kifo yamejadiliwa. Utafiti umebaini kuwa maudhui yanayojitokeza katika ngano ni sawia na yale yanajitokeza katika hadithi fupi. Hata hivyo, maudhui yaliyomo katika ngano yanasawiriwa kwa njia tofauti ikilinganishwa na maudhui yaliyomo katika hadithi fupi. Usawiri huu unaonyesha kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili sio zao la mchakato wa kistari wa kutoka kwa ngano hadi kwa hadithi fupi. Aidha, usawa katika maudhui unaweza kuwa umetokana na masuala yaliyowaathiri wanajamii. Masuala haya yalikuwa sawia kutoka jamii moja hadi nyingine. Ndiposa, kazi zote za fasihi zina maudhui kama vile: uovu, wema na ujanja. Hata hivyo, tanzu kama vile ngano na hadithi fupi zilichipuka nyakati tofauti. Hali hii inathibitishwa na jinsi waandishi au wasimulizi wa tanzu hizi walivyosawiri maudhui haya kwa namna tofauti.

Utafiti huu umebaini kuwa ngano husawiri ujanja kama chanzo cha ubinafsi katika jamii. Aidha, ujanja huu hutumiwa kuendeleza uovu. Hali kadhalika, katika ngano wema hutuzwa huku uovu ukiadhibiwa. Ushujaa katika ngano pia hutambulishwa na sifa zinazopita mipaka ya binadamu (usikawaida). Mwishowe, ngano husawiri kifo kama mkasa unaotokana na makosa ya mtu binafsi.

Hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zinasawiri maudhui yake kwa namna tofauti. Hadithi hizi zinaonyesha kuwa ujanja hutumika kuendeleza sio tu uovu bali pia

wema katika jamii. Aidha, ujanja huu hutumiwa kwa manufaa ya jamii nzima. Mathalan, kifo katika hadithi hizi kinaweza kusababishwa na hali zisizoepukika kwa mfano magonjwa. Mwishowe, ushujaa katika hadithi fupi hutambulishwa na sifa zinazoweza kuaminika. Hali hii ni tofauti na ngano. Katika ngano ushujaa hutambulishwa na sifa zinazozidi mipaka ya binadamu (usikawaida) (Njogu na Chimerah, 1999).

Hata hivyo, kuna hadithi zingine zilizoonyesha sifa za kimaudhui zinazofanana na ngano. Mfano ni hadithi ya “Waliohujumu Ujamaa” iliyomo kwenye diwani ya *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*. Hadithi hii inaonyesha kuwa ujanja hutumika kuendeleza uovu na kifo husababishwa na makosa ya mtu binafsi. Hali hii ni sawia na ngano zilizomo kwenye vitabu vya *Myths and Legends of the Swahili* na *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*. Usawa huu unaonyesha kuwa waandishi hawa walikulia katika mazingira ya fasihi simulizi. Hivyo iliwabidi kwa hiari yao kuchota vipengele vya fasihi simulizi hasa ngano na kuvitumia katika uandishi wa hadithi fupi.

SURA YA NNE

WAHUSIKA WA NGANO NA HADITHI FUPI YA KISASA YA KISWAHILI

4.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeangazia maudhui katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili na ngano. Katika sura hii, tumeangazia wahusika mbalimbali wanaopatikana katika ngano na hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Mtafiti amefanya hivi ili kubaini ikiwa wahusika wanaopatikana katika ngano wanapewa sifa sawia na wale wanaopatikana katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.

4.1 Wahusika wa Ngano na Hadithi Fupi

Wahusika walioangaziwa katika ngano na hadithi fupi ni kama vile: wahusika wajanja, mashujaa, majahili, wema na katili. Wahusika hawa wametumiwa kuendeleza maudhui ya ushujaa, ujanja, wema na uovu katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili na ngano.

4.1.1 Wahusika Wajanja

Mhusika mjanja ni mhusika ambaye hutumia hila kuwahadaa wenzake. Mara nyingi mhusika mjanja hufanya hivi ili kujinufaisha. Wahusika wajanja wamekuwepo katika kazi za kifasihi tangu jadi. Ndiposa, Jacobi (2000) anaeleza hivi:

Kikale cha wahusika wajanja kimekuwepo tangu jadi. Swali ni je tunakubali uwepo wa wahusika wajanja au la (Uk. 62).

Maelezo haya ya Jacobi (2000) yanaonyesha kuwa wahusika wajanja ni vikale katika fasihi. Aidha, Wilkinson (2017) anamuunga mkono Jacobi (2000) kwa kueleza kuwa wahusika wajanja hupatikana katika kazi za kifasihi za jamii mbalimbali. Kazi hizi hujumuisha tanzu kama vile ngano na hadithi fupi.

Ngano ya “Abunuwasi Ajenga Nyumba” iliyomo kwenye kitabu cha *Myths and Legends of the Swahili* ina mhusika mjanja aitwaye Abunuwasi. Abunuwasi anajenga nyumba iliyo na ghorofa. Baadaye anamuuzia mfanyabiashara sakafu ya chini ya nyumba hiyo. Baada ya muda, Abunuwasi anamuuliza mfanyabiashara ikiwa anaweza kununua ghorofa ya kwanza ya nyumba hiyo. Abunuwasi anafanya hivi kwa sababu alikuwa anataka kuhama. Hata hivyo, mfanyabiashara anakataa kununua ghorofa ya kwanza ya nyumba hiyo. Abunuwasi basi anatumia hekima na kuwaita wenzake ili wabomoe nyumba hiyo. Anamjua mfanyabiashara kuwa anahitaji kubomoa ghorofa ya kwanza. Inambidi mfanyabiashara anunue sehemu ya chini ya nyumba hiyo. Anafanya hivi kwa sababu ikiwa sehemu ya juu ikibomolewa basi sehemu ya chini ya nyumba ingeporomoka.

Ujanja huu wa Abunuwasi unamsaidia kwani anamlazimisha mfanyabiashara kununua ghorofa ya kwanza ya nyumba hii. Hata hivyo, japo Abunuwasi ni mjanja anapewa sifa zingine kama vile mnyanyasaji na mbinafsi katika hadithi hii. Hali hii ya mhusika Abunuwasi kupewa sifa hasi ni kawaida. Ndiposa, Park (2004) anaeleza kuwa katika ngano za Waswahili Abunuwasi husawiriwa kama mwongo, mchoyo na mwenye kiburi. Abunuwasi anakiuka maadili ya kijamii anapotumia ujanja ili

kumlazimisha mfanyabiashara kununua nyumba. Isitoshe, Okwepho (1992) anaeleza kuwa mhusika mjanja analeta mtafaruku katika jamii kwa kuvunja sheria za jamii. Aidha, Andwoa (2018) anaeleza hivi:

Mhusika mjanja hutumia ujanja kama mbinu ya kujifaidi. Aidha anatumia ujanja ili kujiokoa kutokana na hali mbalimbali zinazomkumba. Isitoshe, mhusika mjanja huonekana kama shujaa na chanzo cha burudani katika kazi ya fasihi (Uk. 19).

Maelezo haya ya Andwoa (2018) yanatusawiria tabia za mhusika mjanja. Anabainisha kuwa mhusika mjanja huwa ni mwenye tamaa kwani anajali maslahi yake mwenyewe. Aidha, mhusika huyu huonekana kama shujaa. Hali hii inaoana na Abunuwasi katika ngano ya “Abunuwasi Ajenga Nyumba” kwani Abunuwasi anatumia ujanja ili kumlazimisha mfanyabiashara kununua nyumba. Anatumia ujanja kama mbinu ya kumdhulumu mfanyabiashara na kujifaidi. Hali hii inaonyesha kuwa mhusika mjanja hujali maslahi yake mwenyewe.

Ngano nyingine ni ile ya “Liyongo” iliyomo kwenye kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*. Katika ngano hiyo, Liyongo anatumia ujanja ili kujiokoa gerezani. Anatumia shairi kwa madhumuni ya kumtuma kijakazi kumuambia mamake amwekee tupa ndani ya mkate wa wishwa. Ujanja wake unamsaidia kutoroka gerezani kwa kukereza minyororo akitumia tupa. Askari hawagundui ni kwa nini mkate wa wishwa uliletwa pale. Anapotoroka gerezani anaelekea msituni na anaendelea kuwanyanyasa na kuwaua watu. Liyongo

anatumia ujanja ili kujiokoa kwani alifaa kuuawa. Ndiposa, Hornby (2006) anaeleza hivi:

Mhusika mjanja hufaulu kujitoa kwa hali ngumu inayomkumba kwa kutumia akili (Uk. 127).

Maoni haya ya Hornby (2006) yanaonyesha umuhimu wa akili pevu. Liyongo anatumia akili ili kujiokoa na kutoroka gerezani.

Ngano hizi mbili zinathibitisha kuwa wahusika wajanja katika ngano hupewa sifa hasi. Abunuwasi anasawiriwa kama mnyanyasaji katika ngano ya “Abunuwasi Ajenga Nyumba” ilhali Liyongo anasawiriwa kama muuaji katika ngano ya “Liyongo”.

Hadithi fupi za kisasa za Kiswahili pia zimeiga mtindo huu wa ngano wa kuwapa wahusika wajanja sifa hasi. Mfano ni hadithi ya “Waliohujumu Ujamaa” iliyomo kwenye diwani ya *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*. Katika hadithi hii Fisi ni mjanja. Fisi anajifanya amekufa ili wanyama waje kuomboleza. Anafanya hivi ili apate njia rahisi ya kuwaua. Hata hivyo, wanyama hawa hawafikiri kiundani bali wanaswa kwa mtego wa Fisi. Wanyama hao wanakuja kuomboleza katika kasri na baadaye wanauawa. Mwandishi anampa Fisi sifa zingine kama vile muuaji na mlafi. Mwandishi anaeleza hivi:

Maiti ilikuwa ya marehemu ambaye kichwa chake amekiwekelea kwenye upanga na shoka. Vifaa hivyo vilionyesha makali ya kung'aa na vilionyesha kunolewa kwa ajili maalum. Vile vile, macho ya maiti yalifumbwa lakini meno yote yamekenuliwa kuonyesha weupe na ngeja kwa pamoja. Palepale mdomoni badala ya upovu ambao kwa kawaida humtoka mfu, Sungura katika upekuzi wake aliona mate hasa- ishara ya tamaa. Ni vipi tamaa ikitagaa hata kati ya wafu (Uk. 118).

Dondoo hili linalopatikana katika hadithi ya “Waliohujumu Ujamaa” linatupa taswira ya ujanja wa Fisi. Mwandishi anatueleza kuwa alikuwa amejifanya amekufa ilhali kando yake ameweka upanga. Aidha, anaongezea kuwa Fisi alikuwa anadondokwa na mate- ishara ya kuwa yeye ni mlafi. Hadithi hii inamsawiri mhusika wake mjanja ambaye ni Fisi kwa kumpa sifa hasi. Hali hii ni sawia na ngano za “Abunuwasi Ajenga Nyumba” na “Liyongo” ambazo pia huwapa wahusika wajanja sifa hasi.

Inawezekana kuwa mawazo ya hadithi hii yamechotwa kutoka kwa ngano za hapo awali. Ndiposa, Frye (1957) anaeleza kuwa kazi za kifasihi huchota vipengele vyake kutoka kazi zingine zilizotangulia. Kwa msingi huu basi, inawezekana kuwa hadithi andishi imeiga jinsi ya kusawiri wahusika wajanja kutoka kwa hadithi simulizi yaani ngano. Isitoshe, kudanganyika kwa wanyama hawa kunaonyesha kuwa maoni ya Makgamatha (1993) kuwa wahusika wajinga wanastahili kudanganywa yana mashiko. Hata hivyo, ujanja wa Fisi ni tofauti na ujanja wa Abunuwasi. Hii ni kwa sababu fisi anasababisha mauaji moja kwa moja.

Hata hivyo, imebainika kuwa hadithi hii ya “Waliohujumu Ujamaa” inamsawiri fisi kama mhusika mjanja. Hali hii ni tofauti na baadhi ya ngano. Ngano hutumia wahusika kama vile jogoo, kobe na sungura kama wahusika wajanja. Ngano nyingi humpa fisi sifa kama vile mlafi na mpumbavu. Hali hii inaoana na Nawe (2018) ambaye anaeleza kuwa katika ngano za Kiiraqw, fisi huchukuliwa kama mpumbavu, mjinga, mlafi, mvivu na anayekosa kufanya maamuzi sahihi.

Kwa upande mwingine, zipo hadithi zingine zinazowapa wahusika wajanja sifa chanya. Mfano ni hadithi ya “Uganga wa Pete” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Katika hadithi hiyo, mhusika mjanja anayelitwa Maskini anapewa sifa chanya. Mwandishi anamsawiri Maskini kama msamehevu. Mwandishi anaeleza hivi:

Wezi kufikiria kuwa wanajulikana, wakaamua kwenda kumwomba huyu mganga msamaha ili asiwataje kwa mfalme. Walimwendea, wakapiga magoti ya kuomba samahani, na kuahidi kwenda kumwonyesha mganga mahali walipoificha mali ile. Kiongozi wao akaungama kwa unyenyekevu mkubwa, “Ndisi tulioiba kwa mfalme na umetutaja kama wa kwanza, wa pili na wa tatu,” Maskini alimkata usemi kiongozi kwa kukiri kuwa aliwafahamu kuwa ndio walioiba na kuwa tayari alikuwa anajiandaa kwenda kumwambia mfalme. Aliwakubalia kwa ombi lao la kutotajwa na kisha wakaenda kule kulikokuwa kumefichwa mali ya mfalme. Walipofika, walikuta mali yote na wala haikuwa imeguswa kwa kupunguzwa. Yule mganga aliwasamehe wale wezi, wakafumukana kila mmoja kwenda zake (Uk. 106).

Dondoo hili linalopatikana katika hadithi ya “Uganga wa Pete” linaonyesha kuwa Maskini aliwasamehe wale wezi walioiba mali ya mfalme. Anaamua kutowataja kwa mfalme na kumrudishia mfalme mali yake. Aidha, Maskini ni mhusika ambaye

anatumia ujanja kwa maslahi ya jamii. Anawasaidia wanajamii kukamata Simba mla watu. Ujanja wa Maskini unawaleta wanajamii pamoja. Hali hii ni kinyume na maelezo ya Okwepho (1992) kuwa mhusika mjanja huvunja sheria zilizoundwa na wanajamii na huleta mvurugo baina ya wanajamii. Aidha, Maskini anajali maslahi ya jamii. Hali hii ni tofauti na maelezo ya Andwoa (2018) kuwa mhusika mjanja hujali maslahi yake tu. Isitoshe, imebainika kuwa katika hadithi fupi wahusika wajanja sio wanyama tu bali pia binadamu kama vile Maskini.

Hali kadhalika, kuna hadithi ya “Njia ya Mwongo” iliyomo kwenye diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Katika hadithi hiyo, jirani anatumia ujanja. Anachukua nguo za Korir na Kipchumba na kuzificha. Hali hii inawalazimisha kuenda nyumbani na nguo zingine. Baadaye, wanapatikana na makosa ya kucheza badala ya kuchunga mifugo wao. Hatimaye, wanaadhibiwa na wanabadilika kitabia. Jirani huyo basi anatumia ujanja kuwarekebisha.

4.1.2. Wahusika Katili

Wahusika katili ni wahusika ambao huwanyanyasa wahusika wengine bila kuwaonea huruma. Katika ngano ya “Sultan Darai” kuna mhusika katili. Mhusika huyu ni Sultan. Sultan alisaidiwa na paa ili aweze kuwa tajiri. Baadaye, paa anapokuwa mgonjwa anakataa kumlisha paa huyo. Matokeo yake ni paa kufa. Mwishowe, Sultan Darai anaadhibiwa kwani anarejea na kuwa Maskini ghafla. Funzo la ngano hii ni kuwa mkosa shukrani huteseka.

Wahusika katili wanapatikana katika ngano. Hata hivyo, katika ngano, msimulizi hutetea wanyonge na kuwaadhibu wahusika katili. Ndiposa, Adagala na Kabira (1985) wanaeleza hivi:

Msimulizi huwatetea wanaodhulumiwa. Watoto, wanawake, mayatima, wanyonge na watumwa hutetewa na msimulizi (Uk. xvi).

Maelezo haya ya Adagala na Kabira (1985) yanaonyesha kuwa wahusika wanaodhulumiwa hutetewa na msimulizi. Ndiposa, katika ngano wema hushinda uovu.

Ngano ya “Liyongo” iliyomo kwenye kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* ina mhusika katili aitwaye Liyongo. Liyongo anawanyanyasa wananchi wa Shanga. Aidha, alikuwa anawakataza wananchi kuchanja kuni wala kuchota maji. Mwandishi anaeleza hivi:

Liyongo alienda nje ya jiji na kuwanyanyasa wanakijiji. Watu hawangeweza kuingia ndani ya nchi hiyo wala kuchota maji au kuchanja kuni (Uk. 441).

Dondoo hili linalopatikana katika ngano ya “Liyongo” linathibitisha ukatili wa Liyongo. Liyongo aliwakataza wananchi kuchota maji wala kuchanja kuni. Licha ya ukatili wake, Liyongo anauawa hatimaye. Liyongo anauliwa kwa kudungwa na sindano ya shaba kitovuni mwake. Katika ngano hii, Liyongo anaadhibiwa hatimaye kwa kuuawa. Hali hii inaona na maelezo ya Senkoro (2011) kuwa nia kuu ya ngano ni kuonya, kuadhibu, kufunza na kujenga utu bora.

Hata hivyo, sifa anazopewa Liyongo katika kitabu cha Steere ni tofauti na zile anazopewa katika vitabu vya *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (2001) kilichoandikwa na Matundura na *Tenzi Tatu za Kale* (1999) kilichoandikwa na Mulokozi. Steere anamsawiri Liyongo kama mhusika katili anayewanyanyasa wananchi. Kwa upande mwingine, Mulokozi (1999) na Matundura (2001) wanamsawiri Liyongo kama mhusika mwema anayetetea haki za wanajamii. Katika *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (2001), Matundura anaeleza kuwa Liyongo alimuokoa kijana aliyevamiwa na mamba. Aidha, Mulokozi katika *Tenzi Tatu za Kale* (1999) anaeleza kuwa Liyongo alipendwa na wanajamii wengi hadi wagalla walitaka mbegu yake. Aidha, wanajamii walimtetea aliposhikwa ili asiangamizwe.

Kutokana na haya, imebainika kuwa vitabu vilivyoandikwa wakati wa ukoloni vilisawiri mashujaa wa Kiafrika kwa namna hasi. Ndiposa, Steere anamsawiri Liyongo kama mhusika katili. Aidha, vitabu vilivyoandikwa baada ya nchi za Afrika kupata uhuru vilisawiri mashujaa wa Afrika kwa namna chanya. Hali hii inabainika katika vitabu vya Mulokozi (1999) na Matundura (2001) ambao wanamsawiri Liyongo kama mtetezi wa haki ya wanyonge katika jamii.

Kuna hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zilizo na wahusika katili. Mfano ni hadithi ya “Shetani Hana Hatia” iliyomo kwenye diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Paka-shume ni mhusika katili kwani anamnajisi mpwawe. Licha ya kuwa mpwawe yumo katika Shule ya Chekechea, Paka-shume anamtendea unyama. Mwandishi anaeleza hivi:

“Uiona raha gani kukinajisi kitoto cha Shule ya Chekechea? Uliwakosa wanawake?” Vundumile alimchachia mgonjwa wake kwa maswali mazito mazito kama dharuba za makombora ya vita vya wamarekani na wafuasi wa mtandao wa Al-Qaeda.

“Ni Shetani tu...”

“Mwanamume mzima wewe na akili zako unageuka mnyama na kuyatenda haya- huna soni? Katili mkubwa we! Mbona hukwenda Koinange au Majengo ukanunua mapenzi- kuna hata na ya mbao ati! Uliwamaliza makahaba wote wa jiji hili ndiposa ukawageukia watoto?” (Uk. 58).

Mfano huu katika hadithi ya “Shetani Hana Hatia” unabainisha ukatili wa Paka-shume. Paka-shume anamnajisi mpwawe. Mpwa huyo yumo katika Shule ya Chekechea. Mhusika huyu hamhurumii mpwawe licha ya kuwa mpwawe ana umri mchanga. Hata hivyo, baadaye Paka-shume anaadhibiwa. Paka-shume anakatwa viungo vyake vya nyeti na umati wa watu. Mwandishi anaeleza hivi:

Hasira ilikuwa imewatia wazimu. Mmoja alitoa kisu mfukoni, wengine wakaivuta suruali ya mbakaji iliyokuwa na mabaki ya damu. Alikatwa viungo vilivyomchochea kumbaka mpwa wake (Uk. 62).

Dondoo hili linalopatikana katika hadithi ya “Shetani Hana Hatia” linaonyesha jinsi Paka-shume alivyoadhibiwa kwa kukatwa sehemu zake nyeti. Hali hii ya kuadhibiwa kwa wahusika katili inapatikana pia katika ngano za “Liyongo” na “Sultan Darai”. Mfano huu unaonyesha kuwa mwandishi wa hadithi ya “Shetani Hana Hatia” alikuwa na uelewa wa ngano za awali. Ndiposa, Frye (1957) anaeleza kuwa kazi za fasihi huiga kazi zingine zilizotangulia. Aidha, Landmark (2006) akimnukuu Jung (1959) anamuunga mkono Frye (1957) kwa kueleza kuwa taswira

za usimulizi na wahusika huweza kuigwa na kazi za fasihi. Kwa msingi huu mwandishi wa hadithi ya “Shetani Hana Hatia” ameiga jinsi ngano zinavyosawiri hatima ya wahusika katili. Isitoshe, hatima ya wahusika katili katika hadithi hii inaonyesha kuwa mhimili wa nadharia ya vikale kuwa wahusika wanaopatikana katika ngano na hadithi fupi wanafanana una mashiko. Frye (1976) anaeleza hivi:

Katika mazungumzo kati ya Ayubu na marafiki wake watatu ilibainika kuwa wale ambao hutenda wema hutuzwa. Aidha, wanaotenda maovu huadhibiwa (Uk. 229).

Maelezo haya ya Frye (1976) yanabainisha jinsi marafiki wa Ayubu walivyomsawiri Mola. Walikuwa na maoni kuwa labda Ayubu alimkosea Mola ndiposa akateseka. Hali hii ya kuadhibu wahusika waovu pia inapatikana katika ngano tuliyojadili ya “Liyongo”.

Kuna hadithi ya “Mwavyaji wa Roho” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Hadithi hii ina mhusika katili aitwaye Bwana Kitambi. Bwana Kitambi anawauzia vijana dawa za kulevya ili awe tajiri. Kwa kufanya hivi Bwana Kitambi anawaangamiza vijana wengi mtaani. Mwandishi anaeleza hivi:

Tulienda ukumbini kufuatilia taarifa ya habari ya saa kumi na Jael. Masikitiko. Vijana, wasichana kwa wavulana, wamekula unga hawajielewi walikuwa wakieleza masaibu yao. Jael alicheka hata akatoa machozi. Tulishangaa kuona ami yake akitoa machozi huku akishutumu wanaowauzia vijana mihadarati bila kujali madhara yake. Tumbo langu lilijaa maji karai saba.

“Nimejaribu kuacha nikashindwa. Kucha nanunua shilingi mia mbili. Mara nyingine tunajidunga. Sindano yenyewe ni hiyo moja. Sisi ni wangapi hapa?” mmoja alisimulia kwa masikitiko. Alipoulizwa mbona hawaachi kutumia alijibu ni muhali. “Tumezoea. Hiki ndicho chakula na mke wangu sasa. Hata virusi ninavyo. Sina faida hata nikishikwa na polisi! (Uk. 78).

Dondoo hili linalopatikana kwenye hadithi ya “Mwavyaji wa Roho” linatuonyesha ukatili wa Bwana Kitambi. Anawauzia vijana dawa za kulevya. Vijana hawa wanaambukizwa magonjwa kama vile virusi vya ukimwi. Aidha, wanakosa tumaini maishani. Hali kadhalika, kutokana na matumizi ya dawa za kulevya wanakosa kazi na afya yao imezoroteka.

Licha ya matendo yake, Bwana Kitambi anajitokeza na kujifanya anatetea haki za wananchi. Hatimaye, anapewa wadhifa serikalini badala ya kuadhibiwa. Hali hii ni tofauti na ngano. Katika ngano wahusika katili huadhibiwa. Hata hivyo, katika hadithi ya “Mwavyaji wa Roho” mhusika katili ambaye ni Bwana Kitambi ametuzwa. Mwandishi wa hadithi hii alinua kutuonyesha jinsi wahusika waovu wanafanikiwa kutokana na kutochukuliwa hatua za kisheria. Hali hii huweza kuwa imetokana na janga la ufisadi ambalo limeathiri wanajamii. Ndiposa, Frye (1976) anaeleza kuwa wakati mwingine wahusika waovu hawapatwi na mikasa au kuadhibiwa machoni mwetu. Hali kama hii inaonekana katika hadithi ya “Mwavyaji wa Roho” ambapo mhusika Bwana Kitambi anatajirika kutokana na uovu.

Aidha, kuna hadithi ya “Safari ya Maangamizi” iliyomo kwenye diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Hadithi hii ina mhusika aitwaye Pendo. Mhusika huyu anadhulumiwa. Mwandishi anaeleza hivi:

Sikuamini. Kumbe licha ya kunibikiri vile vinyangarika vilikuwa vimeniambukiza virusi vinavyosababisha ugonjwa wa ukimwi. Lo! Nilitamani kufa mara moja (Uk. 169).

Dondoo hili linalopatikana katika hadithi ya “Safari ya Maangamizi” linaonyesha kuwa Pendo alikuwa na tabia njema. Mwandishi anatueleza kuwa kabla ya kunajisiwa kwake alikuwa ni bikra. Hata hivyo, ananajisiwa na wanaume ambao wanamuambukiza ugonjwa wa ukimwi. Katika hadithi hii, hatuoni wanaume hao wakichukuliwa hatua za kisheria ama kuadhibiwa. Dhana ya wanajamii wanaotenda maovu kutoadhibiwa ni ya kawaida katika jamii ya sasa. Hii inatokana na sababu kuwa wahalifu wengine hawachukuliwi hatua za kisheria. Kwa upande mwingine, ngano ya “Liyongo” iliyomo katika kitabu cha Steere inaonyesha kuadhibiwa kwa mhusika Liyongo kwa sababu ya kutenda maovu.

Hata hivyo, wahusika Paka-shume na Bwana Kitambi waliomo katika hadithi za “Mwavyaji wa Roho” na “Shetani Hana Hatia” wamepewa majina ya kimajazi. Majina yao yanaafiki tabia zao. Paka-shume ni jina linaloashiria mnyama anayenyemelea na kuvizia wanyama wengine ili kuwashika. Tabia hii inamuafiki mhusika huyu kwani anamvizia na kumnajisi mpwawe. Aidha, Kitambi ni tumbo linalotokea mbele kutokana na unene. Mara nyingi kitambi hutumiwa kuashiria

mtu tajiri. Jina hili linamuafiki Bwana Kitambi kwa kuwa ametajirika sana. Isitoshe, ana pupa ya kupata mali. Mwandishi anaeleza kuwa alikuwa na magari mengi na biashara nyingi. Mbinu hii ya majazi hupatikana katika tanzu mbalimbali ya fasihi ikiwemo ngano na hadithi fupi.

4.1.3 Wahusika Mashujaa

Shujaa ni mtu mwenye moyo thabiti anayeweza kukabili masuala hatari katika jamii. Majina yenye maana sawia na shujaa ni kama vile: jagina, nguli, jabali na jogoo. Kemunto (2015) anaeleza kuwa shujaa huwa na sifa za kiajabu zilizotiliwa chumvi na jamii husika. Mfano ni Lwanda Magere ambaye anasawiriwa kama mhusika ambaye alikuwa na nguvu nyingi. Aidha, mkuki haungeweza kupenyeza mwili wake. Hata hivyo, Aylestock (2009) anatofautiana na maoni ya Kemunto (2015) kwa kueleza kuwa si lazima shujaa awe na sifa za kiajabu bali anaweza kuwa binadamu wa kawaida. Aidha, Aylestock (2009) anaongezea kwa kueleza kuwa jambo muhimu ni kuwa shujaa akabiliane na mhusika mpinzani na kuibuka na ushindi.

Mulokozi (1996) anaeleza aina tatu za mashujaa ambao hujitokeza katika kazi ya fasihi. Mashujaa hawa ni: mashujaa wa kijadi kwa mfano Liyongo, mashujaa wa kidini kwa mfano Yesu na mashujaa wa kubuni kwa mfano Tajiri Mbaya katika utendi wa Masahibu. Mashujaa hawa huweza kujitokeza katika ngano na hadithi fupi.

Ngano ya “Liyongo” iliyomo kwenye kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* ina mhusika aitwaye Liyongo. Liyongo ni shujaa wa kijadi. Anathibitisha sifa za kishujaa kama vile: akili pevu, nguvu za kimwili, nguvu za kivita na ustadi katika kutunga nyimbo. Katika ngano ya “Liyongo” mwandishi anaeleza kuwa Liyongo alikuwa na nguvu nyingi. Kwa sababu ya nguvu zake aliogopewa na wengi. Mwandishi anaeleza hivi:

Wakatupa vitu vyao na kwenda mbio wasidiriki,
akawakamata akawapiga vita akawaua (Uk. 446).

Dondoo hili linalopatikana katika ngano ya “Liyongo” linaonyesha jinsi Liyongo alivyoogopewa kiasi kuwa askari walitoroka badala ya kumkabili. Aidha, Liyongo aliwanyanyasa wananchi kwani aliwakataza wananchi kuchota maji kisimani. Inashangaza jinsi mtu mmoja anaweza kuogopewa na kijiji kizima kiasi kuwa hawezi kukabiliwa na yeyote. Hali hii inaonyesha kuwa nguvu za Liyongo zimetiliwa chumvi. Kutiliwa chumvi kwa sifa za shujaa ni dhana ya kawaida. Ndiposa, Frye (1957) anaeleza kuwa shujaa wa tanzia huwa na uwezo unaoning’inia kati ya Miungu na binadamu wa kawaida. Aidha, Gichamba (2005) anashadidia maoni haya kwa kueleza kuwa shujaa huwa na tabia za kustaajibisha kiasi kuwa wanajamii humwona kuwa kiumbe asiye wa kawaida.

Hata hivyo, kitabu cha *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (2001) kinaonyesha matukio mengine ambayo hayamo katika kitabu cha Steere. Matundura (2001) anaeleza kuhusu nguvu alizokuwa nazo Liyongo. Anaeleza kuwa Liyongo alikuwa na nguvu kiasi kuwa anafaulu kuangamiza mamba aliyemshambulia kijana mmoja. Aidha,

anasafiri kutoka Pate hadi Shanga kwa siku mbili. Safari hii ingemchukua mtu wa kawaida siku nne. Isitoshe, Liyongo alilala msituni kwa sababu alikuwa na uwezo wa kuuha mnyama yeyote.

Steere anathibitisha kuwa Liyongo alikuwa na akili pevu. Mwandishi huyu anaeleza kuwa wanakijiji walipanga kumfuma mishale anapopanda mti. Hata hivyo, Liyongo anatambua kuwa wanakijiji hao wanataka kumuangamiza. Anaamua kuchuma mikoma kwa kutumia mishale badala ya kupanda mti. Baada ya kisa hiki, wanakijiji walimuona Liyongo kama binadamu asiye wa kawaida. Mwandishi anaeleza hivi:

Wale wakamwaga, wakamwambia-Kukuingia hadaani
Liyongo fumo si mtu, Yunga jini Liyongo okoka (Uk. 448).

Dondoo hili linalopatikana katika hadithi ya “Liyongo” linaonyesha kuwa wanakijiji walimlinganisha Liyongo na ‘Shetani’. Hii ni kwa sababu ya nguvu zake za kiakili. Hali hii ya shujaa kudhaniwa kuwa na usikawaida imo katika ngano ya visakale. Ndiposa, Gichamba (2005) anaeleza kuwa shujaa huwa na tabia ya kustaajibisha kiasi kuwa wanajamii humwona kuwa kiumbe asiye wa kawaida.

Aidha, mtotowe anapomuuliza siri ya nguvu yake Liyongo anatambua mara moja kuwa mtotowe ametumwa ili kumuangamiza. Sifa anazopewa Liyongo ni sawia na sifa za mashujaa katika tendi. Mulokozi (1999) anaeleza kuwa shujaa wa tendi huwa na nguvu za kiakili, kivita, kiume na za uganga. Kwa msingi huu Liyongo

anaonyesha baadhi ya sifa za mashujaa wa tendi kama vile: nguvu za kiakili na nguvu za kivita.

Mwishowe, Liyongo alikuwa na kipawa cha kutunga mashairi na nyimbo. Kipawa hiki kiliwafanya wanakijiji kumtembelea gerezani ili kusikiliza nyimbo zake. Hata hivyo, licha ya uwezo wa Liyongo anauawa kwa njia rahisi. Mtotowe anamuua kwa kumdunga na sindano ya shaba kitovuni mwake. Hali hii inaonyesha kuwa Liyongo alikuwa na nguvu za uganga kwani anauliwa tu na sindano ya shaba kudungwa kitovuni mwake. Aidha, mtotowe Liyongo anakamatwa. Kufa kwa shujaa ni kikale. Ndiposa, Olrik (1965) anaeleza kuwa katika ngano ya visakale ni lazima kuwe na kifo cha shujaa. Aidha, anaongezea kuwa msaliti anahukumiwa. Hali kadhalika, Frye (1957) na Mbogo (2011) wanaunga mkono maoni ya Olrik (1965) kwa kueleza kuwa shujaa lazima aanguke au afe. Isitoshe, Guerin (2005) anaeleza kuwa shujaa lazima afe ili alipie dhambi za jamii. Hali hii ni tofauti kwani Liyongo hafi kwa sababu ya makosa ya wanajamii.

Ngano nyingine iliyo na mhusika shujaa ni ile ya “Abunuwasi na Wezi Wawili” iliyomo kwenye kitabu cha *Myths and Legends of the Swahili*. Ngano hiyo ina mhusika Abunuwasi. Abunuwasi anaonyesha sifa moja ya shujaa ambayo ni akili pevu. Abunuwasi anawadanganya wezi wawili kuwa ana mti unaozaa matunda na wanaamini. Aidha, anawaambia kuwa ana kijiti kinachoweza kufufua watu na wanaamini. Anatumia akili kiasi kuwa wezi hao wawili hawatambui ujanja wake. Mwandishi anaeleza hivi:

Abunuwasi alifikiria namna ya kulipiza kisasi. Abunuwasi basi alipanda mti na kutengeneza shimo katikati ya tunda moja. Baadaye akaingiza dhahabu kadhaa ndani ya tunda hilo (Uk. 114).

Dondoo hili linalopatikana kwenye ngano ya “Abunuwasi na Wezi Wawili” linathibitisha kuwa Abunuwasi ana akili pevu. Abunuwasi anaweka dhahabu ndani ya tunda. Anatumia mbinu hii ili kuwadanganya wezi wawili kuwa ana mti unaozaa dhahabu. Abunuwasi anawashinda adui wake wote. Hali hii inaoana na maelezo ya Child na Fowler (2006) kuwa haiwezikani kumnyanganya jagina cheo chake cha ujagina. Hata hivyo, ushujaa wa Abunuwasi ni tofauti na ushujaa wake Liyongo. Abunuwasi anawashinda maadui wake wote ilhali Liyongo anauliwa hatimaye.

Kwa upande mwingine, kuna hadithi ya “Uganga wa Pete” iliyo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Hadithi hii ina mhusika anayeitwa Maskini. Maskini anafanya jambo ambalo linashangaza. Inashangaza jinsi Maskini alivyobebwa na simba bila kushambuliwa. Hali hii inaweza kumfanya mhusika huyu alinganishwe na shujaa. Mwandishi anaeleza hivi:

Ilikuwa kama saa sita hivi askari alipopeleka ripoti kumhusu mganga; na saa moja baadaye, simba akafika nyumbani kwa mfalme mganga akiwa mgongoni. Japo wote walikuwa wamechoka hoi, simba alikuwa zaidi. Aliweza kuangushwa kirahisi na askari wa mfalme wapatao sita na kwa matumizi ya mafumo mganga akaokolewa (Uk. 108).

Mfano huu unabainisha jinsi Maskini alivyobebwa na simba bila kushambuliwa. Hata hivyo, ushujaa wa Maskini ni wa kubahatisha kwani anapofika kwa mfalme

inabidi aokolewe na watu. Aidha, Maskini anasuluhusha matatizo ya wanajamii. Maskini aliweza kupata pete ya mfalme, mali ya mfalme iliyoibwa na wezi na kushika Simba mla watu. Uwezo wake unawafanya wanakijiji kufikiria kuwa yeye ni mganga. Aidha, wanampa wadhifa serikalini kwa kumuona kama shujaa. Ndiposa, Campbell (2004) anaeleza kuwa shujaa hukumbwa na majaribio ambayo anatarajiwa kuyashinda yote. Kutokana na maelezo ya Campbell (2004), Maskini ni shujaa kwa kuwa ametatua matatizo yanayokumba wanajamii bila kushindwa.

Hata hivyo, ushujaa wa Maskini ni wa kubahatisha. Maskini anauliza mke wake usaidizi kabla asuluhishe jambo. Inasadifu kuwa mke wake yuko katika maeneo masuala haya hutukia. Mke wake basi anamuambia afanye nini. Kwa msingi huu basi Maskini hawezi kulinganishwa na Abunuwasi kwani Abunuwasi anasuluhisha masuala yote yanayomkumba bila kuhitaji usaidizi. Mwandishi wa hadithi hii anasawiri mhusika Maskini kama binadamu wa kawaida anayehitaji usaidizi. Hali hii inaoana na kauli ya Frye (1957) anapoeleza kuwa wakati mwingine shujaa huweza kuwa na uwezo unaotoshana na binadamu wa kawaida.

4.1.4 Wahusika Majahili (Wakinzani wa Nguli)

Park (2004) anaeleza kuwa jahili ni mhusika ambaye humdhuru shujaa ama wahusika wengine ili aweze kupata atakacho. Mfano ni mtotowe Liyongo ambaye alimuua Liyongo ili aweze kuwa mfalme. Aidha, Olrik (1965) anaongezea kuwa katika baadhi ya visakale mhusika jahili huadhibiwa. Isitoshe, Larsen (2018)

anaeleza kuwa Yesu alikuwa ni shujaa. Larsen (2018) anaongezea mawazo yake kwa kueleza kuwa Yesu alikuwa na maadui kutokana na kutenda miujiza.

Ngano ya “Liyongo” iliyomo kwenye kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* ina mhusika jahili. Mhusika huyu ni mtotowe Liyongo. Mtoto wake Liyongo anamuua Liyongo ili aweze kupewa ufalme na wanakijiji. Hata hivyo, baada ya kifo cha Liyongo wanakijiji wanamsaliti kwani wanamshika badala ya kumpa ufalme. Mwandishi anaeleza hivi:

Akaenda kuwaambia watu mjini, ya kwamba amekufa, wakaenda kumtazama, wakamwona amekufa, wakamzika, na kaburi lake laonekana katika Ozi hata leo. Wakamkamata kile kijana, wakaamua, wasimpe ufalme (Uk. 452).

Dondoo hili linalopatikana katika ngano ya “Liyongo” linaonyesha kifo cha Liyongo na kushikwa kwa mtotowe Liyongo. Baada ya Liyongo kufa anazikwa. Kuzikwa kwa Liyongo na kuadhibiwa kwa mhusika jahili ni dhana ya kawaida. Ndiposa, Orlík (1965) anaeleza kuwa katika ngano ya visakale shujaa huzikwa huku mhusika jahili akiadhibiwa. Katika ngano hii, mtotowe Liyongo anasawiriwa kama mwenye tamaa kwani anamuua Liyongo ili apate ufalme.

Kwa upande mwingine, hadithi ya “Uganga wa Pete” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* ina wahusika majahili. Kuna watu kijijini ambao hawakuamini kuwa Maskini ni mganga halisi. Mwandishi anaeleza hivi:

Wakati Maskini akibahatisha ufanifu wake, kulikuwa na watu ambao hawakuamini kabisa uganga wake. “Huyu bwana si mganga bali mbabaishaji tu,” baadhi yao walisikika wakisema. Waliomba kutokee tukio ambalo lingeweza kumbainisha kama mrongo mkubwa. Ni wakati huu ambapo kulikuja najambazi wakapora mali kwa mfalme. Mfalme akaamua kumwita tena Maskini ilia je aseme kama vile vitu vilivyoibwa vimefichwa wapi (Uk. 104).

Dondoo hili linalopatikana katika hadithi ya “Uganga wa Pete” linaonyesha kuwa Maskini alikuwa na wapinzani. Wapinzani hao waliomba kutokee kisa ambacho kingethibitisha kuwa Maskini si mganga. Ni wakati huo ndipo kulikoibwa kwa mfalme. Hata hivyo, Maskini anashinda jaribio hili kwani anapata mali ya mfalme. Hadithi hii ni tofauti na ngano ya “Liyongo”. Katika ngano ya “Liyongo” mhusika jahili anapewa sifa hasi kama mwenye tamaa ilhali katika hadithi ya “Uganga wa Pete” wakinzani wa Maskini wana sifa chanya kwani wanataka tu ukweli ufichuke. Wakinzani hawa hawaadhibiwi. Hali hii ni tofauti na maoni ya Olrik (1965) kuwa mhusika jahili lazima aadhibiwe.

Imebainika kuwa wakati mwingine mhusika jahili humshinda mhusika shujaa. Kwa mfano Liyongo anauliwa na mtotowe. Mhusika jahili hufanya hivi kwa kutambua udhaifu wa shujaa. Kwa msingi huu basi mhusika jahili huweza kuwa shujaa. Ushujaa huu huweza kutegemea mtazamo wa mwandishi na msomaji. Katika kisakale cha Lwanda Magere, Lwanda Magere anauliwa na wanandi. Hii ni baada ya mkewe kutambua siri ya nguvu zake na kuwaambia wanandi. Mke wa Lwanda Magere japo ni mhusika jahili anaweza kuchukuliwa kama shujaa. Inawezekana

kuwa wanandi walimchukulia kama shujaa kwa sababu aliwasaidia kuangamiza adui wao ambaye ni Lwanda Magere.

4.1.5 Wahusika Wema

Wahusika wema ni wahusika ambao hutenda matendo yanayokubalika na jamii. Ogamba (2015) anaeleza kuwa wahusika wa ngano huwa bapa yaani hawabadilishi tabia kutoka mwanzoni mwa kazi za fasihi hadi mwisho. Aidha, anaongezea kuwa wahusika hawa huweza kuwa wema au waovu.

Ngano ya “Sultan Darai” iliyomo kwenye kitabu cha *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* ina mhusika aitwaye seremala. Seremala anasawiriwa kama mhusika mwema kutoka mwanzoni hadi mwishoni mwa hadithi. Mwandishi anaeleza kuwa kila siku alipotoka kazini aliwataka wanawe wote wale pamoja naye. Aidha, alipogundua kuwa mwanawe anateswa na mke wake aliamua kununua mtumwa. Mtumwa huyu anapewa jukumu la kumtunza mwanawe. Seremala anatenda wema kwani hamfukuzi mkewe. Mwandishi anarudia tukio la seremala kuwaita wanawe mara tatu katika ngano ya “Sultan Darai” ili kusisitiza kuwa alikuwa ni mtu mwema. Mwandishi anaeleza hivi:

Akamwambia waite watoto tule chakula. Mwanamke
akamwambia, Ah! Bwana watoto wale mara mbili, nami
nimekwisha wapa sehemu zao (Uk. 17).

Hadithi fupi za kisasa za Kiswahili pia zimekopa mtindo huu wa usawiri wa wahusika kiasi kwamba kuna wahusika wema. Mfano ni hadithi ya “Kadhia ya

Sikujua” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Katika hadithi hii, kuna wahusika wema ambao ni: Bi. Rehema, Staha na Binti Baraka. Bi Rehema alipewa sifa kama vile: mcha Mungu, mwenye mkono wazi, msaidizi wa wote na asiye na kinyongo. Isitoshe, watoto wa Bi Rehema ambao ni Staha na Binti Baraka wamepewa sifa chanya kama vile: wenye bidii, wenye heshima na wasaidizi kwa wote. Wahusika hawa hawabadilishi tabia zao kutoka mwanzoni mwa hadithi hadi mwisho.

Hali hii inayopatikana katika hadithi ya “Kadhia ya Sikujua” ni sawia na ngano tuliyojadili ya “Sultan Darai”. Mwandishi wa hadithi hii alikuwa na uelewa wa ngano za awali. Hata hivyo, tofauti na ngano ambayo huwa na sifa moja kuu inayomtambulisha mhusika, hadithi hii inawapa wahusika wake sifa kadhaa. Mfano ni Bi. Rehema anayepewa sifa ya mkono wazi, msaidizi wa wote na mcha Mungu. Kwa msingi huu, wahusika wa hadithi fupi hawawezi kuitwa bapa maana hawapewi sifa moja kuu inayowatambulisha.

Aidha, kuna hadithi ya “Namchukia Baba Yangu” iliyomo kwenye diwani ya *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007). Hadithi hii inatumia mbinu ya majazi. Wahusika katika hadithi ya “Namchukia Baba Yangu” wanapewa majina yanayoafiki tabia zao moja kwa moja. Mwandishi anawapa wahusika hawa majina kama vile: Bahati, Mfuata Mali na Mafutu. Majina haya yanaafiki matendo ya wahusika hawa hadithini.

Hata hivyo, kuna hadithi zinazokuwa na wahusika wanaobadilika kitabia. Mfano ni hadithi ya “Safari ya Maangamizi” iliyomo kwenye diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Katika hadithi hii mhusika aitwaye Pendo anaweza kuchukuliwa kuwa mwema mwanzoni mwa hadithi. Kabla ya kunajisiwa na wanaume, Pendo anapewa sifa chanya kama vile: mwenye bidii na msaidizi wa wote. Kutokana na sifa hizi alipendwa na wengi. Mwandishi anaeleza hivi:

Sikuamini. Kumbe licha ya kunibikiri vile vinyangarika vilikuwa vimeniambukiza virusi vinavyosababisha ugonjwa wa ukimwi? Lo! Nilitamani kufa mara moja. Nilitaka kujitia kitanzi. Lakini nikawaza, nikaona sifi peke yangu. Sharti nilipize kisasi. Nitawafunza adabu wana wa Adamu (Uk. 169).

Mfano huu unabainisha kuwa Pendo alikuwa na tabia njema. Kabla ya kunajisiwa kwake, Pendo alikuwa bikra. Hata hivyo, baada ya kunajisiwa anakuwa mwovu kupita kiasi kwani anawaambukiza wanakijiji virusi vya ukimwi.

Mwishowe, kuna hadithi ya “Dr. Strese” iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Katika hadithi hii, kuna mhusika aitwaye Dr. Strese. Dr. Strese alikuwa ni mwenye bidii masomoni na pia mwadilifu. Aliweza pia kulipa karo ya wapwaze. Hata hivyo, mwandishi anaeleza kuwa Strese alikuwa na udhaifu. Anaeleza kuwa Dr. Strese aligeuka na kuwa mlevi wa kupindukia baada ya kuchelewa kuo. Hali hii ilimfanya kutowajibika kazini. Mwandishi anaeleza hivi:

Basi pole pole alizuru vilabu vya pombe na wenzake na baada ya muda hamu ikamkalia. Ukarimu wake ukaendelea kuwafaidi rafikize kwenye vilabu hivyo. Hao ndio waliokuwa jamii yake sasa na hakuwakunjia mkono. Maisha yaliendelea na muda si muda, athari ya unywaji pombe ilionekana kazini. Daktari Strese hakuonekana tena kuwajali wateja wake na maana ya maisha kwake ikapotea (Uk. 49).

Nukuu hii inaonyesha kuwa Dr. Strese alibadilika kitabia na akawa mlevi wa kupindukia. Aidha, anakosa kuwajibika kazini. Ulevi wake unasababishwa na ugunduzi wake kuwa hakuwa ameoia licha ya kuwa alikuwa tayari ameanza kuzeeka.

Hadithi hizi mbili za “Dr. Strese” na “Safari ya Maangamizi” zinatonyesha kuwa hakuna mhusika mwema. Kulingana na hadithi hizi, hali ndizo husababisha mtu kuwa mwema au mwovu. Aidha, kila mtu huwa na ubora na udhaifu wake. Hali hii ni tofauti na ngano. Katika ngano kuna wahusika wema. Wahusika hawa hupewa sifa njema kutoka mwanzoni hadi mwishoni mwa ngano. Mfano ni mhusika seremala anayepatikana katika ngano ya “Sultan Darai”.

4.2 Hitimisho

Sura hii imeangazia wahusika wanaopatikana katika ngano na hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Mtafiti amejadili wahusika kama vile: wahusika wajanja, wema, majahili, mashujaa na katili. Imebainika kuwa wahusika wanaopatikana katika ngano pia wanapatikana katika hadithi fupi. Hata hivyo, wahusika wa ngano wanasawiriwa kwa njia tofauti ikilinganishwa na wahusika wa hadithi fupi. Usawiri

huu unathibitisha kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili sio zao la mchakato wa kistari wa kutoka kwa ngano hadi kwa hadithi fupi.

Utafiti huu umebaini kuwa wahusika wajanja katika ngano huwa na sifa hasi kama vile wauaji na wenye tamaa. Aidha, wahusika wema katika ngano hawabadilishi tabia yaani ni bapa. Kwa upande mwingine, wahusika katili katika ngano huadhibiwa huku wahusika mashujaa wanapewa sifa zinazopita mipaka ya binadamu. Isitoshe, wahusika majahili hupewa sifa hasi kama vile wenye tamaa. Hata hivyo, imebainika kuwa ngano ya Liyongo iliyomo katika kitabu cha Steere inamsawiri Liyongo kwa namna hasi. Liyongo anachukuliwa kama mnyanyasaji wa wanajamii. Hali hii ni tofauti na vitabu vya *Mkasa wa Shujaa Liyongo* na *Tenzi za Kale*. Vitabu hivi vinamsawiri Liyongo kwa namna chanya. Vitabu hivi vinamsawiri Liyongo kama mtetezi wa haki za wanyonge anayependwa na wengi.

Kwa upande mwingine, hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zinasawiri wahusika wake kwa namna tofauti. Wahusika wajanja katika hadithi fupi hupewa sifa chanya kama vile wasamehevu na wanaojali maslahi ya jamii. Isitoshe, wahusika wajanja huweza kupewa sifa hasi kwa mfano Fisi katika hadithi ya “Waliohujumu Ujamaa” anasawiriwa kama mlafi na muuaji. Aidha, katika hadithi fupi imebainika kuwa hakuna mhusika mwema kwani hali ndizo humfanya mhusika kuwa mwema au mwovu. Isitoshe, katika hadithi hizi sio lazima mhusika katili aadhibiwe. Aidha, mhusika jahili hupewa sifa chanya kama vile mkweli. Mwishowe, mashujaa wa

hadithi fupi huwa na sifa zinazotoshana na binadamu. Hii ni kwa sababu wanauliza usaidizi wanaposhindwa kusuluhisha jambo.

Hata hivyo, kuna hadithi zingine za kisasa za Kiswahili zilizoonyesha sifa za wahusika zinazofanana na ngano. Mfano ni “Kadhia ya Sikujua” na “Shetani Hana Hatia”. Katika hadithi ya “Kadhia ya Sikujua” mwandishi anasawiri wahusika Bi. Rehema, Staha na Hiana kama wahusika wema. Wahusika hawa hawabadilishi tabia zao kutoka mwanzoni mwa hadithi hadi mwishoni. Isitoshe, Paka-shume anaadhibiwa katika hadithi ya “Shetani Hana Hatia”. Kuadhibiwa kwake kunatokana na uovu wake. Hali hii ni sawia na ngano tulizojadili zilizomo katika vitabu vya *Myths and Legends of the Swahili* na *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*.

Isitoshe, imebainika kuwa katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili na ngano kuwa si lazima mhusika shujaa afe. Wahusika mashujaa wakati mwingine huwapiku maadui wao wote. Mfano ni mhusika Abunuwasi katika ngano ya “Abunuwasi na Wezi Wawili” na mhusika Maskini katika hadithi ya “Uganga wa Pete”.

SURA YA TANO

HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO YA

UTAFITI

5.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia muhtasari wa sura za awali. Aidha, matokeo ya utafiti kwa mujibu wa malengo yameshughulikiwa. Mwishowe, mtafiti ametoa mapendekezo ya utafiti unaoweza kufanyiwa na ambao unahusiana na mada hii.

5.1 Muhtasari

Utafiti huu ulidhamiria kuonyesha mshabaha na tofauti kati ya hadithi fupi ya kisasa na ngano. Ili kufanya hivi, mtafiti ameongozwa na nadharia ya vikale kwa mujibu wa Frye (1957). Alikuwa na malengo manne. Lengo la kwanza lilikuwa ni kubainisha namna mbalimbali miundo hujitokeza katika ngano na hadithi fupi. Pili, mtafiti aliangazia mitindo inayojitokeza katika ngano na hadithi fupi. Tatu, mtafiti alilenga kuangazia maudhui yanayoshughulikiwa katika hadithi fupi na ngano. Aidha, lengo la nne lilikuwa ni kufafanua wahusika mbalimbali wanaopatikana katika ngano na hadithi fupi. Utafiti huu umeangazia diwani tatu. Nazo ni: *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007) ya Mwenda Mbatiah, *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* (2011) ya Leonard Sanja na *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* (2006) ya Mc Onyango. Hadithi tisa ziliteuliwa kupitia mbinu kusudio ili kufanikisha utafiti wetu. Mtafiti alitumia utaratibu maalum wa kuchagua hadithi hizi. Utaratibu huo ulihusu kuteua hadithi zilizo na sifa zinazofanana na ngano na zile zilizo na sifa zinazotofautiana na ngano. Aidha, mtafiti alichambua ngano nne

zinazopatikana katika vitabu vya *Myths and Legends of the Swahili* (1970) ya Jan Knappert na *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* (1870) ya Edward Steere.

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza imeangazia masuala ya kimsingi yanayohusishwa na utafiti huu. Masuala yaliyoangaziwa ni pamoja na: suala la utafiti, sababu za kuchagua mada, malengo ya utafiti, upeo na mipaka na yaliyoandikwa kuhusu mada. Aidha, mtafiti ameshughulikia nadharia ya vikale. Mwisho, mbinu za utafiti zimeangaziwa pamoja na uteuzi wa sampuli, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data.

Sura ya pili imeangazia miundo na mitindo mbalimbali inayojitokeza katika ngano na hadithi fupi. Miundo kama vile: mwanzo, kati na mwisho imechunguzwa. Aidha, mtafiti amechunguza mtindo wa safari, mtindo wa nambari na urudiaji wa maneno na vishazi katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili na ngano.

Isitoshe, sura ya tatu imefafanua maudhui mbalimbali yanayoshughulikiwa katika ngano na hadithi fupi. Maudhui kama vile: wema na uovu, ujanja, ushujaa na kifo. Katika uchunguzi wetu tulidhamiria kuonyesha namna maudhui haya yanasawiriwa katika ngano na hadithi fupi.

Hali kadhalika, katika sura ya nne mtafiti aliazimia kufafanua wahusika wanaopatikana katika ngano na hadithi fupi. Wahusika walioangaziwa ni: wahusika wajanja, katili, majahili, wema na mashujaa. Utafiti huu uliazimia kuonyesha ikiwa

sifa wanazopewa wahusika katika ngano zinafanana na sifa wanazopewa wahusika katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.

Mwishowe, sura ya tano ni hitimisho la utafiti. Katika sura hii, muhtasari wa kila sura ya tasnifu hii imeangaziwa. Matokeo ya utafiti na mapendekezo ya utafiti wa baadaye pia yametolewa.

5.2 Matokeo ya Utafiti kwa Mujibu wa Malengo

Utafiti umebaini kwamba kulingana na ushahidi uliopo hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili sio kimelea cha ngano. Hii ni kwa sababu miundo na mitindo ya ngano na hadithi fupi za kisasa za Kiswahili hutofautiana. Aidha, ngano husawiri maudhui yake kwa namna tofauti ikilinganishwa na hadithi fupi. Mwishowe, sifa wanazopewa wahusika wa ngano ni tofauti na zile sifa wanazopewa wahusika wa hadithi fupi.

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kuonyesha namna mbalimbali ya ngano na hadithi fupi hujitokeza. Aidha, lengo letu la pili liliangazia mitindo inayojitokeza katika ngano na hadithi fupi. Tuliweza kugundua kuwa miundo na mitindo ya ngano na hadithi fupi hutofautiana. Ngano huwa na sifa za kimtindo na kimuundo kama vile: mwanzo wa kifomula, mwisho wa kifomula, mwisho wa kiadili, urudiaji wa maneno na urudiaji wa nambari maalum. Kwa upande mwingine, hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zina sifa zifuatazo za kimtindo na kimuundo: mwanzo na miishio isiyo ya kifomula. Hali kadhalika, hadithi hizi hazikuonyesha urudiaji wa maneno wala urudiaji wa nambari maalum.

Hata hivyo, kuna hadithi ya “Uganga wa Pete” iliyoonyesha sifa za kimtindo na kimuundo sawia na za ngano tulizojadili. Hadithi hii ina mwanzo wa kifomula, mwisho wa kifomula na urudiaji wa maneno. Sifa hizi zinafanana na sifa za kimtindo na kimuundo zilizomo katika vitabu vya *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* na *Myths and Legends of the Swahili*. Isitoshe, imebainika kuwa sehemu ya kati ya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili na ngano hufanana. Hii ni kwa sababu katika ngano na hadithi fupi sehemu hii husheheni migogoro. Aidha, katika sehemu hii ndiyo mwandishi hukuza dhamira yake.

Lengo la tatu katika utafiti huu liliuia kufafanua maudhui yanayoshughulikiwa katika ngano na hadithi fupi. Imebainika kuwa ngano husawiri maudhui yake kwa namna tofauti ikilinganishwa na hadithi fupi. Katika ngano zilizochanganuliwa ujanja hutumiwa kuendeleza uovu, kifo husababishwa na makosa ya mhusika na ushujaa hutambulishwa na sifa zinazozidi mipaka ya binadamu. Isitoshe, katika ngano wema hutuzwa huku uovu ukiadhibiwa. Kwa upande mwingine, katika hadithi fupi ujanja hutumiwa ili kuendeleza wema na pia uovu, ushujaa hutambulishwa na sifa zinazoweza kuaminika na kifo huweza kusababishwa na sababu zisizoepukika kama vile magonjwa. Aidha, katika hadithi fupi sio lazima uovu uadhibiwe. Hadithi fupi za kisasa za Kiswahili huweza kuishia uovu ukikosa kuadhibiwa. Hali hii inaonyesha kuwa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zinasawiri ukweli uliopo katika jamii kuwa wahalifu wengine katika jamii wanakosa kuchukuliwa hatua za kisheria. Hii ni kwa sababu hamna ushahidi wa kutosha dhidi yao au wanakwepa mitego ya polisi kwa kutoa rushwa.

Usawa baina ya maudhui yaliyomo katika ngano na hadithi fupi huweza kuwa umetokana na hali zilizowaathiri wanajamii. Masuala kama vile: ujanja, uovu, wema, ushujaa na kifo yaliathiri jamii nyingi za Kiafrika. Hata hivyo, kuna hadithi ya “Waliohujumu Ujamaa” iliyomo kwenye diwani ya *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*. Hadithi hii ilionyesha sifa moja inayofanana na ngano tulizojadili. Katika hadithi hii, wanyama walikufa kutokana na makosa yao. Hali hii ni sawia na jinsi ngano inavyosawiri kifo.

Hadithi hii ya “Waliohujumu Ujamaa” inasawiri kifo kwa namna sawia na ngano tulizojadili. Hali hii inaweza kubainisha kuwa mwandishi wa hadithi hii alikulia katika mazingira ya fasihi simulizi. Ndiposa kwa hiari yake alichota kipengele cha fasihi simulizi haswa ngano na kukitumia katika uandishi wake wa hadithi fupi.

Hatimaye, lengo letu la nne liliangazia wahusika wanaopatikana katika ngano na hadithi fupi. Imebainika kuwa wahusika katika ngano wanapewa sifa tofauti na wahusika katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Katika ngano, wahusika wajanja na wahusika majahili hupewa sifa hasi kama vile wenye tamaa. Isitoshe, wahusika mashujaa hupewa sifa zinazozidi mipaka ya binadamu. Aidha, katika ngano ni lazima wahusika katili waadhibiwe. Hatimaye, wahusika wema huwa bapa yaani hawabadiliki na kutenda uovu hata mara moja. Kwa upande mwingine, hadithi fupi za kisasa za Kiswahili huwapa wahusika wajanja na majahili sifa chanya. Hata hivyo, wahusika wajanja katika hadithi fupi pia huweza kupewa sifa hasi kwa mfano Fisi katika hadithi ya “Waliohujumu Ujamaa” anasawiriwa kama

mlafi na muuaji. Hali kadhalika, hadithi fupi za Kisasa za Kiswahili huweza pia kutumia binadamu kama wahusika wajanja. Mfano ni Maskini katika hadithi ya “Uganga wa Pete”. Aidha, katika hadithi fupi hakuna mhusika mwema kwani kila mtu ana ubora na udhaifu wake. Isitoshe, wahusika mashujaa hupewa sifa zinazoweza kuaminika. Mwishowe, katika hadithi fupi si lazima wahusika katili waadhibiwe.

Hata hivyo, kuna hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zilizoonyesha sifa zinazofanana na ngano kibahati nasibu. Hadithi ya “Kadhia ya Sikujua” ina mhusika mwema. Katika hadithi hii wahusika Bi. Rehema na Staha wanabakia kuwa wema kutoka mwanzoni mwa hadithi hadi mwisho. Hali hii ni sawia katika ngano. Hata hivyo, wahusika wa hadithi hii hawawezi kuitwa bapa. Hii ni kwa sababu wanapewa sifa nyingi njema zinazowatambulisha. Mfano ni Bi. Rehema ambaye ni mcha Mungu, mkono wazi na msaidizi wa wote. Hali hii ni tofauti na ngano ambapo wahusika hupewa sifa moja kuu inayowatambulisha. Isitoshe, mhusika katili aitwaye Paka-shume katika hadithi ya “Shetani Hana Hatia” anaadhibiwa kwa uovu wake. Hali ya kuadhibu wahusika katili pia inapatikana katika ngano.

Isitoshe, imebainika kuwa kitabu cha Steere kinasawiri Liyongo kama mhusika katili ambaye anawanyanyasa watu. Hali hii ni tofauti na jinsi vitabu vya Matundura (2001) na Mulokozi (1999) vinamsawiri Liyongo. Katika vitabu hivi Liyongo anasawiriwa kama mtetezi wa watu. Matundura (2001) anaeleza kisa

ambacho Liyongo alimwokoja kijana mmoja aliyeshambuliwa na mamba. Hali hii inaonyesha kuwa wakati wa ukoloni baadhi ya wakoloni waliwasawiri mashujaa wa Kiafrika kwa njia hasi. Ndiposa, Steere (1870) anamsawiri Liyongo kwa namna hasi. Hata hivyo, baadhi ya waaafrika waliwasawiri mashujaa wao kwa njia chanya hasa baada ya nchi mbalimbali kujinyakulia uhuru. Hali hii inaonekana katika vitabu vya Mulokozi (1999) na Matundura (2001).

Isitoshe, mhusika jahili huweza pia kuwa mhusika shujaa. Tukiangazia udhaifu wa shujaa, mhusika jahili huweza kumshinda shujaa na kuwa ‘shujaa’ kwa watu wengine. Mfano ni ngano ya “Liyongo”. Katika ngano hii Liyongo anauliwa na mwanawe. Hali kadhalika, imebainika kuwa shujaa si lazima afe bali anaweza kuwashinda maadui wake wote. Mfano ni Abunuwasi katika ngano ya “Abunuwasi na Wezi Wawili” na Maskini katika hadithi ya “Uganga wa Pete”.

5.3 Mapendekezo

Utafiti huu umechunguza mitindo, miundo, wahusika na maudhui katika hadithi fupi na ngano. Ni mapendekezo yetu kwamba utafiti ufanywe katika tanzu zingine haswa riwaya. Hii ni kwa sababu kumekuwa na kuhitilafiana kuhusu asili ya riwaya. Kuna wale wanaoamini kuwa riwaya ni zao la kistari la moja kwa moja kutoka tanzu zingine kama vile hadithi fupi na ngano. Kwa upande mwingine, wataalamu wengine wanaamini kuwa utanzu huu wa riwaya ulichipuka kivyake.

Aidha, katika utafiti huu tumebaini kuwa kuna hadithi zilizoonyesha ukuruba na ngano. Mfano ni hadithi ya “Uganga wa Pete” iliyoonyesha sifa zinazofanana na

ngano. Utafiti wa baadaye unaweza kuangazia hadithi hizi na kuzilinganisha na ngano. Aidha, mtafiti anaweza kuwahoji waandishi wa hadithi zilizoonyesha sifa zinazofanana na ngano ili kubaini ikiwa waliathiriwa na ngano kwa namna moja au nyingine katika uandishi wao.

Mwishowe, utafiti huu umejiegemeza kwenye hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Utanzu wa hadithi fupi umekuwa na mabadiliko mengi tangu wakati wa ukoloni. Ni matumaini yetu kuwa utafiti wa baadaye unaweza kuangazia sifa za hadithi fupi za kale na kuzilinganisha na ngano.

5.4 Hitimisho

Sura hii imeangazia muhtasari wa sura na matokeo ya utafiti kwa mujibu wa malengo. Hali kadhalika, mtafiti amependekeza tafiti ambazo zinaweza kufanywa baadaye kuhusu ngano na hadithi fupi.

MAREJELEO

- Adagala, K. na Kabira, W. M. (1985). *Kenyan Oral Narratives: A Selection*. Nairobi: East African Publications Ltd.
- Andwoa, O. (2018). *Trickster Ambivalence in Ansa's Praising the Lord Plus One*. Journal of Religion and Film. University of Toronto.
- Aylestock, N. (2009). *Supreme Heroes*. S.1: Universe Sn1
- Camara, S. (1986). *Tale Sin the Night: Toward Anthropology of the Imaginary*. In Vana Folklore. Ed Alan Dundes: Moulon and Co.
- Campbell, J. (2004). *The Hero with a Thousand Faces* (3rd ed.). Princeton: Princeton University Press.
- Canonici, N. N. (1995). *Tricksters and Trickery in Zulu Folktales* (Haijachapishwa Chuo Kikuu Cha Kwazulu- Natal, Durban, South Africa).
- Chemutai, J. M. (2016). *Mtindo katika Hadithi Fupi ya Kisasa*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya.
- Child, P. and Fowler, R. (Wah) (2006). *The Routledge Dictionary of Literary Terms*. London: Routledge.
- Feldkamp, J. K. (2008). *Giving the Devil His Due: The Emergence of the Fallen Hero in English Literature*. (Haijachapishwa). Eastern Michigan University, Michigan.
- Frye, N. (1957). *Anatomy of Criticism: Four Essays*. New Jersey: Princeton University Press.

- Frye, N. (1976). *Spiritus Mundi: Essays on Literature, Myth and Society* (vol. 3). Taylor and Francis.
- Frye, N. (1982). *The Great Code: The Bible and Literature* (vol. 19). Toronto: University of Toronto Press.
- Gathara, K. F. (2015). *Taswira ya Jagina katika Tendi: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Nabii Isa*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi, Kenya.
- Gatricya, R. (2014). *The Archetypes of Hero and Hero's Journey in Five Grimm's Fairy Tales*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Yogyakarta, Yogyakarta, Indonesia.
- Gichamba, J. M. (2005). *Sifa za Mashujaa na Umuhimu wao katika jamii zao: Ulinganifu wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi, Kenya.
- Guerin, W. (2005). *A Handbook of Cultural Approaches and the Writing Process*. Newyork: Oxford University Press.
- Hagan, J. (1988). *Influence of Folktales on the Marriage of Anansewa: A Folkloric Approach*. *An African Journal of New Writing*. No's 27 and 28.
- Hornby, A. S. (2006). *The Advanced Learners Dictionary of Current English*. London: Oxford University Press.
- Hull, J. (1981). *Narrative First: Where Story is Always King*. Galicea: Baylor University of Rhode Island.
- Iribe, M. (2007). *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

- Jacobi, J. (2000). *The Psychology of Jung: An Introduction with Illustrations*. United States: Yale University Press.
- Jung, C. G. (1959). *The Archetypes and Collective Unconscious. Collected Works*: Trans. RFC. Hull. Ed. Herbert Read.
- Jung, C. G. (1968). *Psychology and Alchemy. Collected Works, Vol 12*. Trans by RFC. Hull.
- Jung, C. G. (1975). *The Structure and Dynamics of the Pysche. Collected Works*: Vol 8. Trans. RFC Hull. Princeton: Princeton University Press.
- Kemunto, J. (2015). *Uhakiki Linganishi wa Sifa za Mashujaa: Sakawa na Fumo Liyongo*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi, Kenya.
- Kenguru, P. J. (2013). *Athari ya Fasihi Simulizi katika Riwaya ya Utubora Mkulima*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi, Kenya.
- Kingei, G. K. na Kisovi, M. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Knappert, J. (1970). *Myths and Legends of the Swahili*. Nairobi: Heinemann Education Books.
- Konrad, Z. (1983). *Aspects of Trickster: Form, Style and Meaning in Oral Narrative Performance* (Haijachapishwa) Chuo Kikuu Cha Winconsin, Madison.
- Kunene, D. P. (1985). Journey as a Metaphor in African Literature. The Present State/ Le'tat present. Ed. Stephen Arnold. Washington: Three Continents Press, 189-215.

- Landmark, M. (2006). *Dream of a Thousand Heroes: The archetypal Hero in Contemporary Mythology with Reference to The Sandman by Neil Gaiman*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha South Africa, South Africa.
- Larsen, B. (2018). *Archetypal and Fourth Gospel: Literature and Theology in Conversation*. Bloomsburry Publishing.
- Liabenow, A. (2014). *The Significance of the Numbers Three, Four and Seven in Fairytales, Folklore and Mythology*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Grand Valley, Michigan, U. S.
- Makena, M. E. (2018). *Uwasilishaji wa Maudhui katika Hadithi Fupi Teule za Said A. Mohammed*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi, Kenya.
- M'Ngaruthi, T. K. (2007). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Makgamatha, P. M. (1993). *Characteristics of the Northern Sotho Folktales*. Johannesburg: Perkson Publishers.
- Marete, R. G. N. (1992). *An Anatomy of Third World Literature: Northrop Frye's Theory of Modes in Post-Colonial Context*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Massey, New Zealand.
- Masoud, S. K. (2015). *Matumizi ya Motifu ya Nambari katika Ngano za Ki-pemba*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Dodoma, Dodoma, Tanzania.
- Matteru, M. L. (2003). "Fasihi Simulizi na Uandishi wa Kiswahili' katika makala ya semina ya Kimataifa ya uandishi wa Kiswahili 111: Fasihi. Dar-es-Salaam: TUKI.
- Matundura, B. (2001). *Mkasa wa Shujaa Liyongo*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

- Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks, Graphics and Publishing Centre.
- Mbatiah, M. (2007). *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Focus Publishers.
- Mbatiah, M. (2016). *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mberia, K. (1989). *Fumo Liyongo*. Mulika. Na. 21. Uk. 21-23
- Mbogo, E. (2011). *Sundiata*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mbuthia, E. M. na Iribemwangi, P. I. (2014). *An Analysis of Stylistic Trends in Published Kiswahili Short Story Genre*. Journal of Education and Practice, 5(8).
- Mc Mahon, J. W. (1990). *Psychology and You*. New York: West Publishing Center.
- Mc Onyango, O. (2006). *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Focus Publishers.
- Milton, J. (2001). *Paradise Lost*. New York: Oxford University Press.
- Mligo, E. J. (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantiki*. Dar- es- Salaam: Ecnemical Gathering.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mohochi, E. S. (1995). *Fani katika Hadithi Fupi*. (Haijchapishwa). Chuo Kikuu Cha Egerton, Kenya.

- Mohochi, E. S. (1997). “Hadithi Fupi: Utanzu Uliopuuzwa”. Mulika Nambari 24. Dar- es- Salaam: TUKI.
- Mose, E. N. (2005). *Taashira za Kifo katika Tamthilia za Mukwava wa Uhehe, Amezidi, Kilio cha Haki na Visiki*. (Haijachapishwa) Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya.
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: EAEP.
- Mukopi, L. M. (2005). *Hadithi Fupi za Kiswahili kama Utanzu Mahuluti*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya.
- Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Cha Huria.
- Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mulokozi, M. M. (2009). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Muusya, J. K. (2012). Mandhari katika Hadithi Fupi: *Ulinganishaji wa Diwani za Pendo la Heba na Hadithi Nyingine na Mizungu ya Manabii na Hadithi Nyingine*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya.
- Mwangi, I. (2007). *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mwanzi, H. (1987). *Notes on Chameleon’s Second Delivery*. Nairobi: Heinemann Publishers. Nairobi: Vide – Muwa Publishers.
- Mwinyi, H. Y. (2015). *Taswira katika Ngano za Kiswahili kutoka Wilaya ya Kusini Unguja Zanzibar*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Dodoma, Dodoma, Tanzania.

- Nawe, N. (2018). *Taswira ya Fisi katika Ngano za Kiiraqw*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania.
- Ngongolo, M. J. (2015). *Usawiri wa Mwanamke katika Hadithi za Magazeti ya Uduku*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Dodoma, Dodoma, Tanzania.
- Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule ya Sekondari*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nyamsenda, J. C. (2015). *Ushujaa wa Shujaa wa Motifu za Safari za Msako katika Ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibari*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Tanzania, Tanzania.
- O'Grady, J. (2008). *Interview with Northrop Frye* (vol. 24) Toronto: University of Toronto Press.
- Ogamba, D. B. (2015). *A Study of Archetypal Symbols in Selected Igbo Folktales*. Emenyonu, Free Town: E. N. Eustace PALMER.
- Okwepho, I. (1992). *African Oral Literature: Backgrounds, Character and Continuity*. Indiana: Indiana University Press.
- Olrik, A. (1965). *Epic Laws of Folk Narratives. The Study of Folklore*, 129, 134.
- Onchangu, R. N. (2013). *Mtindo katika Riwaya na Hadithi Fupi za Clara Momanyi*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi, Kenya.
- Oyoyo, J. O. (2013). *Uhakiki wa Fani katika Ngano tano za Kiswahili*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi, Kenya.

Park, J. K. P. (2004). *The Oral Written Interface in the Swahili Fictional Prose*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi, Kenya.

Paul, W. (1992). *Notes on Bassa Folklore*. Abuja: Council of Arts and Culture.

Poe, E. A. (1842). *The Mask of Red Death: A Fantasy*. Philadelphia: Graham's Magazine.

Poe, E. A. (1842). *The Pit and The Pendulum: Short Story*: Strelbytskyy Multimedia Publishing.

Poe, E. A. (1843). *The Black Cat: Short Story*. New York: Haper Collins Canada.

Poe, E. A. (1843). *The Tell-Tale Heart*. California: Create Space Independent Publishing Platform.

Poe, E. A. (1844). *The Premature Burial*. Philadelphia: Philadelphia Dollar Newspaper.

Propp, V. (1978). *The Morphology of the Folktale*. Austin: University of Texas Press.

Propp, V. (1984). *Theory and History of Folklore*. Minneapolis: University of Minnesota.

Russel, D. L. (2009). *Literature for Children: A Short Introduction*. Boston: Ferris State University.

Sanja, L. (2011). *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Focus Publishers.

Sengo, T. Y. (1982). *Fasihi*. Dar- es- Salaam: Nyenza Publications Agency.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar- es- Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (1997). *The Significance of Journey in Folktales from Zanzibar*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar- es- Salaam: KAUTU Ltd.

Shabaan, R. (1946). *Kufikirika*. Nairobi: Nelson Publishers.

Shabaan, R. (1951). *Kusadikika*. Nairobi: Nelson Publishers.

Shore, J. (1993). *Analysing Novel and Short Stories*. New York: Texas University.

Solovyeva, N. V. (2015). *Typical Features of the Folktale Narrative Style*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Moscow, Moscow, Russia.

Steere, E. (1870). *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*. London: William Clowes and Sons.

Synder, B. (2005). *Save the Cat: The Last Book on Screen Writing You'll Ever Need*. Studio City, CA: Michael Wiese Productions.

Timammy, R. na Swaleh, A. (2013). Wanawake Wachukua Hatua Nyingine: Analysing Women Identities in Kiswahili Short Stories. *Swahili Forum* 20 (2013) uk. 102-114.

- Vogler, C. (2007). *The Writer's Journey: Mythic Structure for Writer's*. Studio City: Michael Wiese Productions.
- Wa Mutiso, K. (1999). *Sifa ya Majagina Buddha na Muhammed*. Swahili Kolloquim: Universtat. Bayreuth. Mei 14-15
- Wa Mutiso, K. (2005). *Hurafa ya Uyakiniifu katika Hamziyah*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi, Kenya.
- Wa Mutiso, K. (2014). Number Symbolism (no's 1, 4, 7 and 1000) in Swahili Poetry: the case of Utenzi wa Fatumah. *Kiswahili*, 2014, 77. 1.
- Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundations.
- Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers.
- Wilkinson, L. C. R. (2017). *A Blur of Potentialities: The Figure of the Trickster in the Works of Elizabeth Bomen, Elizabeth Taylor, Iris Murdoch and Munel Spark*. University of Exeter.